# Nipashe

Jumatano Januari 22, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580134

The Guardian digital

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Wazazi 17,000 kusakwa watoto kukacha kujiunga na sekondari

UKURASA 3




UKURASA 13

# TCRA yatoa msimamo uzimaji laini za simu



**YAWEKA** bayana makundi yatakayoguswa, wengi wazidi kumiminika kusajiliwa, mtandao wa Nida waleta mambo...*Endelea ukurasa wa 2*

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Mhandisi James Kilaba


## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**POLISI YAZUIA MKUTANO WA NDANI WA CHADEMA**

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, limeuzuia mkutano wa ndani wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo...

UKURASA WA 4

**SHERIA KUASILI WATOTO YAPIGIWA CHAPUO**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ameshauri kufanyika...

UKURASA WA 26

**MAGUFULI AAHIDI UCHAGUZI HURU, HAKI MWAKA 2020**

RAIS John Magufuli, amesema Serikali imejipanga kuhakikisha uchaguzi mkuu wa mwaka huu utafanyika...


## TUME YAFUTA VYUO VIKUU 6

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Aliyesamehewa na Rais auawa tukio la ujambazi

UKURASA 2


MICHEZO SAMATTA APEWA ZIGO KUBWA ASTON VILLA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# TCRA yatoa msimamo uzimaji laini za simu

**Na Waandishi Wetu**

SIKU moja baada ya ukomo wa tarehe ya mwisho iliyowekwa na serikali kukamilisha usajili wa laini za simu kwa alama za vidole, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imeeleza namna ilivyoanza kuzima kwa mafungu.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, James Kilaba, akizungumza katika mahojiano maalum na kituo kimoja cha runinga jijini Dar es Salaam, alisema walianza kuzima laini hizo kuanzia juzi saa 4:00 usiku.

Alisema kuna watu 656,091 ambao walianza kuzimiwa laini za simu ambao wana namba za utambulisho wa taifa, lakini mpaka juzi walikuwa hawajaenda kujisajili. Pia alisema kundi lingine ni watu 318,950 wenye namba za utambulisho wa taifa waliojisajili mwanzoni, lakini si kwa alama za vidole.

"Hawa wameshaitwa mara kadhaa kwenda kujisajili upya kwa alama za vidole, lakini hawajajitokeza. Kundi hili hawana sababu ya msingi ya kutozimiwa laini zao," alisema Kilaba.

Alisema wanachofanya ni kusitisha huduma kwa watumiaji wa laini ambao hawakujisajili kwa alama za vidole kwa muda waliokuwa wamepanga.

Kilaba alisema laini iliyofungiwa itakuwa na uwezo wa kupokea ujumbe mfupi wa maneno unaoeleza taratibu za kusajili laini yake.

"Uhuishaji wa laini za simu kwa wale ambao wameshindwa kujisajili kwa alama za vidole kwa muda ambao tumeweka, wamefungiwa lakini usajili wa laini mpya unaendelea katika maeneo mbalimbali nchini," alisema.

Kilaba alisema hawawezi kuzima laini milioni tano kwa wakati mmoja isipokuwa wanatoa nafasi ili watu wapate nafasi ya kwenda kuhuisha kwenye mitandao yao ya simu.

"Jumla ya watu 975,041 wanazimiwa laini zao kwa mafungu kuanzia leo (juzi) na hatuwezi kuwazimia wote kwa wakati mmoja wakati tunataka wazihuwishe," alisema Kilaba.

Alisema lengo la TCRA ni kumaliza changamoto za udanganyifu na wizi unaofanywa na watumiaji wa laini za simu kwa kujiaminisha kuwa hawawezi kukamatwa.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), Arnold Kihaule, aliiambia Nipashe kuwa hadi sasa mamlaka hiyo imeshatoa asilimia 80 ya namba za utambulisho ya waliojitokeza kujisajili.

Katika baadhi ya maeneo ambako Nipashe limefika, baadhi ya watu wamezimiwa simu zao huku wengine wakiendelea kupata mawasiliano kama kawaida licha ya kutojisajili.

Jijini Dar es Salaam, baadhi ya watu waliozimiwa simu zao walisema hawawezi kutuma ujumbe wala kupiga simu, hivyo simu zao hazina kazi yoyote tena.

Aidha, katika maeneo jijini Dodoma idadi ya wananchi wanaotafuta vitambulisho vya Taifa

INAENDELEA UK 8



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akitoa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara (Fungu 52), kwa kipindi cha nusu mwaka 2019/2020, kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Aliyeachiwa na Rais auawa kwa ujambazi

**Na Godfrey Mushi, MWANGA**

MFUNGWA aliyeachiwa huru kwa msamaha wa Rais John Magufuli kutoka Gereza Kuu la Karanga mkoani Kilimanjaro, ameuawa kwa kushambuliwa na wananchi wenye hasira kali, baada ya kudaiwa kupora Sh. milioni sita nyumbani kwa mfanyabiashara maarufu, Hussein Minja.

Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Thomas Apson, alithibitisha kuwa mtu aliyeuawa kwa kipigo juzi usiku katikati ya Mji wa Mwanga, na kuwa ametambuliwa kwa jina moja la Tillya.

Apson alieleza Nipashe kuwa mfungwa huyo akiwa na wenzake watatu, walivamia nyumbani kwa mfanyabiashara Minja maarufu kama 'Hussein mafriji' na kumtisha kwa mapanga kutoa fedha zote alizokusanya dukani kisha wakafanikiwa kuchukua Sh. milioni sita.

Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Salum Hamduni, alipotafutwa kueleza undani wa tukio hilo, alijibu kwa ujumbe mfupi wa maandishi ya simu ya mkononi (SMS) akisema: "Nipo nje ya ofisi yangu kwa sasa. Nikimaliza kikao nitakutafuta."

Inadaiwa kuwa baada ya kupora fedha hizo ambazo ni mauzo ya vifaa vya kielekroniki katika duka lililopo mkabala na nyumba yake, watuhumiwa watatu wa ujambazi walifanikiwa kutoroka na Sh. milioni sita, lakini 'Tillya' alibaki na Sh. milioni sita, ambazo zilikamatwa alipouawa.

Kwa mujibu wa Apson: "Hao watu walikuwa wanne na huyo mfungwa aliyejulikana kwa jina moja la Tillya aliuawa na wananchi muda mfupi, baada ya kubaki kwa Hussein Mafriji, akimlazimisha aongeze pesa kwa sababu milioni sita haziwatoshi kugawana.

"Baada ya tukio hilo wananchi wenye hasira walimkamata na kumshushia kipigo hadi kupoteza maisha. Nimepewa taarifa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwamba bado Polisi wanaendelea na uchunguzi kuhusu tukio hilo ili waweze kuwasaka na kuwakamata majambazi watatu waliotokomea na fedha hizo." Alisema baada ya Tillya na wenzake watatu kutekeleza tukio hilo la ujambazi, wananchi wenye hasira kali walimvamia na kuanza kumshambulia na kumuumiza vibaya.

"Askari Polisi waliokuwa doria na waliokuwa kituoni waliwahi katika tukio hilo na kufanikiwa kumuokoa Tillya asiendelee kushambuliwa, lakini alifariki muda mfupi," alisema.

Akizungumza na Nipashe, Mfanyabiashara Minja alisema majira ya saa 3 usiku alitoa msikitini kuswali aliingia ndani akala chakula halafu akaingia bafuni kuoga.

"Nilifika chumbani nikawasha taa kisha nikaingia bafuni kwa ajili ya kuoga, nimetoka kuoga nashangaa taa ya chumbani imezimwa, na ghafla wakatokea watu wanne wakasema nipo chini ya ulinzi natakiwa kutoa fedha," alisema.

"Walinipiga wakanikata sikio, kichwani na kunitoboa na bisibisi wakitaka nitoe fedha, niliitoa shilingi 12 wakagawana na mwisho wale watatu walitokea dirishani... walikokuwa wametoboa, akabaki mmoja ambaye ni kiongozi wao akitaka nitoe fedha zaidi nikamsihi aniache kwa kuwa sina fedha zaidi ya hizo," alisema.

Minja alisema wakati wanamshambulia, alipigiwa simu na mmoja wa ndugu yake na aliiweka wazi huku akieleza amevamiwa na majambazi anahitaji msaada na ndipo polisi walijulishwa na huku wananchi wakianza kusogea eneo hilo, na kwamba jambazi huyo alivyotoka walimshambulia.

## Polepole ataka mashtaka kabla ya mchujo uchaguzi

**Na Enock Charles**

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humprey Polepole, amewataka wanachama kuwashtaki kwenye chama watu wenye makosa mbalimbali ya kiuadilifu kabla ya kipindi cha uchaguzi mkuu.

Lengo la kufanya hivyo ni kupatikana mapema katika mchakato wagombea wa nafasi mbalimbali na kuepusha migogoro au migawanyiko ndani ya chama.

Akizungumza na wanachama wa chama hicho Kigamboni jijini Dar es Salaam hivi karibuni, alisema kuna tabia ya watu kupeleka tuhuma mbalimbali kuhusu wanachama wenzao kwa kuchelewa au kusubiri mchakato wa uchaguzi uanze, hivyo kuwagawa wanachama na kusababisha

wasuse kupiga kura na kuleta ushindi hafifu kwa chama hicho.

"Hiki chama nacho huwa mnachelewa kuchukua hatua kwa watu. Tunasubiri uchaguzi unafika mwezi mmoja kabla ya kupiga kura ndiyo tunamsema mtu fulani mbaya na mimi wakati huu nitamsumbua sana Mzee Philip Mangula (makamu Mwenyekiti wa CCM Bara). nitamwambia Mzee kamata wezi wote na wabadhirifu wa fedha ili vijana waanze kuwang'ong'a kuwa ni wezi," alisema.

"Siyo mnachelewa mpaka mwezi wa nane ndiyo mnaanza kusema huyu mwizi wananchi watatushangaa watatuambia mlikuwa wapi kumsema toka mwanzo," aliongeza.

Polepole alikumbusha kilichotokea ndani ya CCM mwaka 2015 kwamba wapo waliokuwa wameteuliwa na chama kugombea nafasi flani na ghafla wanajitokeza watu kumshtaki mhusika.

Kwa mujibu wa Polepole, wako viongozi wakubwa lakini si waadilifu na ni watovu wa nidhamu na wezi, hivyo watoswe katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, baada ya makosa yao kujulikana na kushtakiwa ili kukiwezesha chama kuibuka na ushindi mkubwa.

## HABARI KITAIFA

## Polisi yazuia mkutano wa ndani wa Chadema

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA.**

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga limeuzuia mkutano wa ndani wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), baada ya kutokea sintofahamu kati ya viongozi wa chama hicho kikuu cha upinzani nchini.

Hatua hiyo ilichukuliwa kufuatia kitendo cha Katibu Mwenezi wa chama hicho Jimbo la Shinyanga, Charles Shigino, kuandika barua kwa Jeshi hilo akidai kutoufahamu.

Kadhalika, Shigino alidai kwenye barua hiyo kuwa mkutano huo unahatarisha hali ya usalama.

Akizungumzia kuzuiwa mkutano huo, Mwenyekiti wa Chadema Mkoa wa Shinyanga, Emmanuel Ntobi, alisema walitarajia kufanya mkutano huo kwa ajili ya kupeana maelekezo ya chama kutoka ngazi za juu sambamba na mikakati ya kukijenga chama kuelekea kwenye uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Alisema wakati akijiandaa na mkutano, walikuta askari Polisi wakiwa wametanda kwenye eneo ambalo walipanga kuufanyia katika Hoteli ya Ibanza Kata ya Ibinzamata Mjini Shinyanga, na kuambiwa hawawezi kuufanya kutokana na taarifa walizopewa za hali ya kiusalama.

"Wakati tukijiandaa na mkutano huo ndipo Jeshi la Polisi likatuzuia kutoufanya na tulipohoji ni kwanini, tukaambiwa kuwa Katibu Mwenezi wetu ameandika barua Polisi ya kutoutambua mkutano, na kwamba una hatarisha hali ya usalama, ndipo kuamua kuuhairisha hadi siku nyingine," aliongeza Ntobi.

Alisema kutokana na katibu mwenezi huyo kukiuka katiba ya chama na kuonyesha utovu wa nidhamu pamoja na kukisaliti chama, Baraza la Uongozi la Mkoa limeadhimia kumsimamisha nafasi zake za uenezi Jimbo la Shinyanga na ujumbe wa Mkutano Mkuu Kata ya Ngokolo.

Shigino, alikiri kuandika barua kwa Jeshila Polisi kuzuia mkutano huo kwa madai ni batili na umekiuka katiba ya chama, akidai hakupewa taarifa juu ya kuwapo kwa mkutano huo wakati yeye ndiye mratibu wa mikutano yote, ndipo akaamua kuuzuia.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga, Deborah Magiligimba, alithibitisha kuuzuia mkutano, baada ya kutokea kutokuelewana kati ya viongozi wa chama hicho kwa kuwa ni hatari kiusalama.

Alisema Jeshi hilo liliwapa sharti la kuelewana kwanza ndipo waruhusiwe kufanya mkutano huo tena.

## Wazazi 17,000 kuanza kusakwa watoto kukacha kidato cha kwanza

**Na Lucy Ogutu, Mtwara**

SERIKALI ya Mkoa wa Mtwara imesema itaanza kuwasaka wazazi ambao watoto wao wameshindwa kuripoti shuleni kuanza kidato cha kwanza mwaka huu.

Wanafunzi hao wa kidato cha kwanza wameshindwa kuripoti shuleni, huku idadi ya waliofaulu ni zaidi ya 20,000, hivyo setikali kuagiza wazazi wote waliogoma kupeleka watoto shuleni kukamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, alitoa agizo hilo baada ya kufanya ziara katika Manispaa ya Mtwara Mikindani na kukuta wanafunzi wa kidato cha kwanza zaidi ya 3,000 hawajaripoti shuleni.

Amesema matarajio ya mkoa ni watoto 20,400 na ndiyo waliyofaulu mtihani wa darasa la saba na kutakiwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu.

Alisema hali hiyo haiwezi kuvumiliwa na kusisitiza kuwa tangu shule zifunguliwe zaidi ya wiki tatu, lakini wanafunzi wa kidato cha kwanza walioripoti shule maudhurio hayaridhishi.

Alisema asilimia 75 ya wanafunzi hao hawajaripoti shule na kusisitiza ifikapo Jumatatu ijayo, wazazi wote waliogoma kupeleka watoto shule sheria ichukue mkondo wake dhidi yao, huku akisisitiza nia ya serikali ya kutoa elimu bure ni kuona kila Mtanzania anapata elimu ya msingi na sekondari.

Byakanwa ameshawaagiza wa vijiji, vitongoji na mitaa kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kuhakikisha wazazi hao wanakamatwa na kufikishwa mahakamani.

Kwa upande wake Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mtwara, Germana Mng'aho, alisema takwimu zilizokusanywa na ofisi ya elimu mkoa inaonyesha kuwa hadi Januari 17, mwaka huu watoto walioripoti shule hasa sekondari ni wachache.

Alisema ofisi yake imejipanga kutoa ushirikiano ili kuhakikisha mchakato wa kuwafatilia watoto wote waliofaulu kujiunga kidato cha kwanza, lakini hawajaripoti unafanikiwa.



Katibu Mtendaji wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Prof. Charles Kihampa, akizungumza na wanahabari, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## TCU yafuta vyuo vikuu sita

**Na Romana Mallya**

TUME ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), imefuta vyuo vikuu sita na vituo vya vyuo vitatu kwa sababu ya kushindwa kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Kati ya vyuo hivyo, viwili wamiliki wake waliomba wenyewe vifutwe ambavyo ni Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mkuu Yakobo (AJUCo) na Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Kardinali Rugambwa (CARUMUCo).

Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam.

Prof. Kihampa alisema TCU imeridhia maombi ya wamiliki kufuta vyuo vikuu vishiriki viwili na vituo vitatu vya vyuo vikuu.

"Tume imeridhia maombi mengine ya kufutwa kwa vituo vishiriki vitatu kwa kusitisha utoaji wa mafunzo ambavyo ni Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji-Kituo cha Dar es Salaam (TEKU-Dar es Salaam Centre).

"Chuo Kikuu cha Mt. Yohana cha Tanzania-kituo cha Mt. Marko (SJUT- St. Mark's Centre) na Chuo Kikuu cha Jomo Kenyatta cha Kilimo na Teknolojia- Kituo cha Arusha (JKUAT) cha Arusha. Alisema tume kupitia kikao chake cha cha 97 kilichofanyika juzi, imeridhia maombi yaliyofanywa na wamiliki wa vyuo na vituo hivyo kusitisha utoaji wa mafunzo.

Pia Prof. Kihampa alisema TCU imefuta hati za usajili za vyuo vikuu vitatu na Chuo Kikuu Kishiriki kimoja.

Alivitaja vyuo hivyo kuwa ni Chuo Kikuu Kishiriki cha Josiah Kibira (JOKUCo), Chuo Kikuu cha Mlima Meru (MMU), Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Tiba na Teknolojia (IMTU) na Chuo Kikuu cha Bagamoyo.

Alisema licha ya tume kutoa ushauri na mafunzo ya namna ya mbalimbali za kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia pamoja na muda wa kufanya maboresho kama ilivyotakiwa.

"TCU imedhihirisha kuwa vyuo hivyo havina uwezo wa kujiendesha hata vikipewa muda zaidi. Tume katika vikao vyake vya 89, 91, 92 na 97 vilivyofanyika kati ya mwezi Agosti, 2019 na Januari 2020 imefuta hati za usajili za vyuo hivyo,"alisema.

Prof. Kihampa alisema mwaka 2018 TCU ilitoa muda na kuelekeza wanafunzi 2,607 waliokuwa wakisoma vyuo hivyo wahamishwe hadi mwezi Desemba 2018.

Pia alisema kati ya mwezi Oktoba 2016 na Januari 2017 TCU ilifanya ukaguzi maalum wa kitaaluma kwa taasisi zote 64 za vyuo vikuu, vyuo vikuu vishiriki na vituo vya vyuo vikuu.

Alisema matokeo ya ukaguzi yalibainisha kasoro mbalimbali katika uendeshaji wa vyuo vikuu na vyuo 45 vilikutwa na kasoro ndogo na kupewa ushauri na vilirekebisha katika kipindi kifupi na kuendelea na utoaji elimu.

"Hadi mwezi Oktoba 2019, vyuo vikuu vinane kati ya 19 vilivyositishwa udahili viliweza kufanya marekebisho makubwa na kuruhusiwa kudahili ambavyo ni Chuo Kikuu cha Umoja wa Afrika Tanzania (UAUT) na Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji (TEKU).

Vingine ni Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mkuu Mihayo cha Tabora (AMUCTA), Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala Tanzania (KIUT), Chuo Kikuu Kishiriki cha Marian (MaRUCo) na Chuo Kikuu Kishiriki cha Uhandisi na Teknolojia cha Mt. Yosefu (SJCET).

Alitaja vingine ni chuo Kikuu Kishiriki cha Kikristo cha Tiba Kilimanjaro (KCMUCo) na Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Stefano Moshi (SMMUCo).

Prof. Kihampa alisema tume imeridhishwa na maboresho yaliyofanywa chuo Kikuu Kishiriki cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Mt. Fransisko (SFUCHAS) kilichorekebisha upungufu wa ubora na kuruhusiwa kuanzia juzi kudahili.

Pia alisema TCU imeendelea kusitisha udahili wa wanafunzi wapya kwa chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa (SEKOMU) na kupewa miezi sita kukamilisha maelekezo.

## HABARI KITAIFA

# Sheria kuasili watoto yapigiwa chapuo

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ameshauri kufanyika kwa mabadiliko ya sheria ya kuasili watoto ili kuwasaidia watoto 900,000 wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Ushauri huo aliutoa jana alipokuwa akiwasilisha taarifa ya miezi sita ya utekelezaji ya Wizara hiyo kwa Kati ya Bunge ya Huduma za Maendeleo ya Jamii.

Waziri Mwalimu alishauri sheria ya kuasili mtoto kufanyiwa marekebisho ili kuwasaidia na kupunguza idadi kubwa ya watoto zaidi ya 900,000 wanaoishi kwenye mazingira magumu.

"Sheria hii ni ngumu nchini tofauti na nchi za jirani kama Ethiopia, ,Kenya na baadhi ya nchi zingine... ina mashariti magumu na haijaweka masharti rahisi kwa wazawa kumsaili mtoto na kukaa naye," alisema.

Alibainisha kuwa kwa taarifa za wizara hiyo zilizopo, Julai hadi Desemba mwaka 2019, ni watoto 13 tu ndio waliopata huduma ya kuasiliwa kati ya watoto 900,000 wanaoishi katika mazingira magumu nchini.

Pia, alisema sheria hii ikifanyiwa marekebisho, itasaidia kupunguza wizi wa watoto mitaani na hospitalini kwa sababu itamruhusu mtu kumchukua mtoto kwa masharti rahisi na kukaa naye kama mtoto wake wa kumzaa.

Alisema katika mabadiliko hayo, wananchi wazawa watapewa kipaumbele katika kuwaasili watoto hao tofauti na watu kutoka mataifa ya kigeni.

Alisema masharti ya kuasili mtoto yapo kwenye sheria ya mtoto ya mwaka 2019 na imeainisha masharti ya Watanzania na wageni wanaohitaji kuasili mtoto hapa na nje ya nchi pamoja na adhabu zake kwa wanaokiuka masharti yaliyowekwa kisheria.

Mbunge wa Chemba, Juma Nkamia, alisema Tanzania ni kubwa na kuna idadi kubwa ya watu, hivyo sheria ikifanyiwa mabadiliko itasaidia watoto hao kutunzwa na familia zinazohitaji watoto.

Nkamia alisema watoto hao ni nguvu kazi ya Taifa, hivyo wakitunzwa wataishi mazingira waliozaliwa nayo pamoja na kulisaidia taifa kiuchumi kwa siku za mbele.

Mbunge wa Viti Maalumu, Salma Kikwete, alishauri jamii kuendelea kutunza watoto wao hasa kuhakikisha wanalindwa kila eneo ili kuwaepusha na watu wabaya.

Alisema kutokana na uwapo wa taarifa za watoto kufanyiwa vitendo vya ukatili na baadhi ya watu, kila familia ichukue jukumu la kuwalinda ili kukomesha vitendo hivyo.

Mbunge wa Kinondoni, Maulid Mtulia, alisema sheria hiyo inatakiwa kuwa na mazingira rafiki kwa watu wote ili kuwasaidia watoto wanaoasiliwa kuishi katika mazingira bora.




Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri (katikati), akiongoza zoezi la utoaji wa taulo za kike katika Shule ya Sekondari Ndono, iliyopo wilayani Uyui, kupitia kampeni ya Namthamini inayoendeshwa na vituo vya East Africa Television na Redio kwa mwaka wa nne mfululizo. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Gift Isaya Msuya. **PICHA: EATV**

# Rais ateua wenyeviti, wakuu taasisi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amefanya uteuzi wa wenyeviti wa bodi nne, Katibu Mtendaji wa Baraza la Biashara la Taifa (TNBC) na Mkuu wa Chuo cha Maji.

Taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, ilisema kuwa uteuzi huo ulianza Januari juzi.

Katika uteuzi huo, taarifa hiyo ilisema Rais Magufuli amemteua Prof. Maurice Mbago kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA). Prof. Mbago anashika wadhifa huo kwa kipindi cha pili.

Pia taarifa hiyo ilieleza kuwa Rais Magufuli amemteua Dk. Masatu Chiguna kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) akichukua nafasi ya Prof. Ninatubu Lema ambaye uteuzi wake ulitenguliwa na bodi kuvunjwa.

Sambamba na uteuzi huo, Rais amemteua Prof. Zacharia Mganilwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL). Prof. Mganilwa ni Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT).

Aidha, taarifa hiyo ilieleza kuwa Mariam Alu Nkumbi ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Mkonge Tanzania.

Katika hatua nyingine, Rais Magufuli amemteua Dk. Godwill Wanga kuwa Katibu Mtendaji wa TNBC. Kabla ya uteuzi huo Dk. Wanga alikuwa Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Aidha, Rais Magufuli amemteua Dk. Adam Karia kuwa Mkuu wa Chuo cha Maji.

# Waziri akerwa bei juu mbolea

**Na Mwandishi Wetu, SONGWE**

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, ameelezea kukerwa na bei ya mbolea kuwa juu huku akiitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kupanga na kusimamia bei elekezi ili kumwezesha mkulima kuipata kwa bei nafuu.

Amesema kuwa bei ya sasa ya mbolea ya kukuzia na kupandia bado si rafiki kwa wakulima, hivyo TFRA wana wajibu wa kuhakikisha kuwa bei inapungua zaidi.

Waziri Hasunga aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha vyama vya ushirika kuhusu ununuzi wa mbolea kwa pamoja (BPS) kilichofanyika katika ukumbi wa Mpendejirani eneo la Vwawa, mkoani hapa.

Alisema kanuni za usimamizi na uagizaji wa mbolea kwa pamoja, zilitungwa kutokana na utafiti wa kina uliofanywa na watafiti wa ndani ya nchi na wengine kutoka taasisi za kimataifa na matokeo yake kuonyesha kuwa BPS inaweza kupunguza gharama ya uagizaji kwa zaidi ya asilimia 50.

Pamoja na matarajio hayo ya serikali na wakulima, alisema bado gharama za mbolea si rafiki kwa wakulima pamoja na bei kushuka mwaka 2019 kulinganisha na miaka iliyopita.

Pia alisema licha ya serikali kusisitiza wakulima kutumia vyama vya ushirika katika utatuzi wa changamoto za kiuchumi na kijamii, bado wanaushirika wameshindwa kubuni mfumo madhubuti wa kuwaunganisha katika ununuzi wa pembejeo ambazo zingewapa unafuu wa gharama za uzalishaji.

Alisema hiyo pia inatokana na Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002, kusisitiza kwamba ushirika ni chombo pekee cha kumletea mwananchi mnyonge maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Waziri Hasunga aliwaambia washiriki wa mkutano huo kuwa tayari Wizara ya Kilimo kupitia kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika, imetoa waraka wa kuagiza vyama vyote vya ushirika kupeleka mahitaji yao ya mbolea TFRA ili iagizwe kwa pamoja kupitia BPS.

Alisema vyama vya ushirika vinapaswa kuwa kimbilio la wakulima, hivyo kuagiza mbolea kwa pamoja itasababisha kupungua kwa gharama na kufika kwa wakati.

Pia katika mkutano huo, Waziri Hasunga aliiagiza Taasisi ya Utafiti na Udhibiti wa Viuatilifu katika Ukanda wa Kitropiki (TPRI) kutoa mafunzo kwa wananchi kuhusu matumizi sahihi ya viuatilifu.

# TANGAZO

# KILIMANJARO CO-OPERATIVE BANK LIMITED (KCBL)

**Issued pursuant to regulations 7 and 8 of the Banking and Financial Instituions (Disclosures) Regulation, 2014**

## CONDENSED STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT THE QUARTER ENDED 31/12/2019
(Amounts in shillings)

| | A. ASSETS | Current Quarter Date: 31.12.2019 | Current Quarter Date: 30.09.2019 |
|---|---|---|---|
| 1 | Cash | 1 390 800 | 3 918 609 |
| 2 | Balances with Bank of Tanzania | 237 750 654 | 259 661 853 |
| 3 | Investments in Government securities | - | - |
| 4 | Balances with other banks and financial institutions | 1 128 055 985 | 993 350 593 |
| 5 | Cheques and items for clearing | - | - |
| 6 | Inter branch float iterms | - | - |
| 7 | Bills negotiated | - | - |
| 8 | Customers' liabilities for acceptances | - | - |
| 9 | Interbank Loans Receivables | - | - |
| 10 | Investments in other securities | - | - |
| 11 | Loans, advances and overdrafts (net of allowances for probabl | 223 571 103 | 225 607 837 |
| 12 | Other assets | 40 513 780 | 182 927 084 |
| 13 | Equity Investments | - | - |
| 14 | Underwriting accounts | - | - |
| 15 | Property, Plant and Equipment | 1 165 697 777 | 1 181 570 009 |
| 16 | **TOTAL ASSETS** | **2 796 980 099** | **2 847 035 985** |
| | **B. LIABILITIES** | | |
| 17 | Deposits from other banks and financial institutions | - | - |
| 18 | Customer deposits | 5 770 752 799 | 5 672 187 157 |
| 19 | Cash letters of credit | - | - |
| 20 | Special deposits | - | - |
| 21 | Payment orders/transfers payable | - | - |
| 22 | Bankers' cheques and drafts issued | 16 440 739 | 3 873 216 |
| 23 | Accrued taxes and expenses payable | 58 825 182 | 78 794 704 |
| 24 | Acceptances outstanding | - | - |
| 25 | Interbranch float items | - | - |
| 26 | Unearned income and other deferred charges | - | - |
| 27 | Other liabilities | 584 498 581 | 464 601 892 |
| 28 | Borrowings | - | - |
| 29 | **TOTAL LIABILITIES** | **6 430 517 301** | **6 219 456 969** |
| 30 | **NET ASSETS/(LIABILITIES)(16 minus 29)** | **(3 633 537 202)** | **(3 372 420 984)** |
| | **C. SHAREHOLDERS' FUNDS** | | |
| 31 | Paid up share capital | 6 529 001 775 | 6 379 464 064 |
| 32 | Capital reserves | 453 542 327 | 453 542 327 |
| 33 | Retained earnings | (9 577 692 810) | (9 562 085 906) |
| 34 | Profit (Loss) account | (1 060 425 717) | (665 209 190) |
| 35 | Other capital accounts | 22 037 223 | 21 867 721 |
| 36 | Minority Interest | - | - |
| 37 | **TOTAL SHAREHOLDERS' FUNDS** | **(3 633 537 202)** | **(3 372 420 984)** |
| 38 | Contingent liabilities | - | - |
| 39 | Non performing loans & advances | 1 529 826 966 | 1 526 968 400 |
| 40 | Allowances for probable losses | 1 257 800 008 | 1 265 443 509 |
| 41 | Other non performing assets | 79 127 956 | 79 009 928 |
| | **D. SELECTED FINANCIAL CONDITION INDICATORS** | | |
| (i) | Shareholders Funds to total assets | -129.91% | -118.45% |
| (ii) | Non performing loans to total gross loans | 98.11% | 97.26% |
| (iii) | Gross loans and advances to total deposits | 27.02% | 27.68% |
| (iv) | Loans and advances to total assets | 7.99% | 7.92% |
| (v) | Earning assets to Total Assets | 5.51% | 5.49% |
| (vi) | Deposits Growth | 1.74% | 0.54% |
| (vii) | Assets growth | -1.76% | -29.28% |

## CONDENSED STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME FOR THE QUARTER ENDED 31/12/2019 (Amounts in shillings)

| | | Current Quarter Date: 31.12.2019 | Comparative Quarter (Previous Year) Date:31.12.2018 | Current Year Cumulative Date: 31.12.2019 | Comparative Year (Previous Year) Cumulative Date:31.12.2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Interest Income | 13 115 382 | 39 915 028 | 58 041 221 | 295 320 814 |
| 2 | Interest Expense | 27 494 540 | 25 355 562 | 102 353 908 | 243 211 557 |
| 3 | Net Interest Income ( 1 minus 2) | **(14 379 158)** | **14 559 466** | **(44 312 687)** | **52 109 257** |
| 4 | Bad Debts Written -Off | - | - | - | - |
| 5 | Impairment Losses on :Loans and Advances | - | 877 730 392 | (7 524 550) | 1 198 259 690 |
| 6 | **Non Interest Income:** | **15 943 202** | **14 043 561** | **112 910 735** | **78 743 507** |
| | 6.1 Foreign Currency Dealings and Translation Gains/ (Loss) | - | - | - | - |
| | 6.2 Fees and Commissions | 7 220 800 | 11 389 083 | 40 408 119 | 60 131 480 |
| | 6.3 Dividend Income | - | - | - | - |
| | 6.4 Other Operating Income | 8 722 402 | 2 654 478 | 72 502 616 | 18 612 027 |
| 7 | **Non Interest Expenses:** | **396 780 572** | **495 940 270** | **1 136 548 315** | **1 556 349 730** |
| | 7.1 Salaries and Benefits | 143 224 139 | 137 416 106 | 517 512 851 | 590 830 617 |
| | 7.2 Fees and Commission | 1 176 175 | 13 139 914 | 49 535 937 | 58 754 715 |
| | 7.3 Other Operating Expenses | 252 380 258 | 345 384 250 | 569 499 527 | 906 764 398 |
| 8 | **Operating Income/ (Loss)** | **(395 216 527)** | **(1 345 067 635)** | **(1 060 425 717)** | **(2 623 756 656)** |
| 9 | **Income Tax Provision** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| 10 | **Net Income / (Loss) After Income Tax** | **(395 216 527)** | **(1 345 067 635)** | **(1 060 425 717)** | **(2 623 756 656)** |
| 11 | **Other Comprehensive Income (itemize)** | | | | |
| 12 | **Total Comprehensive Income/(loss) for the year** | **(395 216 527)** | **(1 345 067 635)** | **(1 060 425 717)** | **(2 623 756 656)** |
| 13 | Number of Employees | 22 | 32 | 22 | 32 |
| 14 | Basic Earnings Per Share | -309.76 | -97.50 | -831.12 | -190.19 |
| 15 | **Number of Branches** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | **SELECTED PERFORMANCE INDICATORS** | | | | |
| (i) | Return on Average Total Assets | -42.39% | -56.67% | -454.96% | -331.63% |
| (ii) | Return on Average Shareholders' Fund | -18.16% | -54.80% | -194.90% | -1775.83% |
| (iii) | Non Interest Expense to Gross Income | -1365.45% | -919.11% | -664.83% | -416.06% |
| (iv) | Net Interest Income to Average Earning Assets | -530.32% | -356.49% | -474.313% | -695.39% |

Average figures shall be computed by summing up the end balances for respective months in the period divided by number of months in the period.

## CONDENSED STATEMENT OF CHANGES IN EQUITY AS AT 31/12/2019

| Current Year | Share Capital | Share Premium | Retained Earnings | Regulatory Reserve | General Provinsion Reserve | Others | Total |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Balance as at the beginning of the year** | 7 363 802 064 | 0 | -6 497 512 011 | 9 096 425 | 806 449 | 453 542 328 | 1 329 735 255 |
| Profit for the year | | | (1 060 425 717) | | | | -1 060 425 717 |
| Other Comprehensive Income | | | | | | | - |
| Transactions with owners | (834 800 289) | | | | | | (834 800 289) |
| Dividends Paid | | | | | | | - |
| Regulatory Reserve | | | | 12 645 392 | | | 12 645 392 |
| General Provision Reserve | | | | | (511 044) | | (511 044) |
| Others | | | (3 080 180 799) | | | | (3 080 180 799) |
| **Balance as at the end of the current period** | **6 529 001 775** | **-** | **(10 638 118 527)** | **21 741 817** | **295 405** | **453 542 328** | **(3 633 537 202)** |
| **Previous Year** | | | | | | | |
| **Balance as at the beginning of the year** | **1 512 496 093** | **-** | **(3 888 172 293)** | **93 021 759** | **27 594 788** | **487 455 289** | **(1 767 604 364)** |
| Profit for the year | - | - | (2 623 756 656) | - | - | - | (2 623 756 656) |
| Other Comprehensive Income | - | - | - | - | - | - | - |
| Transactions with owners | 5 851 305 971 | - | - | - | - | - | 5 851 305 971 |
| Dividends Paid | - | - | - | - | - | - | - |
| Regulatory Reserve | - | - | - | (83 925 334) | - | - | (83 925 334) |
| General Provision Reserve | - | - | - | - | (26 788 339) | - | (26 788 339) |
| Others | - | - | 14 416 937 | - | - | (33 912 961) | (19 496 024) |
| **Balance as at the end of the previous period** | **7 363 802 064** | **-** | **(6 497 512 011)** | **9 096 425** | **806 449** | **453 542 328** | **1 329 735 255** |

## CONDENSED STATEMENT OF CASH FLOW STATEMENT FOR THE QUARTER ENDED 31/12/2019 (Amounts in shillings)

| | | Current Quarter Date:31.12.2019 | Previous Quarter Date:30.09.2019 |
|---|---|---|---|
| I: | **Cash flow from operating activities:** | | |
| | Net income/ (Loss) | (395 216 527) | (232 357 973) |
| | **Adjustments for:** | - | - |
| | - Impairment/Amortization | - | - |
| | - Depreciation | 15 872 232 | 15 872 232 |
| | - Net change in Loans and Advances | 2 036 734 | 41 987 202 |
| | - (Gain)/loss on Sale of Assets | - | - |
| | - Net change in Deposits | 98 565 642 | 30 602 458 |
| | - Net change in Short Term Negotiable Securities | - | - |
| | - Net change in Other Liabilities | 119 896 689 | 205 962 101 |
| | - Net change in Other Assets | 142 413 304 | (96 873 293) |
| | - Tax Paid | - | - |
| | - Others ( specify) | (22 704 404) | 17 155 338 |
| | - Minority interest | - | - |
| | ***Net cash provided (used) by operating activities*** | **(39 136 330)** | **(17 651 935)** |
| II: | **Cash flow from investing activities:** | | |
| | Dividend Received | - | - |
| | Purcharse of Fixed Assets | - | - |
| | Proceeds from Sale of Fixed Assets | - | - |
| | Purchase of Non-Dealing Securities | - | - |
| | Proceeds from Sale of Non-Dealing Securities | - | - |
| | Others (specify) | - | - |
| | ***Net cash provided (used) by investing activities*** | - | - |
| III: | **Cash flow from financing activities:** | | |
| | Repayment of Long-term Debt | - | - |
| | Proceeds from Issuance of Long Term Debt | - | - |
| | Proceeds from Issuance of Share Capital | 149 537 711 | (1 200 000 000) |
| | Payment of Cash Dividends | - | - |
| | Net Change in Other Borrowings | - | - |
| | Others | | - |
| | ***Net Cash Provided (used) by Financing Acities*** | **149 537 711** | **(1 200 000 000)** |
| IV: | **Cash and Cash Equivalents:** | | |
| | **Net Increase/ (Decrease) in Cash and Cash Equivalents** | **110 401 381** | **(1 217 651 935)** |
| | **Cash and Cash Equivalents at the Beginning of the Quarter/Year** | **1 256 796 058** | **2 474 447 993** |
| | **Cash and Cash Equivalents at the end of the Quarter/Year** | **1 367 197 439** | **1 256 796 058** |

| ***Name and Title*** | ***Signature*** | ***Date*** |
|---|---|---|
| Janeth. J. Minja<br>**Ag. GENERAL MANAGER** | ......................... | 22ND JANUARY 2020 |
| Anna. H. Teete<br>**SENIOR ACCOUNTANT** | ......................... | 22ND JANUARY 2020 |
| Denis. A. Ruhangisa<br>**INTERNAL AUDITOR** | ......................... | 22ND JANUARY 2020 |

We, the under-named, non-executive members of the board of directors, attest to the correctness of the above statements. We declare that the statements have been examined by us, and to the best of our knowledge and belief have been prepared in conformance with the instructions and are true and correct.

| ***Name*** | ***Signature*** | ***Date*** |
|---|---|---|
| **1. Dr G Machimu, CHAIRMAN, BOARD OF DIRECTORS** | ......................... | 22ND JANUARY 2020 |
| **2. Ms A.A. Mshana ,VICE CHAIR PERSON BOARD OF DIRECTORS** | ......................... | 22ND JANUARY 2020 |

# MINIMUM DISLOSURES OF CHARGES AND FEES

| NUMBER | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| 1.0 | Current Accounts | |
| | (a) Required minimum opening balance | 100 000 |
| | (b) Monthly service fee (breakdown per customer type): | |
| | Individuals | 8 000 |
| | Co-operatives | 6 500 |
| | Companies | 8 000 |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | 1 000 |
| | (d) Fees per ATM withdrawal | 1 000 |
| | (e) ATM min statement | 500 |
| | (f) Interim statement per page | 1 500 |
| | (g) Periodic scheduled statement | 1 000 |
| | (h) Cheque book | 20 000 |
| | (i) Dishonoured cheque | 40 000 |
| | (j) Special clearance | N/A |
| | (k) Counter cheque | 700 |
| | (l) Stop payment | 30 000 |
| | (m) Standing order | N/A |
| | (n) Balance enquiry | N/A |
| | (o) New ATM card issuance | 10 000 |
| | (p) ATM card renewal or replacement (indicate costs for different card types) | 10 000 |
| | (q) Overdrawn account interest charge | N/A |
| | (r) Unarranged overdraft | N/A |
| | (s) Interbank transfer | 13 000 |
| | (t) Bill payments through ATM | 1 000 |
| | (u) Deposit fee i.e for school fees | 1 000 |
| | (v) Withdrawal without cheque leaf | 5 000 |
| | (w) Withdrawal charges above 6 million | 0.15% |
| 2.0 | Savings Accounts (Disclosure for product specific types) | |
| | (a) Required minimum opening balance | 30 000 |
| | (b) Monthly service fee | 1 000 |
| | (c) Interim statement | 1 500 |
| | (d) Account closure | 10 000 |
| | (e) School fees deposite charges | 1 000 |
| | (f) ATM withdrawal fee | 1 000 |
| | (g) Withdrawal charges over the counter | 600 |
| | (h) Replacement of ID Card | 5 000 |
| | (i) Withdrawal above 3 million without notice | 0.25% |
| | (j) Stop payment charges | 30 000 |
| | (k) Salary processing fee | 3 000 |
| | (l) Pension processing fee | 2 000 |
| | (m) Searching past records fee | 10 000 |
| | (n) Dormant Account Activation | 10 000 |
| | (o) Certificate of Balance | 3 000 |
| 3.0 | Electronic Banking | |
| | (a) Internet banking monthly fee | N/A |
| | (b) Internet transfer | N/A |
| | (c) SMS banking | N/A |
| | (d) Other TT/SWIFT | 13 000 |
| | (e) Transfer from bank account to mobile | 1 000 |
| 4.0 | Foreign Exchange Transaction | N/A |
| | (a) Purchase/sale of TCs transaction over the counter | N/A |
| | (b) Purchase of foreign cheque | N/A |
| | (c) Sale/purchases of cash passport | N/A |
| | (d) Telegraphic transfer | N/A |
| | (e) Telex/SWIFT | N/A |
| | (f) Transfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank) | N/A |
| 5.0 | Personal Loans | |
| | (a) Processing /Arrangement/Appraisal fee | 1.5-4% |
| | (i) Personal loans | 24% |
| | (ii) Overdrafts | 18-24% |
| | (iii) Mortgage finance | N/A |
| | (iv) Asset finance | N/A |
| | (b) Unpaid loan instalment i.e. above the existing rate | 5% |
| | (c) Early repayment | N/A |
| | (d) Valuation fees | N/A |
| | (e) Discharge of Security Document to other banks | 120 000 |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Janeth. J. Minja | Ag. General Manager | | 22ND JANUARY 2020 |
| 2 | Anna .H. Teete | Senior Accountant | | 22ND JANUARY 2020 |
| 3 | Denis. A. Ruhangisa | Internal Auditor | | 22ND JANUARY 2020 |

215593602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Unahitajika uchunguzi maelfu kukataa shule*

TAARIFA kuwa wazazi 17,000 mkoani Mtwara, wataanza kusakwa baada ya watoto wao kutoonekana shuleni na kuanza masomo ya kidato cha kwanza zinaashiria kuwa , licha ya serikali kutoa elimumsingi bure, changamoto bado ni nyingi.

Wazazi hao ambao watasakwa ni wale ambao watoto wao wameshindwa kuripoti shuleni kuanzia kidato cha kwanza mwaka huu.

Mkuu wa Mkoa, Gelasius Byakanwa, anatoa agizo la kuwasaka baada ya kufanya ziara katika Manispaa ya Mtwara Mikindani na kukuta wanafunzi wa kidato cha kwanza zaidi ya 3,000 wakiwa hawajaripoti shuleni.

Kinachotokea Mtwara kinaakisi ukweli kuwa licha ya serikali kugharamia elimu bado kuna changamoto lukuki ikiwamo utayari na uhiari wa wazazi kuwaruhusu kuripoti shuleni.

Hivyo tunashauri kuwa pamoja na Mtwara kufanya msako ni bora serikali mkoani humo, ikafanya utafiti kubaini kile kilichosababisha tatizo hilo.

Ni ukweli kuwa ingawa hakuna kulipa ada wanafunzi wa familia maskini huenda hawana uwezo wa kwenda shule kwa sababu ya gharama nyingine kama kununua sare, vitabu, nauli na mahitaji ya msingi kikiwamo chakula.

Wazazi au walezi hawana fedha za kuwalipia nauli ya kwenda shule kwa wanaokaa mijini na miji midogo, kuwanunulia sare na mahitaji mengine kama vitabu, daftari na kuwapa chakula, hivyo inawezekana ni moja ya sababu zilizochangia utoro huo.

Si hivyo ni wazi kuwa ukosefu wa mabweni katika sekondari hasa zilizo mbali na vijiji ama makazi ya wanafunzi wengi, wakati mwingine kunawalazimisha wanafunzi kupanga vyumba karibu na shuleni.

Iwapo walezi na wazazi mkoani Mtwara hawana uwezo ni changamoto kubwa inayosababisha kutoripoti shuleni kwa wanafunzi hao.

Tunaona kuwa miundombinu mibovu na uhaba wa usafiri mashuleni nalo ni tatizo hasa kwa wanafunzi wa vijijini ambao wanalazimika kusafiri mwendo mrefu kwenda shule na kurudi nyumbani.

Kuna uwezekano kuwa shule nyingi za sekondari zina ukosefu wa miundombinu hiyo hivyo kuwakatisha tamaa wanafunzi hao.

Wakati mwingine umaskini na ukosefu wa fedha husababisha watoto kutumikishwa na walezi na wazazi wao, jambo linalowaelekeza zaidi kwenye kazi za kusaidia familia badala ya kufikiria masomo.

Hivyo wakati msako huo unapofanyika ni vyema yote hayo yakaangaliwa kwani huleta mkwamo na wanafunzi kuacha shule au kutoripoti shuleni kama ilivyotokea kwa shule hizo za Mtwara.

Aidha, tunafahamu kuwa mabinti kutokuripoti shuleni ni changamoto nyingine inayowakumba wasichana tatizo kubwa likiwa ni unyanyasaji kingono, kijinsia, ubaguzi na kuzuiliwa kusoma kwa sababu mbalimbali ikiwamo kuozwa utotoni.

Wasichana wengi wanaathiriwa na unyanyasaji wa kijinsia kutoka kwa jamii zao, wana ndugu na hata walimu wao. Wengine hunyanyaswa kijinsia na kingono na bodaboda au hata watu wazima ambao huwataka kingono baada ya kuwapa zawadi, lifti au pesa wakati wakiwa njiani kuelekea shuleni, yote haya huwakwamisha kimasomo.

Baadhi ya shule za kata hasa vijijini zina ukosefu wa walimu wa masomo mengi jambo linalowakatisha tamaa walezi, wazazi na wanafunzi na kusababisha baadhi ya wanafunzi kukataa kwenda shuleni.

Ukosefu wa walimu huwalazimisha wanafunzi wakati mwingine kutafuta njia mbadala wa kujifunza au kulipia mafunzo binafsi ya ziada bila hivyo ni wanashindwa kufanya vizuri kwenye mitihani yao.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge



Na Mary Geofrey

# Sekta ya afya yaanika mafanikio makubwa

**WIZARA** ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na taasisi zote zilizo chini yake, ipo katika kampeni yake maalum ya kukagua utekelezaji wa miradi yake na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano.

Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya ni hospitali zote nchini, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), Mpango wa Taifa wa Damu Salama, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na Taasisi ya Utafiti ya Magonjwa ya Binadamu (Nimri).

Wiki iliyopita maofisa mawasiliano wa taasisi hizo kwa kushirikiana na waandishi wa habari, walifanya ziara katika ofisi zote na kuzungumza na wakurugenzi watendaji ambao walieleza kwa kina nini kinafanyika katika taasisi hizo na mafanikio yanayotokana na uwekezaji uliofanywa na serikali katika sekta ya afya.

Katika ziara iliyoanza wiki iliyopita na inayoendelea kila taasisi imepata fursa ya kuelezea kwa kina utekelezaji wa majukumu yao, mafanikio na malengo yake ya kuhakikisha wanatoa huduma bora kwa wananchi.

Kikubwa ambacho kilionekana kuwa ni mafanikio makubwa katika hospitali ambazo walitembelea katika Jiji la Dar es Salaam ni uboreshaji wa huduma za tiba.

Aidha, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika hospitali, watoa huduma na madaktari bingwa, uwapo wa miundombinu ya majengo na vitanda vya kutosha kulaza wagonjwa ni miongoni mwa mafanikio yaliyoonekana dhahiri katika hospitali zote walizotembelea.

Walipata fursa ya kutembelea Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na Tawi la Mloganzila, Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI), Hospitali ya Saratani ya Ocean Road na Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala.

Katika hospitali hizo, wakurugenzi wote walieleza hali waliyokuwa hapo awali kabla ya serikali kuwekeza fedha, wanavyotekeleza majukumu ya kuhakikisha wanarejesha afya na uhai wa Watanzania na mipango ya baadaye ya kuhakikisha wanapunguza rufani za kwenda nje ya nchi.

Ninachoweza kusema ni kwamba serikali imepiga hatua kubwa kwenye sekta ya afya, imewekeza vya kutosha, imesimamia utoaji wa huduma bora na zaidi uwapo wa vifaa tiba na dawa.

> **Kikubwa ambacho kilionekana kuwa ni mafanikio makubwa katika hospitali ambazo walitembelea katika Jiji la Dar es Salaam ni uboreshaji wa huduma za tiba.**

Katika hospitali hizo kubwa nchini, imeonekana wazi kuwa tatizo la wataalamu wabobezi limepatiwa ufumbuzi kwa kiasi kikubwa na wanaendelea na mikakati yake ya kumaliza kabisa tatizo kwa kuwapeleka madaktari wengi nje ya nchi kujinoa kutoa tiba za kibingwa nchini.

Kuhusu suala ya dawa na vifaa tiba na dawa nalo limepatiwa ufumbuzi kwa sababu kadhaa ikiwapo kuanzishwa maduka ya dawa katika hospitali zote zilizotembelewa.

Pia suala la miundombinu limefanyika katika hospitali zote, ujenzi wa majengo ya kisasa mapya kwa ajili ya kutolea huduma za kibingwa na majengo ya zamani yakiwa yamepanuliwa na kukarabatiwa ili wagonjwa wapate nafasi ya kupata matibabu kwa uhuru.

Kadhalika eneo la utoaji huduma bora na kwa wakati, uwapo wa teknolojia ya kisasa katika vyumba vya kulaza wagonjwa, mitambo ya kisasa ya kutoa huduma ni miongoni mwa mafanikio ambayo yanaonekana wazi. Kadhalika katika eneo la huduma za dharura wamejipanga vyema kutokana na kuwa sehemu ambazo zinatolewa huduma zote na mgonjwa akitoka hapo ni kwa ajili ya kwenda wodini kupumzika na siyo kusubiria huduma.

Kutokana na kuwapo kwa huduma hizo nchini, wagonjwa waliokuwa waende nje ya nchi kupatiwa matibabu sasa wanatibiwa nchini kwa gharama nafuu kulinganisha na nje ya nchi.

HABARI KITAIFA

## NHC yakusanya mil. 618/- kodi Kigoma

**Na Munir Shemweta, KIGOMA**

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) Mkoa wa Kigoma limekusanya Sh. 618,246,592 sawa na asilimia 70 ya makusanyo ya mwaka 2019.

Akitoa taarifa ya makusanyo ya kodi kwa miradi ya shirika hilo kwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, kwa mwaka 2019/20, Kaimu Meneja wa NHC Mkoa wa Kigoma, Ramadhani Sadick, alisema walipangiwa kukusanya Sh. 886,732,105 na kubainisha kuwa ziada iliyopatikana ilitokana na uhusiano mazuri na wateja na huduma bora zinazotolewa.

Kwa mujibu wa Sadick, NHC imekuwa ikifanya jitihada kuhakikisha inaboresha uhusiano na wapangaji ili kuwapo maridhiano kati ya shirika na wateja jambo alilolieleza linasaidia kupunguza migogoro baina ya pande hizo.

"Shirika limekuwa likifanya mazungumzo na wateja ili kuona namna bora ya kuwasaidia kutekeleza majukumu ya kiupangaji ilhali wakiendelea na biashara zao na tunatoa fursa ya kulipa kodi kwa awamu tofauti na utaratibu uliozoeleka wa kulipa kodi kwa mara moja," alisema.

Kuhusu hali ya soko, Sadick alisema shirika limekuwa likifanya utafiti mara kwa mara ili kuhakikisha bei linazotoza kwenye nyumba za kupanga zinaendana na hali ya soko na mazingira halisi.

Akigeukia nyumba za kuuza katika mradi wa Mlole, alisema shirika lilijenga nyumba 36 za makazi na nyumba 26 kati ya hizo ziliuzwa huku nyumba 13 zikipangishwa kwa wateja ambao walipewa fursa ya kununua pale watakapohitaji.

Pia alibainisha kuwa fursa hiyo inatolewa pia kwa mwananchi yeyote anayetaka kununua nyumba zilizopangishwa na kwamba mkataba wa upangishaji unatoa fursa kwa mnunuzi asiye mpangaji kununua nyumba yoyote aitakayo.

Naibu Waziri Mabula alilitaka shirika kuangalia namna bora ya kushirikiana na halmashauri zilizoko nje ya miji katika kujenga nyumba za watimishi badala ya kuangalia halnashauri za mjini pekee.

Katika kuhakikisha shirika linajenga nyumba za bei nafuu kwa watumishi katika halmashauri, alilitaka kukabidhiwa viwanja huku kazi ya kuweka miundombinu na gharama zingine ikibaki halmashauri husika.

# Kisima cha gesi hatarini kuzamishwa maji bahari

**Na Lucy Ogutu, MTWARA**

KISIMA cha gesi asilia cha Mnazibay kilichopo Wilaya ya Mtwara vijijini kiko hatarini kumezwa na maji ya bahari kutokana na kuta za bahari kulika siku hadi siku na kukaribia kisima hicho.

Kisima hicho kilijengwa umbali wa mita 150 kutoka usawa wa bahari, lakini kwa sasa zimebaki mita chache kufikia kisima hicho.

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Evodi Mmanda, alitoa taarifa hiyo kwa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara aliyetembelea ofisi yake na kupata taarifa ya wilaya.

Alisema ziara iliyofanywa na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hivi karibuni ilitembelea kisima hicho na kubaini hali ya mmomonyoko wa bahari unaoendelea kwa kasi inayohatarisha huenda kikazama.

Aidha, alishauri wataalamu wa miamba kutoka Wizara za Madini na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, na kitengo cha usimamizi wa bahari na maeneo tengefu, Wizara ya Uvuvi na Mifugo washirikiane kujua chanzo cha hali hiyo ili kuja na mapendekezo ya nini kifanyike.

Alisema kwa mujibu wa taarifa zilizopo eneo hilo, kina chake ni kirefu hivyo yawezekana eneo hilo linalika chini kwa chini na huenda kikadondoka kipande kikubwa cha ardhi na kikaleta madhara makubwa.

Baada ya kupokea taarifa hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, alithibitisha kuwapo kwa hali hiyo na kwamba mwaka jana alitembelea eneo hilo na kutoa ushauri kwa mamlaka husika kuangalia uwezekano wa kujenga uzio ili kunusuru kisima hicho, lakini mpaka hivi leo mkoa haufahamu hatua zilizofikiwa.

Aidha, aliishauri wilaya hiyo kuandika taarifa haraka iwezekanavyo zifike kwenye mamlaka husika ili tatizo hilo liweze kufanyiwa kazi.

Mwaka 2018, Waziri wa Nishati, Merdadi Kalemani alitembelea kisima hicho na kukuta hali hiyo na kutoa maagizo kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kujenga ukuta katika eneo hilo lakini hakuna kilichofanikiwa hadi sasa.



Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Mikopo ya Nyumba ya Tanzania Mortgage Refinance (TMRC), Charles Itembe (wa tatu kushoto), akishikana mkono na Mwakilishi Mkazi wa Taasisi ya Fedha ya Kimataifa (IFC) nchini, Frank Ajilore, katika hafla ya kutangaza ushirikiano kati ya taasisi hizo mbili, jijini Dar es Salaam jana. Kutoka (kulia) ni Mkurugenzi wa Utafiti wa Uchumi na Sera kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Suleiman Misango na Ofisa Mtendaji Mkuu wa TMRC, Oscar Mgaya. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Wizara kukutana kudhibiti bodaboda

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Maliasili na Utalii na ile ya Mambo ya Ndani ya Nchi, zinatarajia kukutana kujadili namna ya kukabiliana na bodaboda na baiskeli zinazotumika kusafirisha mazao ya misitu, yakiwamo magunia ya mkaa kutoka kwenye misitu kupelekwa maeneo ya mijini.

Hayo yalisemwa juzi jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu huku akibainisha kuwa mazungumzo hayo yatasaidia kupunguza ajali za barabarani kati ya waendesha magari na bodaboda zinazobeba magunia ya mkaa kuzidi uwezo.

Alisema inapotokea kuna mzigo kama huo, madereva wa bodaboda hizo kushindwa kuzimudu pindi wanapopishana na magari katika barabara kuu.

Kwa mujibu wa Kanyasu, uamuzi huo unakuja kutokana na wimbi la bodaboda na baiskeli kuwa vyombo vikuu vya kusafirishia magunia ya mkaa kutoka katika misitu mbalimbali na kupelekwa mjini kwa ajili ya kuuzwa.

Takwimu zilizopo zinaonyesha Dar es Salaam inatumia zaidi ya tani 500,000 za mkaa kwa mwaka na robo ya tani hizo husafirishwa kwa kutumia bodaboda na baiskeli.

Alisema takribani hekta 400,000 za misitu huteketea kila mwaka na kwamba hali hiyo ikiendelea, baada ya miaka 12 misitu yote itakuwa imekwisha nchi nzima.

Kanyasu alisema endapo hatua za makusudi hazitachuliwa mapema kukabiliana na tatizo hilo, misitu yote nchini itatoweka kutokana na uwapo vyombo rahisi vya kusafirishia mkaa.

Alisema kukutana kwa wizara hizo mbili kutatoa mwelekeo wa namna ya kukabiliana na tatizo hilo na askari wa usalama barabarani watashirikiana na maofisa misitu kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuvidhibiti vyombo hivyo.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, TFS pekee yake haiwezi kupambana na vyombo hivyo vya usafirishaji mazao ya misitu, lakini kwa kusaidiana Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa pamoja watavidhibiti, hivyo kupunguza uharibifu wa misitu.

Amesema mazungumzo hayo yanatarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi huu na anaamini kuwa yatasaidia kuokoa misitu inayokatwa kila siku kwa ajili ya matumizi ya mkaa.

Kwa mujibu wa takwimu zilizopo, alisema kwa siku zaidi ya bodaboda 3,000 na baiskeli 1,500 zimekuwa zikibeba wastani wa magunia ya mkaa matano kwa mara moja kila moja kupitia barabara ya Morogoro kwenda jijini Dar es Salaam.

Alizitaja pia barabara za Bagamoyo na Kilwa kuwa hutumika zaidi ya bodaboda 6,000 na baiskeli 3,000 kusafirisha mkaa kwenda Dar es Salaam.

# Mwanamke aibua madai kunyanyaswa na mtendaji

**Na Ndalike Sonda, KAHAMA**

MKAZI wa Kijiji cha Idahina, Halmashauri ya Ushetu, Kahama mkoani Shinyanga, Christina Sahani, amemlalamikia Ofisa Mtendaji wa Kata ya Idahina, Matheo Andrea, kwa madai ya kumweka mahabusu na walinzi wawili wa kiume.

Sahami (40) amedai kuwa jambo hilo limemletea shida wakati wa usiku kutokana na kusumbuliwa na walinzi hao.

Akizungumza jana na waandishi wa habari katika ofisi za Shirika la Kutetea Haki za Binadamu wilayani Kahama (Shihabi), Sahani alidai alikamatwa na Ofisa Mtendaji huyo kwa tuhuma za kuandika barua ya kufanya mauaji dhidi ya mke mwenza.

Sahani alisema baada ya kukamatwa wiki iliyopita majira ya saa 11:00 jioni, aliwekwa mahabusu na mtendaji huyo huku akitakiwa atoe Sh. 600,000 ili atoke mahabusu.

Baada ya kushindwa kulipa, alisema alirudishwa kwenye chumba hicho na kisha kufungiwa na walinzi hao ambao waliambiwa wamlinde hadi asubuhi.

Alisema kuwa ilipofika usiku, mlinzi mmoja alikwenda kunywa pombe na aliporudi alimtaka mwanamke huyo kutoa Sh. 600,000 zilizohitajika na uongozi, huku akimshika shika kiunoni jambo ambalo lilimtisha na kuwatishia angepiga kelele kuwa wanambaka.

"Niliwekwa mahabusu na walinzi wawili wa kiume na usiku mmoja alikwenda kunywa pombe. Aliporudi aliomba nitoe ile pesa, huku akinishika kiunoni ananiambia kuwa huna hata shanga nikamwambia nitapiga kelele maana mnataka kunibaka ndipo wakaogopa tukalala hadi asubuhi.

Alisema mtendaji huyo alipofika kituoni hapo asubuhi aliamrisha atolewe na kumtaka arudi siku atakayohitajika na kwamba baada ya kuachiwa alikwenda kushtaki ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama na Shihabi.

Kutokana na madai hayo, Shihabi wilayani Kahama, imelaani vikali matukio ya unyanyasaji yanayodaiwa kutekelezwa na baadhi ya viongozi wa serikali wakiwamo maofisa watendaji wa vijiji, kata na wenyeviti.

Mkuu wa Kitengo cha Haki na Jinsia wa Shahabi, Theopista Paschal, alisema shirika hilo litachukua hatua za kisheria kwa kumfikisha katika mamlaka husika mtendaji huyo. Ofisa Tarafa wa Kahama, Julius Chagama, alikiri kupokea malalamiko hayo na kwamba atayafikisha kwa Katibu Tawala wa wilaya, kisha kwa Mkuu wa Wilaya kwa ajili ya kufanyiwa kazi za kinidhamu na kisheria ili kutafuta haki.

Kwa upande wake ofisa mtendaji huyo alikiri kumshikilia mwanamke huyo kwa tuhuma za kuhusishwa na kutaka kufanya mauaji yanayotokana na imani za ushirikina na kwamba aliwaelekeza walinzi wakae nje wakimlinda mwanamke huyo.



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Mkoa wa Shinyanga, Emmanuel Ntobi (kushoto), akizungumza na wanachama nje ya ofisi za chama hicho, Wilaya ya Shinyanga jana. Habari Uk. 3. **PICHA: MARCO MADUHU**

# TCRA yatoa msimamo uzimaji simu

INATOKA UK 2

imepungua ikilinganishwa na siku za hivi karibuni.

Nipashe lilizungumza na baadhi ya wananchi ambao laini zao hazijafungiwa, walisema walikata tamaa wakijua jana laini zao zitafungiwa lakini wameendelea kupata mawasiliano.

Mmoja wa Wakazi Mbwanga jijini humo, Ester John, alisema laini yake haikusajiliwa siku za nyuma lakini jana aliendelea na kupata huduma ya mawasiliano kama kawaida.

"Laini yangu ni ya zamani lakini nashukuru naendelea kupata mawasiliano ya kupiga na kupigiwa simu bila tatizo lolote ila nitahakikisha naisajili leo leo," alisema.

Msajili laini za simu za mkononi kwa njia ya alama za vidole jijini Dodoma, Amani Adamu, alisema kwa siku ya jana watu waliofika kusajili laini za simu kwa kufungiwa walikuwa hawafiki hata 10.

"Wako wachache waliofika hapa kwa ajili ya kusajili laini zao za simu kwa kudai zilifungiwa jana usiku na tulipowafanyia usajili laini hizo zilifunguliwa," alisema.

Hata hivyo, alibainisha kuwa katika wateja hao waliofika kusajili laini zao zikiwa zimefungiwa, wote walikuwa wa mtandao wa Halotel na hakuna wa mitandao mingine.

Gazeti hili pia lilimtafuta Msajili wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA) Wilaya ya Dodoma, Khalid Mrisho, ambaye alisema kuna idadi ndogo ya wananchi waliojitokeza kwenye ofisi hizo kujiandikisha na kupiga picha kwa ajili ya kupata vitambulisho vya taifa.

"Kama unavyoona hapa hakuna watu tangu asubuhi tumehudumia watu wasiozidi 50 tofauti na siku 15 za nyuma kabla ya Januari 20 nafasi ilikuwa haitoshi mpaka foleni zilizunguka barabarani," alisema.

Aliongeza kuwa wananchi wamekuwa na tabia ya kukimbizana na muda wa mwisho katika kila tukio kubwa la kitaifa linapofanyika kila mwaka.

Aidha, alisema Nida wanaendelea kutoa huduma ya vitambulisho vya taifa kwa wale waliokosa na wale wanaofikia umri wa miaka 18 ya kisheria kupata vitambulisho.

Imeandikwa na Mary Geofrey, DAR, na Ibrahim Joseph, DODOMA

# NMB yazipiga jeki shule madawati, viti

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imetoa msaada wa madawati bora 60 na viti vyake 60 kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Magingo iliyopo katika Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma.

Akitoa taarifa kwenye hafla ya kukabidhi vifaa hivyo iliyofanyika katika Shule ya Msingi Magingo Madaba, Meneja wa NMB Kanda ya Kusini, Haji Msingwa, alisema NMB pia imechangia viti vya maabara 132 kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Lipupuma .

Msingwa alisema vifaa vyote hivyo vimegharimu Sh. milioni 8.5, na kwamba katika mwaka 2020, NMB imetenga bajeti ya zaidi ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuchangia maendeleo ikiwamo kusaidia sekta ya afya na elimu.

"NMB itaendelea kuunga mkono juhudi za wadau wake katika kuhakikisha kuwa changamoto za jamii zinapatiwa ufumbuzi katika kujenga afya na elimu bora," alisisitiza.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Madaba na Diwani wa Kata ya Mkongotemba, Vastus Mfikwa, aliishukuru NMB kwa kupunguza changamoto ya madawati katika shule mbili za sekondari zilizopo katika kata yake ambapo vifaa hivyo vitasaidia kuboresha elimu katika kata hiyo.

Alisema Shule ya Sekondari Magingo ni miongoni mwa shule zilizofanya vizuri kwenye mtihani wa taifa wa kidato cha nne, ambapo Halmashauri ya Madaba imekuwa ya kwanza kati ya halmashauri nane za Mkoa wa Ruvuma, na imeshika nafasi ya 23 kitaifa kati ya halmashauri 185 Tanzania na msaada huo utachochea zaidi katika elimu.

Ofisa Elimu Kata ya Mkongotema, Edwin Thadei, alisema kata hiyo ina shule mbili za sekondari za Magingo na Lipupuma ambazo zilikuwa zinakabiliwa na changamoto ya meza na viti, na kwamba msaada huo umepunguza tatizo kwa asilimia 90.

"Kabla ya msaada kutoka Benki ya NMB, sekondari za Magingo na Lipupuma zilikuwa na upungufu wa meza 77, viti 87 na stuli 82," alisema.

Akizungumza kabla ya makabidhiano ya vifaa hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema, alisema Benki ya NMB imekuwa msaada mkubwa katika Wilaya ya Songea kwa kutatua changamoto katika sekta ya afya na elimu.

Alisema msaada huo unakwenda kuchochea ufaulu kwa wanafunzi kwa sababu wanasoma katika madarasa yenye mazingira rafiki ya kusomea ambapo amesisiza kuwa urithi pekee kwa watoto ni elimu.

Antony Mayemba, wanafunzi katika Sekondari ya Magingo alipongeza benki hiyo kwa msaada huo ambao alisema umepunguza changamoto ya viti na meza kwa wanafunzi.

HABARI KITAIFA

## Makundi maalum yapata mil. 900/- kwa miaka mitano

**Restuta Damian, BUKOBA**

JUMLA ya Sh. milioni 912 .9 zimetolewa na Halmashauri ya Wilaya Karagwe mkoani Kagera kwa vikundi 394 vyenye watu 6,547 kuanzia mwaka 2015 hadi Januari 15, mwaka huu.

Hayo yalibainishwa na mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Wallace Mashanda, wakati akiongea na Nipashe, na kueleza kuwa halmashauri hiyo inatoa mikopo kwa makundi ya walemavu, vijana na wanawake ambao wana sifa kupitia vikundi ambavyo wameunda wao kwa kufahamiana na kutambua fedha inayotolewa itarejeshwa.

Alisema matarajio yaliyopo ni kutoa mikopo ya zaidi ya Sh. bilioni moja, fedha zinazotokana na mapato ya ndani ifikapo Julai mwaka huu kwa vikundi vyenye sifa.

Aidha, Mashamba alisema lengo la utoaji wa mikopo hiyo ni kutaka kukwamua wananchi kuwaondoka katika umaskini kwa kuinua vipato vyao kwa kutokana na juhudi mbalimbali watazozifanya.

Aliongeza kuwa wananchi walio wengi hujishughulisha na shughuli za ujasiriamali kama uvuvi, kilimo, biashara, useremala ushonaji na biashara ya bodaboda, vitu hivyo huwawezesha kuwapatia kipato cha kujikimu.

Alisema hadi sasa kiasi ambacho kimeshatengwa kupitia fedha ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ni Sh.milioni 401.7 kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka huu.

Kwa mujibu wa mashamba, katika kusaidia makundi hayo, kuna utaratibu wa kuanza kurejesha mkopo huo baada ya miezi mitatu tangu kuchukua ili awaweze kuwa na muda mzuri wa kufanya marejesho.

Hata hivyo, alisema licha kutoa pesa hutoa elimu ya namna ya kusajili na kupanua biashara ikiwa vikundi 1000 vimekamilisha usajili na vingine havina sifa hutumia muda kuelimisha upungufu ya awali.

**Aliongeza kuwa wananchi walio wengi hujishughulisha na shughuli za ujasiriamali kama uvuvi, kilimo, biashara, useremala ushonaji na biashara ya bodaboda, vitu hivyo huwawezesha kuwapatia kipato cha kujikimu.**

# Waziri atoa miezi miwili kuboreshwa huduma afya

**Na Erasto Mgeni, NJOMBE**

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, ametoa miezi miwili kwa timu ya usimamizi wa huduma za afya Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe kufanya mabadiliko ya uendeshaji wa mfumo wa uendeshaji huduma kwenye vituo vya afya wilaya humo.

Aidha, alizuia wataalamu wa idara ya afya kusafiri nje ya wilaya kwa muda huo hadi watakapotekeleza maagizo yake.

Dk. Ndugulile aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara yake ya kikazi wilayani Ludewa, kutembelea miradi ya maendeleo ya afya inayotekelezwa.

"Ninatoa miezi miwili kufanya marekebisho ndani ya mfumo mzima wa uendeshaji wa huduma za afya katika wilaya ya Ludewa," alisema.

Aidha, waziri huyo alisema ametoa maelekezo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Ofisa Afya wa wilaya wasisafiri kwa miezi miwili na muda huo wautumie kutembelea vituo vya afya kuweka mifumo vizuri ili wananchi wapate huduma nzuri na kwa wakati.

Waziri huyo alifikia hatua hiyo baada ya kubaini mfumo wa uendeshaji huduma za afya usiofuata taratibu za kiserikali.

Kadhalika, alimtaka Mkuu wa wilaya hiyo, kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kusimamia kikamilifu maagizo yaliyotolewa.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri, Revocatus Haule, alisema watahakikisha wanatekeleza maagizo yaliyotolewa na kufanya usimamizi na ufuatiliaji wa karibu katika kurejesha mfumo mzuri wa uendeshaji wa huduma za afya wilayani hapo.

Awali, Waziri Ndugulile alikagua ujenzi wa madaraja zinazotekelezwa na kikundi cha wanawake na vijana kilichoanzishwa wilayani hapo, ili kuwasaidia katika kuendesha maisha yao huku akiwapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula (kushoto), akikagua moja ya jalada la ardhi katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma, akiwa katika ziara ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi katika mkoa huo, juzi. Katikati ni Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigoma, Sebastian Siwale na (kulia) ni Karani wa Masijala ya Ardhi, Haiba Mramba. **PICHA: WIZARA YA ARDHI**

# Mfumo wa kielektroniki sasa kuboresha makusanyo Ikungi

**Na Elisante John, SINGIDA**

HALMASHAURI ya Ikungi, mkoani Singida imepanga kutumia Sh. bilioni 36.8 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shughuli nyinginezo kwa kipindi cha mwaka 2020/21.

Aidha, fedha hizo ni kutoka serikali kuu, makusanyo ya ndani na wafadhili mbalimbali, ikiwa ni ongezeko la kutoka Sh. bilioni 25.4 mwaka 2019/2020.

Akiwasilisha makadirio ya bajeti hiyo mwishoni mwa wiki kwenye Kikao cha Ushauri cha Wilaya (DCC), Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ikungi, Justice Kijazi, alisema fedha hizo zitapatikana kwa kuimarisha vyanzo mbalimbali ikiwamo kuimarisha mfumo wa makusanyo kwa njia ya kielektroniki.

Kwa mujibu wa Kijazi, mapendekezo ya bajeti hiyo ni mazuri, kutokana na kujikita kwenye miradi ya maendeleo ikiwamo afya, maji, elimu, kutatua na kuboresha sekta ya kilimo, mifugo na kuwapatia vijana, wanawake na wazee mikopo kwa ajili ya ujasiriamali.

Mkurugenzi huyo alisema halmashauri pekee haiwezi kutatua kero zote zilizopo lakini kwa ushirikiana na wananchi na wadau wengine wa maendeleo watapiga hatua kubwa.

Naye Mwenyekiti wa DCC, ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Edward Mpogolo, aliwataka watumishi, wananchi na wataalamu kushirikiano kikamilifu katika kuhakikisha halmashauri hiyo inazidi kupepea kwenye maendeleo yanayogusa maisha ya wananchi moja kwa moja.

Aidha, alisema mafanikio ya miradi ya maendeleo inapatikana iwapo kutakuwa na usimamizi thabiti, moyo wa uzalendo kutoka kwa wananchi na viongozi wenye dhamana ya kuongoza.

Mkuu huyo kwa wilaya aliwaonya baadhi ya wanasiasa wanaopita kwenye maeneo mbalimbali kuhamasisha wananchi wasishiriki shughuli za maendeleo, kwa madai kuwa ni jukumu la serikali, na kwamba wanakosea sana kufanya hivyo.

"Ndugu zangu, watu wa aina hii siyo rafiki wa maendeleo tunayoyataka, na viongozi wa aina hii tutawapeleka kwenye vyombo vya sheria ili washughulikiwe...bajeti hii leo tunayoshauri hapa ni yetu sote, na mapendekezo yake ni ya wananchi wote, inatoka chini kwenda juu," alisema.

Mwaka jana Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwa ziarani wilayani humo, alieleza kuridhishwa kwake na usimamizi wa fedha za serikali kiasi cha kunufaisha wananchi wengi tofauti na hali ilivyo kwenye wilaya nyingine.

Naye Waziri wa Tamisemi, Suleiman Jafo, aliagiza halmashauri nyingine kwenda kujifunza Ikungi kwa namna walivyotumia fedha kujenga majengo mengi na ubunifu wa kuwa na jengo la ukumbi ambalo watalitumia wao na wakati huo huo linakodishwa na kuingiza kipato kwenye halmashauri.

# Magufuli amkumbuka Mrema Bodi Parole

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amefanya uteuzi wa wenyeviti watano wa bodi za taasisi za Serikali baada ya bodi za taasisi hizo kumaliza muda wake.

Taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, imeeleza juzi kuwa wenyeviti hao wameongezewa muda baada ya vipindi vyao vya awali kumalizika;

Kwanza, Rais Magufuli amemteua Agustino Lyatonga Mrema kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Parole.

Pili, Rais Magufuli amemteua Dkt. Harun Ramadhani Kondo kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Posta Tanzania (TPC).

Kwa mujibu wa taarifa hiyo,uteuzi wa Mrema an Dk. Kondo ulianza Januari 20, mwaka huu.

Pia, Rais Magufuli amemteua Prof. Mayunga Habibu Hemed Nkunya kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC) na vile vile amemteua Fidelis Kashumba Mutakyamilwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Taifa Mipango na Matumizi ya Ardhi.

Kadhalika, Rais Magufuli amemteua Peter Maziku Maduki kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa uteuzi wa Prof. Nkunya, Mutakyamilwa na Maduki umeanza Januari 17, mwaka huu..

Wakati huo huo, Rais Magufuli amemteua Dk. Noel Biseko Logwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa. Uteuzi wa Dk. Logwa umeanza Januari 17, 2020 na kabla ya uteuzi huo, alikuwa Mhadhiri na Mkuu wa Idara ya Akiolojia na Mafunzo ya Urithi (Archeology and Heritage Studies) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Taarifa ya Balozi Kijazi ilieleza kuwa Dk. Logwa amechukua nafasi ya Prof. Audax Mabula ambaye amestaafu.

**Wakati huo huo, Rais Magufuli amemteua Dk. Noel Biseko Logwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa. Uteuzi wa Dk. Logwa umeanza Januari 17, 2020 na kabla ya uteuzi huo, alikuwa Mhadhiri na Mkuu wa Idara ya Akiolojia na Mafunzo ya Urithi (Archeology and Heritage Studies) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.**

# Maofisa ZEC, mawakala vyama wafundwa uandikishaji Pemba

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

MAOFISA wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) na mawakala wa vyama vya siasa Wilaya ya Wete wametakiwa kufuata maelekezo ya Tume ili waweze kuendesha vyema uandikishaji na uhakiki wa wananchi katika daftari la kudumu la wapigakura.

Wito huo umetolewa na Ofisa wa uandikishaji wa ZEC, Omar Zubeir Mbwana, wakati akifungua mafunzo ya siku moja kwa wakala hao, yaliyofanyika Wete.

Omar aliwataka mawakala kufuata sheria na taratibu walizoelekezwa na ZEC na sio vyinginevyo na kuisadia tume hiyo katika kutoa taarifa kwa wananchi wote ambao wameshafikia muda wa kuorodheshwa katika daftari hilo kujitokeza ili waweze kuorodheshwa pamoja na kuhakikiwa taarifa zao.

Aidha, Omar alifahamisha kuwa zoezi litajumuisha makundi mawili ambapo la kwanza ni wale ambao hawajaorodheshwa katika daftari hilo kuwa wapigakura na kundi la pili ni wale ambao walishaorodheshwa.

"Kwa upande wa mpigakura mpya atalazimika kuwa na kitambulisho cha Mzanzibari ambacho kimehakikiwa na kwa yule ambae alishaorodheshwa katika daftari hilo kuwa na kitambulisho kilichohakikiwa pamoja kitambulisho cha kupigakura kwa kuhakikiwa," alielezaOmar.

Mapema Ofisa huyo aliahidi kuwa kila mwananchi ambae ana sifa za kuandishwa katika daftari hilo hatonyimwa haki yake.

"Lengo la mafunzo haya ni kuwasaidia mawakala wa tume na wale wa vyama vya siasa kujua sheria na taratibu ambazo zilizowekwa na tume katika vituo na kuepuka kufanya mambo kinyume cha taratibu, pamoja na ushirikiano kati ya wakala na watendaji ili waweze kufanya kazi zao kwa kuzingatia sheria," alisema Omar.

Omar alitoa wito kwa wananchi wote wa Wilaya hiyo kujitokeza kwa wingi katika kujiandisha katika daftari hilo kwa wenye sifa.

Nae Mohammed Juma Ali kutoka ( CCM) alieleza kuwa amefarajika sana na mafunzo hayo na kuitaka tume hiyo kufanya kazi kwa uadilifu ili wananchi wote waweze kupata haki yao ya msingi.

"Kujiandikisha ni haki ya kila mwananchi wa nchi hii... ninaiomba tume ya uchaguzi, Serikali pamoja na wananchi kwa ujumla kufanya kazi kwa uadilifu ili watu wote wapate haki hiyo," alieleza Mohammed.

Hata Mohammed aliwataka wananchi wote ambao wana sifa za kuorodheshwa katika daftari hilo kufika vituoni walikopangiwa ili kujiandikisha kwa utulivu na utaratibu uliowekwa na tume.

Nae Khamis Abdalla Khamis (CUF) alisema kuwa kwa kiasi fulani mafunzo hayo yamekidhi malengo licha ya kasoro ndogo ndogo ambazo ameziona.

" Niwaombe wananchi wenzangu kutoacha haki yao ya msingi kwani kila mwananchi ambae ameshafikia umri wa kuchagua ama kuchaguliwa ajiandishe ili ifikapo muda wa kupiga kura aweze kuchagua," alieleza Khamis.

Hata hivyo, Khamis aliiomba tume kuwaorodhesha wananchi wote ambao hawajahakikiwa na wanavyo vitambulisho vya zamani kuwaorodhesha na kufanyia uhakiki ili waweze kupata haki yao.

Uandikishaji wa daftari la kudumu la wapigakura kwa Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba linatarajiwa kuanza Januari 25 hadi 29, mwaka huu.



Wachuuzi wa matunda wakiwa wamepanga bidhaa zao jirani na barabara katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana, hivyo kusababisha usumbufu kwa magari na watumiaji wengine wa barabara hiyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wanafunzi Kisarawe wamwangukia Kalemani

**Na Mwandishi Wetu, KISARAWE**

SIKU chache baada ya Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) kusambaza nguzo na kuzisimika katika eneo la Gumba karibu na Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Christon, wilayani Kisarawe mkoani Pwani, wanafunzi katika shule hiyo wamemwomba Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani kuamuru waunganishiwe umeme kwani wanapitia kipindi kigumu.

Wakizungumza na waandishi wa habari wakati wa muda wa mapumziko jana, wanafunzi Brian, Said na Buguzi ambao walijitambulisha kwa jina moja kila mmoja walisema nguzo zimeshasimikwa katika hilo kilichobaki ni kuunganishiwa tu umeme.

Walisema wanamuomba Dk. Kalemani ambaye pamoja na Naibu wake, Subira Mgalu kuhakikisha wananchi wanapata umeme, walisema na kwamba shule imekuwa ikitumia fedha nyingi kwa uendeshaji wa jenereta ambalo kwa sasa limeharibika.

Wanafunzi hao ambao wapo kidato cha nne, walisema kazi kubwa imeshafanyika na kilichobaki ni kuunganishiwa tu umeme kwa utasaidia sana kuinua kiwango cha taaluma shuleni hapo.

Walisema shule imekuwa ikifanya vizuri na endapo umeme utaunganishwa basi wanatarajia kufanya vizuri katika mitihani yetu ya taifa Miezi miwili iliyopita Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, alifanya ziara eneo hilo na kuwataka wakazi wa eneo hilo kushirikiana kikamilifu na wafanyakazi wa Tanesco wanaotekeleza mradi wa kusambaza umeme.

Katika ziara hiyo, Jokate alijionea tatizo la umeme linavyoikabili shule hiyo na kuthibitishiwa na wataalamu wa Tanesco kuwa tatizo la umeme katika eneo hilo litamalizwa katika utekelezaji wa azma ya serikali ya kusambaza umeme vijijini.

"Umeme ni nyenzo muhimu katika kuinua taaluma, na pia huongeza fursa za kiuwekezaji. Umeme wa uhakika utaifanya wilaya yetu kuwa katika nafasi nzuri kitaaluma na kiuchumi," alinukuliwa Jokate.

Hata hivyo, juhudi za kumpata Mkuu wa shule hiyo, August Minja, kuzungumzia suala hilo haikuzaa matunda kwani alikuwa na shughuli ya kikazi nje ofisi.

Mkoa wa Pwani una kaya 254,810, kati ya hizo 169,937 ni kaya za vijijini na ni asilimia 67 ya kaya zote za mkoa. Kaya 84,873 au asilimia 33 ni kaya za mijini.

## Wanawake 615 wakeketwa kwa miezi 3 Hanan'g

**Na Jaliwason Jasson, MANYARA**

HALMASHAURI ya Hanang' mkoani Manyara kwa kipindi cha miezi mitatu iliyopita, imewabaini wanawake 615 wamekeketwa, na kitendo hicho kimeufanya mkoa huo kuendelea kuwa kinara wa ukeketaji.

Hayo yalisemwa juzi Mjini Katesh, na Ofisa Ustawi wa Jamii, Marha Sulle, wakati akizungumza na Nipashe.

Sulle alibainisha kwamba wanawake hao walifanyiwa kitendo hicho cha kikatili kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2019, na kati yao waliobainika ni wale waliofika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya hususan wale wanaliokwenda kujifungua.

Aidha, alisema jamii ya wilaya hiyo inaendelea kufanya ukeketaji kwa dhana potofu kuwa wanafanya hivyo ili wanawake wasichepuke kwenye ndoa zao.

Pia, alisema kuwa dhana potofu imejengeka kwenye jamii hiyo kuwa mwanamke ambaye hajakeketwa hastahili kuolewa, hivyo wanawake wanalazimika kukeketwa ili waolewe.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema mpango mkakati waliyojiwekea ni kuendelea kutoa elimu katika jamii ili kudhibiti ukatili huo unaoendelea kwenye jamii.

"Kibaya zaidi siku hizi wanawakeketa hata watoto wadogo, tena kwa siri sana na tumekuwa tukiwabaini wakati wa kuletwa kliniki," alisema Sulle.

Kwa mujibu wa takwimu za kitaifa, Mkoa wa Manyara ndio unaongoza kwa ukeketaji kwa asilimia 58.

Mmoja wa wazee aliyezungumza na Nipashe kwa sharti la kutokutajwa majina yake, alisema wao wamerithi utamaduni huo kutoka kwa babu zao, hivyo kuwazuia ni kazi ngumu kwa kuwa ni vigumu kwa watu kuacha asili yao.

Vestina Lucas, mkazi wa eneo hilo, alisema wapo wanawake wengine hawafahamu kama sehemu zao za siri zimeondolewa, kutokana na kukeketwa wakiwa watoto wachanga.

**Sulle alibainisha kwamba wanawake hao walifanyiwa kitendo hicho cha kikatili kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2019, na kati yao waliobainika ni wale waliofika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya hususan wale waliokwenda kujifungua.**

# Wadau wa kilimo watakiwa kuwatumia maofisa ugani

**Na Allan Isack, KITETO**

WADAU wa kilimo wilayani Kiteto mkoani Manyara, wametakiwa kubadilika na kuanza kuwatumia maofisa ugani ili kulima kilimo chenye tija ambacho kitawazalishia mavuno mengi.

Wadau hao walisema endapo wakulima watalima kilimo chenye tija, kitawasaidia kuendesha maisha yao na kupata maendeleo ya kimaisha.

Abasi Famau, alisema tatizo kubwa lililopo ni wakulima kuendelea kulima kilimo cha mazoea badala ya kubadilika kwa kulima kitaalamu.

Famau alisema wakulima wengi hawajabadili fikra ya kulima kilimo cha kitaalamu na kutumia mbegu bora na zana za kisasa.

Alisema wakulima wa vijijini wanapaswa kubadilika kwa kutumia kilimo ambacho watawatumia maofisa ugani ambao watawapa ushauri wa kitaalamu.

"Kuna wakulima bado hawajabadilika hata wakati wa palizi wa mazao shambani hayapangilii hivyo, ni vigumu kufikia malengo ya kilimo biashara endapo hatutabadilika," alisema Famau.

Alisema wanapaswa kubadilika kwa kujiunga na vyama vya msingi vya ushirika ambavyo vitawapatia elimu ya mauzo pamoja na kuwatafutia masoko ya uhakika.

"Pamoja na kuwa mazao machache lakini tukijiunga na vyama vya msingi tutaweza kupiga hatua kwa namna moja au nyingine," aliongeza Famau.

Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Tumaini Magessa, amekuwa akiwasisitiza wakulima wa eneo hilo, kuwatumia maofisa ugani ambao wapo kwenye kata zao.

Magessa alisema wakulima wanapaswa kuachana na kilimo cha mazoea na kupata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa maofisa ugani ambao wanapatikana kwa urahisi.

Hivi karibuni, aliagiza madiwani na watumishi wa serikali wenye mashamba wilayani Kiteto kumwonyesha mashamba yao ili aone kama wamelima kitaalamu.



Mganga Mkuu Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Olkokola, wilayani Arumeru, Ezekiel Jackson, akimpima shinikizo la damu mkazi wa Kijiji cha Olkokola, Naishooki Loishiye (39) jana. Loishiye ambaye ni mama mwenye watoto 10 aliojifungulia nyumbani, alisema uwapo wa kituo hicho kilichojengwa kwa nguvu za wananchi utaleta mabadiliko chanya kwa kuwarahisishia kupata huduma za afya. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Huduma kituo afya zawakuna wananchi

**Na Allan Isack, ARUSHA**

WANANCHI wa Kata ya Lemanyata Halmashauri ya Arusha, wamekiri kunufaika na huduma bora za afya zinazopatikana zinazotolewa katika Kituo cha Afya cha Olkokola.

Kituo hicho cha afya tangu kianze kutoa huduma za afya, huduma zinapatikana kwa saa 24.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wengine, Naishooki Loishiye(39), alisema kwa sasa jamii inayowazunguka imepata mwanga na wameanza kubadili mtazamo wao, kuhusu afya ya uzazi na uzazi wa mpango. Alisema jamii imekuwa ikihimiza wajawazito na watoto wa chini ya miaka mitano kuhudhuria kliniki.

Pia aliwataka wanaume kwenda na wenzi wao kliniki, jambo ambalo hapo awali halikuwa likifanyika kulingana na mila na desturi zao.

Naishooki alisema yeye ni mama mwenye watoto 10, amethibitisha kwamba kituo hicho, kimeleta mabadiliko chanya kwa wananchi wa Olkokola, kwenda kupata huduma za afya kituoni hapo.

Alisema kwa upande wake kituo hicho kina faida kwa kuwa alikwenda kujifungulia kituoni hapo, tofauti na awali alikuwa akijifungulia nyumbani, kitendo ambacho ni hatari kwa maisha yake.

Kadhalika, ameishukuru serikali kwa kuwarahisishia upatikanaji wa huduma kwa wagonjwa na kuwapo kwa dawa muhimu na vifaa tiba tofauti na hapo awali.

Aidha, alisema kujengwa kwa kituo hicho, kitapunguza vifo kwa watoto na kinamama ambao walikuwa wakipoteza maisha kwa kujifungulia nyumbani.

Mganga Mfawidhi Kituo cha Afya Olkokola, Dk. Ezekiel Jacob, alisema katika kituo hicho kuna ongezeko kubwa la wagonjwa 700 kwa mwezi sawa na wastani wa asilimia 90.

"Shime wananchi wote tuunge mkono juhudi za serikali kwa kulipa kodi na kuchangia shughuli za maendeleo katika maeneo yetu kwa ajili yetu na Taifa letu kwa ujumla," alisema Dk. Ezekiel Jacob.

# Kata sita Moshi zakosa mawasiliano barabara

Na Godfrey Mushi, MOSHI

MAWASILIANO ya barabara inayounganisha kata sita za Wilaya ya Moshi yamekatika, baada ya kujaa maji yanayotokana na mvua zinazoendelea kunyesha kwa zaidi ya miezi miwili sasa.

Baadhi ya wanafunzi wamekwama kwenda shuleni kuendelea na masomo yao na kurejea majumbani, huku baadhi ya kaya zililalamikia hali mbaya ya miundombinu hiyo kusababisha adha kubwa kwao. Wakizungumza na Nipashe iliyofika jana katika eneo hilo kujionea uharibifu wa miundombinu hiyo, baadhi ya wananchi wa Mabogini, Kahe na Harusini wameeleza kero hiyo inasababisha adha kubwa zaidi kwa wagonjwa na wanafunzi.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kitongoji cha Mabogini Harusini, Abdala Kilango, alisema maeneo hayo hayana mawasiliano ya barabara, baada ya kukatika kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

"Kiujumla hali siyo nzuri hapa kwetu na wafanyabiashara wa mazao na wasafirishaji wa mazao ya mpunga wanaotokea kwenye mradi mkubwa wa umwagiliaji wa Lower Moshi wameshindwa kwenda sokoni na hakuna magari yanayoingia wala kutoka," alisema Kilango.

Naye, Dominata Mboya, mkazi wa Mabogini, alieleza masikitiko yake kuhusiana na ubovu wa miundombinu ya barabara akisema kama hali itaendelea hivyo jambo hilo litaathiri zaidi wagonjwa na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Barabara iliyokatika mawasiliano ya Mabogini/Kahe yenye urefu wa zaidi ya kilomita 22 inaunganisha kata sita za Wilaya ya Moshi.

Kwa upande wake, Shafii Mlacha, mkazi wa Kahe, alisema kwa sasa vyombo vya usafiri vimekuwa vikilazimika kupita katika mashamba ya watu ili kupenya na kuingia barabara kuu maeneo ambayo hayajaathirika.

Alipotafutwa kuzungumzia madai hayo ya wananchi, Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura) Wilaya ya Moshi, Mhandisi Roy Johansen, alisema tayari hatua za kukabiliana na tatizo hilo limeanza kuchukuliwa.

"Tayari tumeshaanza kuchukua hatua na tumempata mkandarasi kutoka Kampuni ya KGG ya jijini Dar es Salaam ambaye atafanya kazi ya kurejesha mawasiliano ya barabara hiyo pamoja na kuijenga baada ya kutengewa kiasi cha Sh. milioni 600," alifafanua Mhandisi Johansen.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, ambaye alifika eneo la tukio na kuona kero hiyo, alisema hatua za kudhibiti maji hayo zitaanza mapema kesho kwa mkandarasi kuanza kazi ya kujaza kifusi ili kufungua mawasiliano wakati wakisubiri mvua kukatika.



Moja ya maeneo ya Kijiji cha Mabogini, Wilaya ya Moshi, ambayo yamekosa mawasiliano ya barabara, baada ya mvua kubwa kunyesha jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Warioba aitupia macho sheria inayolinda haki wenye ulemavu

Na Godfrey Mushi, MOSHI

SERIKALI imesema inaendelea kufuatilia kwa karibu Sheria Namba 9 ya Mwaka 2010 inayohusu Haki na Ulinzi kwa watu wenye ulemavu, namna inavyotekelezwa na halmashauri za wilaya mkoani Kilimanjaro ikiwamo mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kwa makundi maalum.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, alisema sheria hiyo pamoja na mambo mengine inataka kuhakikisha walemavu wanapatiwa haki hiyo ikiwamo pia masuala ya ajira, elimu, afya na utengamao wa maisha yao ili kuondokana na dhana potofu ya utegemezi kwa kundi hilo.

"Huu ni mkakati wa serikali wa kuhimiza kila wakati utoaji wa mikopo ya uwezeshaji kiuchumi makundi maalumu hasa na watu wenye ulemavu. Kimsingi sheria hiyo inalenga kutoa fursa kwa makundi hayo kuwa na kipato halali na kufurahia ustawi wa nchi," alisema.

Alisema serikali inaendelea na jitihada zake za kuwawezesha watu wenye ulemavu kwa kuwatengea asilimia mbili katika kila halmashauri, mikopo ambayo haina riba na inayolenga kuwasaidia kujikwamua kiuchumi.

"Ipo haja ya kila mwenye ulemavu kujitahidi kujishughulisha na shughuli ya kumwongezea kipato kwa kuzingatia uwezo aina ya ulemavu wake, kwa kuwa serikali inaendelea kuweka mkazo katika kuliangalia kundi hili."

Zaidi alieleza: "Huu ni wakati sahihi wa kundi hili kuangaliwa na kupatiwa elimu ya ujasiriamali ili kujikimu katika mahitaji yao na familia zao kwa ujumla." Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii ya Manispaa ya Moshi, Rose Minja, alisema halmashauri hiyo imetoa mkopo wa Sh. milioni 100 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Kwa mujibu wa Minja, hivi sasa katika Manispaa ya Moshi kumejitokeza mwitikio kwa vikundi vya watu wenye ulemavu kuomba mikopo hiyo ya uwezeshaji kiuchumi.

"Kwa sasa mikopo hiyo inatolewa chini ya sheria mpya ambayo ni lazima vikundi viwe vinatekeleza mradi wa pamoja, ambapo wanavikundi pia wameeleza changamoto za utekelezaji wa mradi pamoja na kimsingi mambo yamebadilika na sasa ni tofauti na ilivyokuwa awali," alieleza ofisa huyo.

## Vijiji kikwazo cha ukusanyaji mapato

Na Mwandishi Wetu, SIHA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Siha, imeshtukia ujanja unaofanywa na watu waliopewa dhamana ya kukusanya mapato katika ngazi ya vijiji, kuwa ndio chanzo cha kutofikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato yake kwa asilimia 80.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Ndaki Muhuli, alisema waligundua udhaifu huo baada ya kufanya uchunguzi wa namna mapato ya ndani yanavyokusanywa vijijini.

Alikuwa akizungumza jana katika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani kilichoketi kujadili mpango wa bajeti wa mwaka 2020/2021.

"Tulifanya uchunguzi na kubaini ukusanyaji wa mapato uliokuwa ukisimamiwa na vijiji vyenye vyanzo vya mapato walikuwa wanakusanya na kuzipeleka halmashauri.

Sasa asilimia 15 ya fedha hizo zilikuwa zinarudi vijijini ingawa walikuwa hawawezi kukusanya vizuri, mwisho wa siku kinachokuja halmashauri ni nusu, nusu kinabaki kwa wakusanyaji," alisema.

"Kijiji hakifaidiki na halmashauri haifaidiki, kwa sababu hiyo tukaona tuweke wasimamizi wengine kukusanya mapato, tumewapa mikataba mipya inayowataka kila baada ya siku moja kupeleka fedha benki na akikiuka mkataba unakuwa umevunjika rasmi."

Maeneo yaliyokuwa na vyanzo vya mapato na yaliyokuwa yakisimamiwa na vijiji ni lango la Ngarenairobi, Lawate, kituo cha mabasi Sanya Juu pamoja na minada ya mifugo ya kuuzia na kununua mifugo.

Alisema tangu wafanye mabadiliko hayo katika ukusanyaji wa mapato ya ndani, wamejitathmini na kuona matokeo chanya na sasa wamefikia asilimia 46 ya ukusanyaji mapato.

Aidha, akitoa nasaha zake katika kikao hicho, Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Joseph Mabiti, aliwataka madiwani wa halmashauri hiyo kuwa wabunifu wa katika kubuni miradi ya maendeleo na wawe wasimamizi wa karibu wa miradi hiyo.

**"Kijiji hakifaidiki na halmashauri haifaidiki, kwa sababu hiyo tukaona tuweke wasimamizi wengine kukusanya mapato, tumewapa mikataba mipya inayowataka kila baada ya siku moja kupeleka fedha benki na akikiuka mkataba unakuwa umevunjika rasmi."**

TUJIKUMBUSHE



Ukurasa 18

**Mwaka wa uchaguzi waganga, wapiga ramli wasipewe nafasi**

Rais Tshisekedi awatishia kuwafuta kazi mawaziri



Ukurasa 17



Ukurasa 15

**Mkongwe Wasira ageukia kuinua wanawake, vijana**


# siasa

JUMATANO JANUARI 22, 2020

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 19

**Haftar mbabe anayepasua vichwa viongozi AU na EU**

SUBIRA MGALU:

# Nimevaa kiatu cha Bibi Titi baada ya kupita miaka 52

• Mhasibu Mkuu aliyeukwaa uwaziri

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

"WANANCHI wa Mkoa wa Pwani, wamefarijika kwa nafasi hii niliyoteuliwa na Rais kuwa Naibu Waziri wa Nishati.

Nafasi niliyo nayo kwa Mkoa wa Pwani, ni mbunge mwanamke wa pili kuwa Waziri, baada ya Titi Mohamed mwaka 1965 alipokuwa Waziri Mdogo (Naibu Wazairi), ni miaka 52 imepita, tangu wakati huo hatukupata uteuzi nafasi ya waziri" anaeleza Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu.

Subira anasema, si kwamba kwa kipindi hicho chote hakukuwapo wanawake ambao wanafaa kuwa mawaziri, walikuwepo wengi lakini katika awamu ya tano imempendeza kumteua kwa nafasi hiyo.

**INAENDELEA UK.16**



Naibu Waziri Subira Mgalu. **PICHA: MAKTABA.**

**Salah: Inakuwaje wanawake wamemwondoa Al-Bashir wanaenguliwa** Ukurasa 20

KUELEKEA ROBO KARNE MKUTANO BEIJING

# Wanawake wakubali mwelekeo mzuri, Mongella awapa darasa




Balozi Getrude Mongella. **PICHA: MAKTABA**

**Na Mwandishi Wetu**

SEPTEMBA mwaka huu, itatimia miaka 25 tangu kufanyika kwa mkutano wa Umoja wa Mataifa (UN) kuhusiana na maendeleo ya wanawake, uliofanyika mwaka 1995, katika jiji la Beijing nchini China.

Mkutano huo ulifanyika Septemba mwaka 1995, ukisimamiwa na mwanadiplomasia maarufu nchini, Balozi Getrude Mongella, katika kusanyiko la Beijing zilitolewa ahadi za kurekebisha sheria zilizokuwa zinawabagua wanawake.

Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kuwashirikisha na kuwawezesha wanawake, katika maendeleo, ili kuimarisha mapambano dhidi ya umasikini na kufikia maendeleo endelevu hiyo yote ni kwa wanawake kushiriki kwenye shughuli za kimaendeleo.

Aidha, Beijing pamoja na mambo mengine mengi, ililenga kumkomboa mwanamke na zilipitishwa sera na programu ambazo zitastawisha usawa wa jinsia, katika maisha ya watu.

Wajumbe kwenye mkutano huo wa nne wa viongozi duniani ndiyo waliotoa ahadi hizo, Septemba mwaka mwaka 1995, yote hayo yalilenga kuhakikisha wanawake hawabaguliwi kwa namna yoyote na wanakuwa chachu ya maendeleo.

Wakati huu wa kuelekea miaka 25 ya Beijing, wadau mbalimbali wameanza kukutana katika semina, warsha na makongamano kufanya tathmini jinsi utekelezaji wa maazimio ulivyo, tangu kufanyika kwa mkutano huo.

Katika moja ya warsha iliyowakutanisha washiriki zaidi ya 100 kutoka mikoa mbalimbali nchini, wanasema miaka 25 baada ya Beijing, angalau sasa kuna nuru, lakini bado wanawake wanaendelea kubaguliwa.

> Tunapozungumzia ushiriki wa wanawake katika uongozi, jamii inatakiwa iliangalie hilo kwa mapana yake, kwani ushiriki wao katika uongozi siku zote umekuwa na manufaa mengi.

Warsha hiyo iliyoshirikisha wawakilishi wa makundi mbalimbali ya wabunge, madiwani, wanasheria, waandishi wa habari na wanafunzi wa vyuo na sekondari, iliandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Ni kuelekea mwishoni mwa mwaka jana TGNP ilipokutanisha wadau hao kwa kushirikiana na Chama cha Wanasheria Wanawake (Tawla), asasi ya Landesa, Msichana Initiative, Haki Ardhi, Haki Elimu, Care International na Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa), huku Balozi Mongella akitoa neno.

### WITO KWA WANAWAKE

Kiongozi huyo ambaye alikuwa mgeni rasmi, anatoa neno kwa kuwaasa wanawake kuhusu umuhimu wa kuchagua viongozi wanaojali maslahi ya wanawake, katika uchaguzi mkuu wa 2020.

"Chagueni viongozi wanaoweka na kutekeleza ajenda ya wanawake kwenye Ilani yao ya uchaguzi. Wanawake hatutaki kuwezeshwa kwa sababu tunaweza, tunataka kuondolewa vikwazo katika kila hatua," anasema.

"Balozi Mongella anaendelea kusema: "Kama ni mawe au kokoto na miba tusaidie kuviondoa tusonge mbele. Tanzania ya viwanda haitajengwa kwa maji yanayochotwa na wanawake kwenye ndoo na nishati ya kuni zinazokatwa na wanawake na kubebwa kichwani."

Anasema, katika harakati hizo, wanawake wanapaswa kuwashirikisha wanaume, na wao wakumbuke kwamba wanawake ndiyo wamewazaa, hivyo hawawezi kuwaacha nyuma.

"Wanawake tuwajengee uwezo vijana wa kiume watambue mchango wa wanawake, katika jamii na pia waungane na vijana wa kike, katika kuijenga nchi yetu," anasema.

### TATHMINI YA TGNP

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, anashauri wanawake wasiishie kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapigakura, bali wakati wa uchaguzi wajitokeze kuomba nafasi ya uongozi.

"Tunapozungumzia ushiriki wa wanawake katika uongozi, jamii inatakiwa iliangalie hilo kwa mapana yake, kwani ushiriki wao katika uongozi siku zote umekuwa na manufaa mengi," anasema Liundi.

Liundi anasema, wakati mwingine tatizo linaweza kuwa katika vyama vya siasa kwa vile vyote 19 vilivyosajiliwa, hakuna hata kimoja, ambacho mwenyekiti wake ngazi ya taifa ni mwanamke.

Hata hivyo, tunashukuru kwamba, kwa mara ya kwanza tangu nchi hii ipate uhuru, imekuwa na Makamu wa Rais mwanamke, Samia Suluhu Hassan na kwamba hiyo ni hatua ya kupongezwa.

"Tunashukuru hata kwenye bunge kwani liliongozwa na Spika wa kwanza mwanamke Anne Makinda na pia bunge la sasa lina Naibu Spika mwanamke Dk. Tulia Akson," anasema.

Devote Mlay ni mwanachama wa TGNP, anasema serikali, imeweka sheria na mipango bora kwa ajili ya kupunguza ukatili wa kijinsia, ingawa bado kuna changamoto kwa watekelezaji wa sheria hizo kuanzia ngazi ya serikali ya mtaa na kata.

"Madaktari, waendesha mashitaka pamoja na mawakili wanaleta ugumu katika kutekeleza majukumu yao hali inayomfanya muhanga kubaki njia panda," anasema Mlay.

Aidha, Mlay anasema, baadhi ya Watanzania hasa vijana wamekuwa wakitumia mitandao ya kijamii vibaya badala ya kupashana habari za mambo ya ukatili wa kijinsia, na kubaki kushabikia mambo yasiyo na maana hasa ya ngono na kusababisha kesi nyingi za ukatili wa kijinsia kuishia juu juu.

### MAONI YA WATAALAM

Mtaalamu wa Masuala ya jinsia Leticia Mukurasi anawaambia washiriki wa semina ya kufanya tathmini ya mkutano wa Beijing kuwa maendeleo hasa katika elimu watoto wa kike wanajitahidi kwamba wako sawa na wa kiume.

"Kwa tathmni yangu ndogo ni kwamba hayo yamefanyika vizuri, lakini baadhi ya maeneo bado hawajawa sawa ingawa wanajaribu kuwa na uwiano sawa na watoto wa kiume," anasema Mukutasi.

Anasema, katika masuala ya afya na uchumi pia wanawake hawapo nyuma wanajifungulia hospitalini, pia kiuchumi wanajaribu kuondokana na umaskini kwa njia mbalimbali ikiwamo biashara kubwa na ndogo.

# Mkongwe Wasira ageukia kuinua wanawake, vijana

Na Sabato Kasika

## • Aunda taasisi maalumu, aanzia kazi Bunda



Stephen Wasira. **PICHA: MAKTABA**

BAADA ya kimya cha muda mrefu, mwanasiasa mbobezi aliyetumikia serikali tangu awamu ya kwanza, Stephen Wasira, ameibuka kivingine na sasa amejikita katika kuhudumia jamii akiwalenga vijana na wanawake, atakaowafikia kupitia taasisi aliyoanzisha na kuzindua hivi karibuni.

Wasira anasema, ameanzisha asasi kwa lengo la kuwatafutia wanawake na vijana fursa za kimaendeleo na kiuchumi na kuwaunganisha na taasisi za fedha, ili waweze kukopeshwa na kufanya shughuli mbalimbali.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili wiki hii, mkongwe huyo wa siasa ambaye ni mwenyekiti na mwanzilishi wa taasisi ya Stephen Wasira Foundation, ambayo ilizinduliwa rasmi wiki iliyopita mjini Bunda mkoani Mara na mkuu wa mkoa huo, Adam Malima, ikiwa ni ishara ya kuanza rasmi kazi kwenye jamii.

Mbali na kuwatafutia fursa hizo, anasema, Stephen Wasira Foundation pia ina jukumu la kusaidia kufanikisha uandishi wa andiko la miradi, kuwezesha makundi hayo kunufaika na fursa mbalimbali zinazopatikana.

Anasema, wanawake na vijana ni makundi yanayokabiliwa na changamoto mbalimbali za kimaendeleo ikiwamo umaskini, ukosefu wa ajira na matatizo ya afya, hasa kwa akina mama.

Anaeleza kuwa ni muhimu jamii kuelewa kuwa taasisi yake haifanyi biashara ya fedha za kukopesha, bali ni kiungo wa kuunganisha makundi hayo kwa ajili ya fursa zitakazowawezesha kupata maendeleo.

**SWALI: Stephen Wasira imezinduliwa rasmi wiki iliyopita mjini Bunda mkoani Mara. Je, ilianzishwa lini na makao makuu yako wapi?**

**JIBU:** Stephen Wasira Foundation iliandikishwa Julai 20 mwaka 2018, chini ya sheria ya wadhamini, sura ya 318 RE ya mwaka 2002 kuwa taasisi isiyo ya kiserikali na isiyo ya kibiashara au faida na inayoongozwa na bodi ya wadhamini. Binafsi nina uzoefu wa muda mrefu, katika kutumikia jamii yetu na uelewa nilioupata kwa kujua changamoto za kimaendeleo zinazowakabili vijana na akina mama wa Mkoa wa Mara na hususan Wilaya ya Bunda na Tanzania kwa ujumla ndiyo maana nikaanzisha taasisi hii ambayo usajili wake ni namba 5574. Na ilikuwa haijazinduliwa rasmi kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo, ambazo ziko juu ya uwezo wetu, lakini sasa ambacho kilitukwamisha kimeisha na tumeanza kazi ya kutafutia fursa makundi ya wanawake na vijana, ili kuhakikisha yanainuka, kwani ndiyo makundi muhimu kwa maendeleo ya nchi. Lakini nisisitize kuwa shughuli zetu siyo za faida. Vilevile makao makuu ya taasisi yetu yapo Msasani jijini Dar es Salaam.

> Waswahili wanasema wema unaanzia nyumbani, hivyo hata mimi nimeanzia kwetu Bunda. Wala hilo halina uhusiano wowote na mambo ya siasa na vilevile siasa haziwezi kuzuia mambo ya maendeleo.

**SWALI: Makao makuu yako Msasani Dar es salaam, lakini imezinduliwa rasmi Bunda, kwanini uzinduzi ufanyike Bunda na siyo maeneo mengine au mkoa mwingine? Hakuna mkakati wowote wa kisiasa hapa?**

**JIBU:** Waswahili wanasema wema unaanzia nyumbani, hivyo hata mimi nimeanzia kwetu Bunda. Wala hilo halina uhusiano wowote na mambo ya siasa na vilevile siasa haziwezi kuzuia mambo ya maendeleo. Hivi kweli inawezekana mtu aache kufanya shughuli za maendeleo kwa kuhofia kusemwa kwamba ana mikakati ya kisiasa?

Wenye mawazo hayo ninawaomba wayaondoe kabisa, sisi tumeanzisha taasisi kushughulikia changamoto za vijana na wanawake, hivyo tusiingizwe kwenye mambo ya siasa. Kwa taarifa yako ni kwamba tunataka kufungua ofisi Bunda, kwani kwa kawaida wema unaanzia nyumbani, nasi tunafanya hivyo na kisha tutaendelea kujipanua kadri inavyowezekana. Lakini nirudie kusema kwamba hakuna uhusiano wowote na masuala ya siasa, wala siasa haziwezi kuzuia maendeleo. Ndiyo maana tumegawa vitabu 1,450 vyenye thamani ya Sh. milioni 16, katika shule 29 za sekondari za Wilaya ya Bunda yenye majimbo matatu ya Bunda Vijijini, Bunda Mjini na Mwibara wakati wa uzinduzi wa taasisi yetu. Pia nikwambie kwamba wakati wa uzinduzi, kulikuwa na wawakilishi kutoka vyama mbalimbali vya siasa kuanzia CCM Chadema, NCCR-Mageuzi na vingine. Kwa maana kwamba tunaunganishwa na Utanzania siyo itikadi za kisiasa.

**SWALI: Sababu za kuweka makao makuu ya taasisi Msasani Dar es Salaam ni zipi, wakati taasisi inajishughulisha na wanawake na vijana wa Mkoa wa Mara hususan wilayani Bunda?**

**JIBU:** Kimsingi, Dar es Salaam ndiko kwenye fursa nyingi, hivyo tumeona makao makuu yaendelee kuwa huku na tunapopata hizo fursa tunawajulisha walengwa na kuwaunganisha ili waweze kuzichangamkia kwa ajili ya maendeleo yao. Hiyo ndiyo sababu kubwa ya masingi ambayo imetufanya tuweke makao makuu ya taasisi yetu jijini Dar es Salaam.

**SWALI: Muda mrefu kidogo umekuwa kimya mara baada ya kumalizika kwa kampeni za uchaguzi wa marudio ya ubunge wa jimbo la Kinondoni Dar es Salaam. Kulikuwa na nini hadi uwe kimya na sasa umeibuka na taasisi hiyo?**

**JIBU:** Labda nianze na hili la taasisi, kwamba kuwa na taasisi siyo jambo la ajabu, lakini pia suala la mimi kukaa kimya na kisha kuibuka na taasisi yangu ni la kawaida tu. Kwanza kabisa kwa wale wanaonifahamu, wanatambua kuwa mimi siyo mtu wa kupenda kuongeaongea sana, na ndivyo nilivyo. Kukaa kimya siyo kwamba sipo, na siyo lazima kuongea sana, ili iweje? Lakini nikuthibitishie kuwa kuzindua taasisi yangu hakuna uhusiano wowote na mambo ya siasa, hasa wakati huu nchi inapoelekea kwenye uchaguzi mkuu. Lengo letu ni kusaidia wanawake na vijana kupata fursa ya kujiletea maendeleo, na uwezo huo tunao, kwani tuna uzoefu wa kutosha.

**SWALI: Vipi kuhusu kuwania ubunge wa jimbo la Bunda Mjini, katika uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika mwishoni mwa mwaka huu, una mpango huo au umeachana na siasa?**

**JIBU:** Hayo masuala ya siasa yaweke pembeni tuzungumzie Stephen Wasira Foundation na majukumu yake na jinsi, ambavyo imejipanga kuwasaidia wanawake na vijana. Hilo swali halina nafasi ila umeamua kulichomekea. Lakini jambo la msingi, ambalo ninaona linafaa kujadili ni kuhusu hii taasisi. Hayo mengine tuachane nayo kwanza na tusiulizane maswali kuhusu ubunge wa Bunda Mjini wakati kuna majukumu mengine ya kufanya katika jamii inayotuzunguka.

**SWALI: Taasisi yako bado ni changa na ndiyo kwanza ina miaka miwili na ilizinduliwa karibuni ina malengo mengine yapi ya zaidi kwa baadaye?**

**JIBU:** Ndiyo, tuna malengo makubwa. Kwanza ni kuimarisha taasisi na pia kupanua shughuli zetu ikiwamo kusaidia jamii. Kwa mfano, hivi karibuni tumetoa msaada wa vitabu 1,450 kwa sekondari za wilaya Bunda, hivyo ndivyo tunataka kujikita kwenye jamii. Kwa hiyo tuombeane ili tufikie malengo hayo kwa kutoa mchango wetu kwenye jamii. Jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali katika kuboresha maisha ya Watanzania, hatuna budi kuziunga mkono, kwani kuboresha huduma za jamii kunahitaji ushirikiano, na taasisi yetu imekuja muda muafaka wakati kuna uhitaji wa mambo mbalimbali ikiwamo uboreshaji wa sekta ya elimu.

# Nimevaa kiatu cha Bibi Titi baada ya kupita miaka 52



Zainabu Vulu, mmoja wa wabunge wa viti maalumu mkoani Pwani.



Mwanasiasa wa kwanza mwanamke wa Tanzania, Bibi Titi Mohamed, akiwa jukwaani na Mwalimu Julius Nyerere wakati wa harakati za Uhuru. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**INATOKA UK.13**

Huyo ni mbunge wa viti maalum kwa mkoa wa Pwani, ambaye ameteuliwana na kuandikwa historia nyingine kwa upande wa wabunge wanawake.

Mbunge huyo anasema, mbali na mkoa kuandika historia ya kuwa na mbunge mwanamke anayetumikia nafasi yake, wizara hiyo nyeti haikuwahi kuwa na kiongozi mwanamke wa ngazi ya juu.

"Imempendeza mheshimiwa Rais John Magufuli, kuniteua katika nafasi hii ya Naibu Waziri katika wizara ambayo haijawahi kuwa na kiongozi mwanamke katika nafasi ya waziri au naibu. Kwa hiyo, hapa utaona namna gani wananchi nao wana mategemeo na utendaji kazi wangu," anasema.

Subira anaelezea nafasi nyingine alizowahi kushika kabla ya kuwa Mbunge Viti Maalumu, ni pamoja na Mkaguzi wa Hesabu katika ofisi za Mkoa wa Pwani na Mhasibu Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu.

> Mbali ya nafasi hizo pia nimewahi kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (MNEC) mwaka 2000.

Anasema, katika nafasi zote hizo alizitumikia vyema na kwa mafanikio, akiongeza:" Mbali ya nafasi hizo pia nimewahi kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (MNEC) mwaka 2000. Nilipotoka katika nafasi hiyo, ndio nikaingia katika ubunge viti maalumu."

**MFUMO DUME?**

Subira ana maoni kwa mfumo dume uliopo katika jamii inayomzunguka Mgalu, akiueleza:" Mfumo dume si wa kiwango cha kutisha, kwani wanaume wengi ndio waliokuwa wananiunga mkono hata kipindi nilipogombea nafasi ya NEC. Hivyo, dhana hiyo ipo, lakini si ya kutisha".

Anasema, ingawa wapo wanaoamini kuwa mwanamke pekee yake hawezi kuongoza lakini, yeye anachosimamia ni kwamba anaweza kutokana namna wanaume walivyomwamini na sasa wanaendelea kumpa ushirikiano.

**NAFASI UBUNGE**

Subira anarejea nafasi yake ya ubunge wa Viti Maalum, akisema, amefanikiwa kuunda vikundi mbalimbali vya wajasiriamali, lengo ni kumuwezesha mwanamke ajishughulishe na kuachana na utegemezi.

Anasema vikundi hivyo vimepatiwa elimu ya ujasiriamali ambavyo vipo katika jimbo la Chalinze, katika kata za Msoga, Kimange, Bwilingu na Miono.

Mbunge huyo mwanamke, anasema amewezesha baadhi ya shule ya sekondari kupata msaada wa maktaba ya kisasa, kupitia wahisani ambao ni wadau wa maendeleo katika sekta ya elimu.

"Kuna kazi nyingi nimefanya kama mbunge katika Mkoa wa Pwani. Nimeshirikiana na serikali na wadau mbalimbali kuondoa changamoto kwa wananchi tunaowahudumia, ikiwamo Daraja la Mpiji, Kata ya Pangani" anaeleza.



Naibu Waziri Subira Mgalu. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**CHANGAMOTO ZAKE**

Kuhusu changamoto anazokutana nazo, Subira anasema daima hazijakwamisha jitihada za mwanamke katika kuongoza, lakini anakiri katika upande wa pili wa shilingi kuwapo wanawake ambao ni kikwazo kwa wenzao.

"Wanawake sisi kwa sisi tuna changamoto kubwa. Kama unavyofahamu mimi ni mbunge ninayechaguliwa na wanawake. Maneno mengi pamoja na kazi unazofanya bado unakutana na vikwazo, lakini kwangu nachukulia kama fursa na kuendelea kufanya kazi kwa bidii," anasema Subira.

**MWENYEKITI CHALINZE**

Akizungumzia utendaji wa naibu waziri huyo, Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Pwani na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chalinze, Saidi Zikatimu, anamtaja mbunge huyo kuwa ni mfano wa kuigwa na jamii ya Mkoa Pwani.

Zikatimu anasema, nafasi aliyoipata Mgalu, ameonyesha namna wanawake wakipewa nafasi wanaweza kuwakilisha vizuri hasa kutoka kwa Mkoa wa Pwani.

"Mwanamke kufanya kazi ni wajibu. Mfumo dume ni mawazo ya mtu na dhana potofu ambayo imejengeka kwa baadhi ya watu, wapo wanawake wamefanya kazi na wamedhihirishia umma kuwa, kuongoza sio lazima uwe mwanaume.

"Tumeona Mgalu anavyofanya kazi, Ummy Mwalimu na Joyce Ndalichako, tusiwaweke wanawake nyumbani, tukidhani hawawezi kufanya kazi kwenye jamii," anaeleza Zikatimu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Mkuranga, Juma Abed, anasema kazi anayoifanya Subira Mgalu, ameonyesha uhodari wa hali ya juu na kudhihirishia, umma kuwa wanawake wanaweza kutumikia nafasi za juu.

> Tumeona Mgalu anavyofanya kazi, Ummy Mwalimu na Joyce Ndalichako, tusiwaweke wanawake nyumbani...

Abed anasema, Pwani wana kila sababu ya kujivunia uwepo wa Naibu Waziri wa Nishati kwa kazi anazozifanya, na haoni sababu ya kuendelea mfumo dume kwenye jamii, kwani kazi zinazofanywa na viongozi wanawake baadhi ya wanaume hawawezi kufanya hivyo.

Anaongeza kuwa nafasi aliyo nayo Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, mawaziri na manaibu waziri kwenye serikali iliyopo, wanaonyesha namna wanawake wanavyomudu wajibu wao.

Hadi sasa Mkoa wa Pwani una wabunge wa Viti Maalumu wa Chama Cha Mapinduzi watatu, Subira Mgalu, Hawa Mchafu na Zainab Vullu, ambao ni injini ya maendeleo kwenye maeneo mbalimbali, ikiwamo kuanzisha vikundi vya ujasiriamali, kutoa misaada mbalimbali kwa makundi tofauti na katika huduma za jamii.

## Rais Tshisekedi awatishia kuwafuta kazi mawaziri



Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Félix Tshisekedi. **PICHA: MTANDAO**

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Félix Tshisekedi, ametishia kuwafuta kazi mawaziri wake na hata kulivunja bunge, iwapo washirika wake wa kisiasa ambao wanaegemea katika mrengo wa rais wa zamani Joseph Kabila, wataendelea kumdharau.

Tshisekedi alisema kuna baadhi ya mawaziri ambao wamekuwa wakimwambia kuwa, wanapata shinikizo na kusisitiza kuwa, hana nia ya kulivunja bunge lakini, iwapo mzozo utazuka, atalazimika kufanya hivyo.

"Ninayoyasema ndiyo ambayo yatafanyika na ndiyo nimedhamiria kufanya ndiyo yatakayotekelezwa, sababu raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo wamenipa jukumu la kuwaongoza na bila shaka wataniuliza nini nimewafanyia kwa muda wa miaka mitano, " anasema.

"Wamenipa taabu sana wanasubiri nishindwe kutimiza kazi yangu, wananisukuma kufanya mambo ambayo sijapanga kuyafanya, kama ni kuvunja bunge naweza kulivunja, na kama itabidi nifikie hatua hiyo sitachelewa kufanya hivyo," aliongeza.

Katika hatua nyingine, Tshisekedi ametupilia mbali madai ya kuwapo mpango wa kuigawa nchi hiyo, akisema mazungumzo hayo hayana msingi na ni mbinu za kutaka kuchelewesha ajenda ya maendeleo kwa taifa hilo.

Aidha, ameeleza kuwa anashangazwa na namna ambavyo baadhi ya watu wanataka kulikuza suala la kuigawa vipande nchi hiyo, kiongozi huyo akisisitiza kuwa hakuna atakayejaribu kufanya hivyo.

Matamshi yake yamekuja baada ya majuma kadhaa yaliyopita baadhi ya wanasiasa kuzituhumu nchi za ukanda huo na baadhi ya wanasiasa wa DRC kutaka kuligawa vipande eneo la mashariki mwa Congo.

Rais Tshisekedi ambaye amekuwa madarakani kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa, aliingia katika maelewano na chama cha zamani wa rais Joseph Kabila cha PPRD, kushirikiana naye katika serikali yake, baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2018.

Hivi karibuni wakati Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Tshisekedi , akielekea kusherehekea mwaka mmoja tangu achukue hatamu ya uongozi wa nchi, joto la kisiasa linaendelea kuikumba nchi hiyo, akikabiliana na upinzani mkali.

Rais Tshisekedi alikabiliwa na upinzani, huku baadhi ya wakosoaji wake ikiwa ni pamoja na mpinzani wake mkuu Martin Fayulu, wakiendelea kupinga uongozi wake.

Akiwa katika mji wa Kikwiti, Martin Fayulu, mpinzani wa serikali anasema mwaka 2020 ni mwaka wa ukombozi wa Congo, huku akitangaza maandamano ya amani kuanzia Januari 17 kukumbuka mauaji ya baba wa taifa nchini Congo Emery Patrice Lumumba.

Kupitia maandamano hayo, mgombea huyo ambaye alishindwa katika uchaguzi wa urais uliopita anatarajia kukemea kile alikichoita mpango wa Kabila juu ya ukandamizaji wa nchi.

Radio Ufaransa

# Mwaka wa uchaguzi waganga, wapiga ramli wasipewe nafasi



Kazi za waganga wa kienyeji hudaiwa kuhitajika zaidi wakati wa uchaguzi. **PICHA: MTANDAO**

**Na Gaudensia Mngumi**

DUNIANI watu wanaokumbukwa na kusifiwa ni mashujaa waliotenda mambo makubwa, tena baadhi walitoa maisha yao kwa ajili ya mtu, taifa na hata dunia nzima.

Kujitolea na kujitoa kwa moyo wa dhati kufanya mambo ni ushujaa ambao unaifanya taifa, jamii na hata duniani pengine iwaone ni watu wa muhimu ambao hata kama wamefariki lakini kazi zao na urathi (legacy) zao zinaishi.

Wapo mashujaa wengi wakiwamo Mababa wa Afrika , Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa Ghana Kwame Nkurumah na shujaa Nelson Mandela, hawa wanaheshimika kwa ushujaa na kufanya mambo yaliyotukuka. Japo wamefariki dunia wanaishi, wanakumbukwa na wanaendelea kuenziwa.

Lakini wakati mwingine, miongoni mwa watu wanaotwaa ushujaa na kuonekana kuwa ni watu wa muhimu ni waganga na wapiga ramli. Wapo baadhi ya wananchi wakiwamo wafanyabiashara, wanasiasa na watumishi wa umma na sekta binafisi , wanaowathamini waganga wa kienyeji na hata kuwaona kama mashujaa wao.

Wanaweza kuwa mashujaa licha ya kwamba wanatuhumiwa kuwa ni wahusika wakuu kwenye mikakati ya wanasiasa wengi kwenye nyakati hizi za uchaguzi kama ulivyo mwaka huu.

> Tunapozungumzia siasa tukumbuke mauaji ya albino ambayo hadi leo yanazihuzunisha familia zao, lakini pia kuna mashambulizi dhidi yao.

Waganga hawa kupitia ramli zao wanapeleka msiba kwa watu wengi, kwani wanadaiwa kuwaelekeza watu pengine wenye nia za kugombea nafasi mbalimbali zinazojiri kwenye uchaguzi kuleta viungo vya binadamu na kusababisha mauaji ya watoto, wanawake na hata albino nyakati hizo ili kushinda nafasi mbalimbali za uchaguzi.

Mauaji hayo huacha shida kubwa kisaikolojia, kiuchumi, kihisi na kimaendeleo kwani si familia tu hata na umma kwa ujumla haziwezi kuwajua au kuwafahamu ni nani aliyewaua mpendwa wao wala sababu za mauaji hayo kadhalika wanaoachiwa kilio na msiba hawana wa kumwuliza.

Waganga hao huua bila sababu na hakuna anayefahamu chanzo, nia, wala wahusika japo kila mtu aliyekuwa akifuatilia vifo hivyo, anafahamu ama kuna alilolisikia kuhusu sababu za mauaji hayo.

Kwa ujumla wengi huyahusisha na mwenendo wa uchaguzi.

Kwa vile mahakama na polisi wanasikiliza na kupeleleza kesi hizo ili kutenda haki si vyema kuingilia uhuru wala mwenendo wa vyombo hivyo mahiri vya dola, lakini ni vyema na vyenyewe vikajua kuwa nyakati za uchaguzi kuna madai ya kuwatoa watu kafara.

Katika kukumbushana na kurejesha kumbukumbu za mambo yasiyopendeza yanayofanyika nyakati za uchaguzi wanasiasa wakumbuke kuwa hakuna hata mmoja, anayependa atendewe udhalimu na kunyimwa haki ya kuishi, hivyo ni vyema kujitazama.

Wakati umefika wa asasi za kiraia na wadau wengine kuwafundisha wananchi na wanasiasa umuhimu wa maisha hii ni kwa sababu Watanzania wengi huenda hawajui thamani ya maisha na huua wengine kama wadudu, jambo linalosikitisha.

Mathalani, mwanaume akihisi mkewe amejifungua mtoto ambaye ana wasiwasi siyo wake anamwua, tena kwa kumkata shingo au kumcharanga mapanga.

Watu wanawaua wenzao kwa 'hisia za ajabu au hata za kipuuzi', kwa mfano miaka kadhaa iliyopita watafiti wa ardhi kutoka Chuo cha Kilimo Seliana mkoani Arusha, walipigwa na kuchomwa moto huko Dodoma kwa madai eti ni wanyonya damu.

Huu ni unyama na uuaji watu kikatili hebu wauaji wa albino na watu wengine kama watoto waliokuwa wameuawa mkoani Iringa na watafiti wa Seliani wajitizame, pengine hawajakamatwa na polisi lakini wajigeuzie mkuki wakijihoji hivi kulikuwa na sababu ya kuwaua watu hao?

Tunapozungumzia siasa tukumbuke mauaji ya albino ambayo hadi leo yanazihuzunisha familia zao, lakini pia kuna mashambulizi dhidi yao.

Lazima ufike wakati Watanzania wathamini haki za wenzao na haki kuu ya msingi ya maisha kama ambayo inalindwa na katiba na sheria zote .

Kadhalika kupambana kwa dhati na wauaji wa albino, wale wanaowachinja wazee wanawake kwa wanaume kwa madai eti ni wachawi pamoja na watoto.

Aina hii ya mauaji hufanywa mikoa ya Kanda ya Ziwa na kuifanya Tanzania kunuka na kuchafuka kwa damu za watu wasio na hatia wanaochinjwa kwa madai ya kishirikina jambo ambalo dola linahitaji kuukomesha udhalimu huo hasa wakati wa uchaguzi.

Lakini pia katika kukomesha uuaji polisi na mahakama zishughulikie kesi za mauaji kwa kasi ili haki na ukweli upatikane.

Kuna usemi kuwa haki inayochelewa ni haki inayopotea. Sitaki nifike huko. Lakini pia ulinzi wa maisha ya kila mwananchi pia unahitajika hasa wakati huu wa uchaguzi na kudhibiti waganga wanaoibuka kiholela.

Hivi ni kweli watoto wadogo hawajui hatima zao, wazee wa mikoa ya Mwanza, Kigoma, Geita, Shinyanga, Tabora na Simiyu kadhalika nao wanafahamu kuwa iko siku wanaweza kucharangwa mapanga hasa wakati huu tunapozidi kuingia ndani ya mwaka wa uchaguzi?

Ni wazi kuwa awamu ya nne imefanya makubwa kudhibiti viongozi na matendo ya uasi hasa kujilimbikizia mali haramu ambayo yalitajirisha wachache na kuongeza umaskini kwa wengi na kuosababisha taifa kuwa na majambazi wakiwamo waganga wa kienyeji waliochochea mauaji mara kwa mara.

Hongera kwa serikali kwa kudhibiti tamaa za ufisadi na utajiri wa viongozi wa umma na washirika wao ambao uliwaacha wengi wakiwa maskini.

Baadhi ya maskini hao, walisukumwa kwenda kwa waganga wa kienyeji kupata mbinu za kutajirika ikiwa ni pamoja na kupitia uongozi wa kisiasa, wengine wakitakiwa kuua albino na kubaka mabinti, kuua wazee na hata wenye ulemavu wa akili.

Rushwa nayo kabla ya kudhibitiwa iliongeza uovu ndani ya jamii kwani wapo wahalifu ambao waliukwepa mkono wa dola kwa kutumia pesa walizonazo.

Jeuri ya pesa ndiyo iliyochochea mauji, ujangili na kuua wanyama, kuingiza na kuuza dawa za kulevya pamoja na uporaji wa ardhi, mali kwenye nyumba za watu na ukandamizaji wa wanyonge ili kupata pesa ikibidi kununua uongozi.

Jamii ambayo ina uchungu na huzuni kuwa ndugu zao waliuawa inakuwa na msukumo wa kulipiza kisasa ambacho kinaongeza hatua nyingine ya kuuana.

Hongera serikali kwa kuwashughulikia na kuwaadhibu kisheria wadhalimu hao ili kuondokana na kizazi cha walipa kisasa. Wakati mwingine jamaa za watu waliouawa wanaathirika kisaikolojia na kuamua kuua wengine kama dawa ya kutibu majeraha ya moyo yanayotokana na vifo vya ndugu zao waliouliwa.

Pengine wanaumia na kuamini kuwa jamii inalea uovu na kutukuza uhalifu ukiwamo uuaji ndiyo sababu ya kuchukua hatua hiyo.

# Haftar mbabe anayepasua vichwa viongozi AU na EU

**Na Mwandishi Wetu**

AKIWA na cheo cha 'Field Marshal' kamanda Khalifa Belqasim Haftar, mwenye uraia wa Libya na Amerika ni kiongozi wa Jeshi la Taifa la Libya (Libyan National Army), anayeongoza mapambano dhidi ya serikali ya Walibya iliyoko Tripol inayoungwa mkono na jumuiya ya kimataifa.

Haftar ana nguvu kubwa, ameyaweka chini ya uongozi wake majimbo tisa ambayo awali yalikuwa yamechaguliwa na wananchi na sasa yako chini ya utawala wa kijeshi anaouongoza na ilipofika Mei mwaka 2019 hadi sasa anatambuliwa kama kiongozi anayeiongoza nchi hiyo katika vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Kutokana na seke seke hilo, mwishoni mwa wiki iliyopita, jijini Berlin nchini Ujerumani, ulifanyika mkutano mkubwa wa upatanishi baina ya serikali inayotambuliwa kimataifa nchini Libya na mbabe wa kivita upande wa mashariki mwa nchi hiyo Kamanda Haftar.

Kikao hicho kufanyika nchini humo ni kudhihirisha kuwa kwa muda mrefu Ujerumani imekuwa ikihangaika kutaka kuchukua nafasi ya kuwajibika kimataifa. Mara nyingi haiko wazi, iwapo hilo si suala linalobishaniwa. Lakini suala kubwa hapo ni je, uwezo wa kijeshi ukoje? Lakini bila shaka, nguvu za Ujerumani zinaweza kusaidia kwa kuitazama hapo zamani pamoja na uwezo wake wa kidiplomasia.

Jumapili iliyopita Kansela Angela Merkel alikutana mjini Berlin na marais wa Ufaransa, Urusi, Uturuki na Misri. Pia mawaziri wakuu wa Uingereza na Italia. Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, pamoja na wawakilishi wa Umoja wa Falme za Kiarabu, Umoja wa Ulaya (EU) na Umoja wa Afrika AU.

Libya ambayo inapitia katika mzozo mkubwa, iliwakilishwa na pande zote zinazohusika katika vita hiyo huku kiongozi wa serikali inayotambulika kimataifa Faiz al-Farraj na mbabe wa kivita jenerali Khalifa Haftar ambaye anadhibiti sehemu kubwa ya ardhi ya nchi hiyo..

Lakini tukio la kuwapo katika mkutano huo viongozi wote wanaohusika katika mzozo huo, bila ya wao kukutana ana kwa ana linamaanisha kubwa kuhusiana na hali ya mzozo nchini Libya. Tangu pale alipoangushwa kutoka madarakani kiongozi wa muda mrefu wa Libya, Mouammar Gaddafi, mwaka 2011, nchi hiyo imajikuta katika vita vinavyoendelea, ambamo mataifa kadhaa ya nje yanahusika.

Hapa kuna masuala ya mafuta na gesi na wakimbizi, ambao wahalifu kutoka nchini Libya wanasaidia kuwasafirisha kupitia bahari ya Mediterania, ama kuwashikilia nchini Libya katika hali mbaya kabisa.

Na pia kuna suala la ugaidi wa makundi ya Kiislamu. Mchanganyiko wa vurumai lote hilo kwa muda mrefu haukuwa ukiangaliwa kama ilivyokuwa katika vita nchini Syria. Lakini vita vya mataifa mengine vinavyopiganwa nchini Libya, ni mzozo wa muda mrefu.



Kamanda Haftar anayedaiwa kusababisha mgogoro wa Libya kuathiri ukanda mzima wa Sahel. **PICHA MTANDAO.**

> Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, pamoja na wawakilishi wa Umoja wa Falme za Kiarabu, Umoja wa Ulaya (EU) na Umoja wa Afrika AU.

Serikali ya Ujerumani ilianzisha juhudi za kupambana na hali hiyo, na kuyaita mataifa yenye ushawishi na nguvu katika mkutano wa Berlin, kuweza kuzungumzia kwa uwazi, pamoja na utendaji, kuweza kuwaleta pamoja viongozi wanaopambana nchini Libya kwa ajili ya upatanishi, hususan kuzuwia mtandao wa kimataifa unaounga mkono vita, upelekaji wa silaha na kujinufaisha kiuchumi.

Bila ya usaidizi wa kimataifa, kila kitu kingesimama, si upande wa serikali inayoungwa mkono kimataifa ama mbabe wa kivita Haftar, kusingewezekana kuchukua hatua.

Kwa Ujerumani kujiingiza katika hatua za kidiplomasia ilikuwa sahihi. Katika nyakati hizi za siasa kali za kizalendo, mpango huo binafsi unatambulika na Umoja wa Mataifa kuwa ni suluhisho halisi la Libya. Sasa hatua ya kusitisha mapigano na jumuiya ya kimataifa kuangalia usitishaji huo vinaweza kupatikana pamoja na utimizaji wa masharti ya vikwazo vya silaha vya Umoja wa Mataifa.

Wakati hayo yakijiri jijini Berlini wiki iliyopita kabla ya mkutano huo, mataifa ya Afrika yameshinikiza kuwa na sauti zaidi katika mzozo wa Libya.

Nchi zinazopakana na Libya zinashinikiza kuwa na sauti zaidi katika juhudi za kukomesha mzozo katika taifa hilo jirani ambalo athari za mgogoro huo zinaibuka kuwa chanzo cha kutokuwa na uthabiti wa kisiasa, kiuchumi na amani katika kanda hiyo.

Hayo yanajiri wakati mataifa ya Bara la Ulaya, Uturuki na Urusi, yalishiriki katika kongamano la amani la Libya mjini Berlin zikiwa juhudi za kimataifa za kumaliza mapigano kati ya kamanda wa eneo la Mashariki ya Libya Khalifa Haftar na serikali inayotambuliwa na Umoja wa Mataifa mjini Tripoli.

Mwenyekiti wa Muungano wa Afrika Moussa Faki pia, alishiriki katika mazungumzo hayo ya Berlin na kutumaini kuleta mtazamo wa bara Afrika lakini halitakuwa jukumu rahisi.

Kwa mujibu wa msemaji wa Faki, Ebba Kalondo, aliyezungumza kabla ya mkutano huo, alisema mataifa jirani kama Chad, Sudan, Algeria, Tunisia, Misri na zaidi yanaathirika kutokana na athari hizo za kivita.

Kalondo anasema Muungano wa Afrika umekuwa ukitaka kuwa na jukumu zaidi katika harakati zinazoendelea lakini mara kwa mara umepuuzwa. Kwa muda mrefu, eneo la Sahel na mataifa ya Afrika yamekuwa yakiathirika kutokana na mzozo wa Libya.

Baada ya upande wa uasi uliungwa mkono na Jumuiya ya Kujihami ya Jeshi la NATO kumuondoa madarakani Muammar Gadafi, mwaka 2011, Libya imetumbukia katika mzozo wa makundi ya kijeshi kushindania mamlaka ya serikali.

Katika ghasia hizo, wanamgambo wa Kiislamu na wasafirishaji wa wahamiaji wamepanua ushawishi wao.

Pengo la usalama nchini Libya liliwezesha kusambaa kwa wapiganaji, silaha na vilipuzi katika mipaka yake na kuingia nchini Mali, Niger na Burkina Faso ambazo zinakabiliwa na ongezeko la ghasia za kijihadi licha ya kampeni ya kanda hiyo kukabiliana na wanamgambo hao wa Kiislamu.

Taifa hilo la Kaskazini mwa Afrika bado limesalia katika mizozo ambayo kwasasa ni kati ya vikosi vinavyoongozwa na Haftar katika eneo la Mashariki na serikali inayotambuliwa na Umoja wa Mataifa ya Tripoli. Vikosi vinavyoongozwa na Haftar vilishambulia mji mkuu wa nchi hiyo Aprili mwaka jana.

Desemba mwaka jana , Rais wa Niger Mahamadou Issoufou, alisema jamii ya kimataifa inahusika katika kile kinachoendelea katika eneo hilo kupitia maamuzi mabaya ya kuingilia Libya, akimaanisha kampeini ya NATO ya mwaka 2011.

Aliliambia shirika la habari la Ufaransa la AFP kwamba Libya iko Afrika na tatizo la Libya haliwezi kutatuliwa kwa kutenga Muungano wa Afrika, Rais wa Chad Idriss Deby, akaongeza kuwa kutatuliwa kwa mzozo wa eneo la Sahel kunahusika moja kwa moja katika kumaliza msukosuko nchini Libya.

Mwaka jana 2019, kundi la kijihadi liliwauwa watu 4,000 chini Burkina Faso, Mali na Niger licha ya kuwako kwa maelfu ya vikosi vya Ufaransa , ujumbe wa amani wa Umoja wa Mataifa nchini Mali na Muungano wa G5 wa Sahel miongoni mwa majeshi ya mataifa matano ya kanda hiyo.

Kwa mujibu wa mwanadiplomasia mmoja kutoka Ulaya, "Afrika inatafuta kusikilizwa zaidi hivi sasa huku hali ya usalama ikiendelea kudorora katika eneo la Sahel." Lakini Umoja wa Mataifa unaandaa mazungumzo hayo ya Berlin na kuchukua jukumu muhimu katika mazungumzo hayo.

Claudia Gazzini wa shirika la mizozo ya kimataifa, hali hii inasalia katika mikono ya Umoja wa Mataifa na chini ya uongozi wa Umoja wa Mataifa na hivyo inamaanisha kuwa Muungano wa Afrika umepuuzwa.

***Makala inatoka DW.***

UCHAMBUZI

# Salah: Wanawake tumeenguliwa



Mwanaharakati Salah akichagiza masuala ya mabadiliko ya kisiasa nchini Sudan. **PICHA MTANDAO.**

**Na Mashaka Mgeta**

PICHA ya Alaa Salah (23), akiwa amesimama juu ya gari amevaa baibui nyeupe, akiongoza umati wa waandamanaji waliokuwa wakipaza sauti zao kutaka kuondoka madarakani kwa aliyekuwa Rais wa Sudan, Omar al-Bashir.

Picha hiyo ilimuongezea umaarufu duniani kote kutokana na namna ilivyochagiza maandamano yaliyochangia kuondolewa madarakani kwa utawala wa miaka 30 ya al-Bashir. Aprili 11, mwaka jana, kiongozi aliachia ngazi.

Hali hiyo ilitafsiriwa pia kama kielelezo cha wajibu wa mwanamke kuwa mstari wa mbele kwa harakati na maandamano ya utetezi wa misingi ya demokrasia, ambapo mara nyingi wanawake wanakuwa wengi kuliko wanaume.

Lakini miezi sita baadaye, Salah anasema wanawake wametengwa wakati ambapo Sudan inahaha kuunda serikali ya kidemokrasia.

Msichana huyo mwenye umri wa miaka 23 na wanaharakati wengine wanaotetea haki za mwanamke, walikwenda Umoja wa Mataifa (UN) huko New York, Marekani mwishoni mwa mwaka jana, wakiomba msaada wa jumuiya ya kimataifa ili wanawake wapate uwakilishi kwenye serikali mpya ta nchini humo.

> Tunaona kila siku, kamati inayoundwa tena na tena, mara zote inakuwa na wanaume, jambo ambalo linatuchanganya akili.

"Wanawake waliongoza kamati za kupinga utawala wa al-Bashir, walipanga njia za maandamano na kutotii amri iliyowazuia watu kutoka nje ya makazi yao kuunga mkono maandamano, hata katikakati ya kutangazwa kwa hali ya hatari iliyowasababishia madhara kutoka kwa maofisa wa usalama..."

"Wanawake wengi walipigwa mabomu ya machozi, walitishwa, walitukanwa, waliwekwa jela pasipokuwa na mashitaka," Salah akaliambia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa wakati wa mkutano uliohusu wanawake, Amani na usalama.

Akaongeza, "Hata hivyo, mbali na uwajibikaji huo ulioonekana wazi, mbali na ujasiri na uongozi wao, wanawake wameachwa katika mchakato wa kawaida wa kisiasa kwa miezi kadhaa baada ya mapinduzi."

Kwa mujibu wa Salah, baada ya al-Bashir kuondolewa madarakani, Agosti mwaka jana, jeshi na viongozi wa vyama vya upinzani walijadiliana na kukubaliana kuhusu mgawanyo wa madaraka, lakini ni mwanamke mmoja pekee aliyeshiriki mazungumzo hayo.

Shirika la habari la Reuters liliripoti kuwa, wanawake wamepewa nafasi mbili kati ya sita zinazowawakilisha raia kwenye baraza la taifa lenye wajumbe 11, litakaloongoza Sudan mpaka uchaguzi utakapofanyika ndani ya kipindi cha miaka mitatu tangu kufanyika makubaliano hayo.

Wakati wa utawala wa al-Bashir, asilimia 25 ya viti kwenye bunge la nchi hiyo vilikuwa vya wanawake, lakini hapakuwa na mwanamke yeyote kwenye baraza la mawaziri.

Salah na wanaharakati wengine wanashinikiza ili kufikiwa kwa asilimia 50 ya wanawake katika uwakilishi kwenye serikali mpya ya Sudan.

Akizungumza na jarida la TIME kupitia kwa mkalimani, Salah anasema nia yake ni kuona serikali inawasikiliza wanawake ili kuwa na nchi inayotarajiwa na raia wote.

Salah, akiwa mwanafunzi anayesoma kuwa mhandisi msanifu, alikuwa 'kioo' cha mapinduzi wakati picha yake hiyo ilipoanza kusambaa hasa kupitia kwenye mitandao ya kijamii Aprili mwaka jana.

"Maisha yangu yamebadilika baada ya picha ile kusambaa" Salah anaiambia TIME na kuongeza, "vyovyote itakavyonibidi kuwatumikia watu wetu (Wasudan) nipo tayari kwa hilo."

Anaeleza kuwa ni dhahiri kwamba harakati za kutetea uwapo wa demokrasia nchini humo zitafanikiwa ikiwa wanawake watachukua nusu ya nafasi za uongozi wenye dhamana ya kufanya uamuzi serikalini, na pale mchakato wa kisiasa utakapowahusisha watu wa imani na kabila tofauti.

Wanawake walioteseka kwa ukandamizwaji katika miongo ya utawala wa al-Bashir, walikuwa mstari wa mbele kushiriki maandamano yaliyomuondoa kiongozi huyo madarakani.

"Serikali imekuwa kwa miaka 30, ikiwakandamiza wanawake kupitia sheria na sera za kibaguzi," mwanaharakati mwingine wa haki za wanawake nchini humo, Samah Jamous, anasema.

Jamous ni miongoni mwa wanawake kutoka Sudan walioshiriki mkutano wa UN, anayeiambia TIME kupitia kwa mkalimani kwamba, "imefikia hatua yake na njia pekee ni kusihi maisha tunayoyastahili kwa utawala wa al-Bashir kuondoka madakarani."

Maandamano nchini Sudan yalianza Desemba mwaka juzi, wakati raia wa Sudan walipoingia mitaani wakilalamikia hali ngumu ya kiuchumi, ikiwemo ongezeko la bei ya mikate, upungufu wa chakula na mafuta na ukomo wa kuchukua fedha benki.

Jeshi lilichukua madaraka na hivyo kuibua shangwe ya ushindi kwa waandamanaji.

Hata hivyo, maandamano hayo yaliendelea kwa madai kuwa majenerali wa jeshi walioshika madaraka ya nchi kwa muda na kutaka kuwepo utawala wa kiraia.

"Kwa kuzingatia hukumu la wanawake katika kufanya kazi kwa ajili ya Amani na maendeleo, kutetea haki za binadamu na kutoa msaada wa kibinadamu unapohitajika, hakuna sababu ya kutokujumuisha (wanawake) kwa usawa katika nafasi zote," Salah anasema alipozungumza UN.

"Baada ya mapambano ya miongo kadhaa na namna tulivyojitoa kukomesha utawala wa kidikteta wa al- Bashir, kukosekana kwa usawa wa kijinsia hauwezi na hautakubalika kwa wanawake na wasichana wa Sudan," anasema.

Kwa suala la kuwapo usawa wa kijinsia, mtandao wa wanawake na makundi ya kisiasa nchini Sudan, yanafanya utetezi wa sheria zinazolinda haki za mwanamke na msichana, na kutaka watu walioshiriki vitendo vya unyanysaji wa kijinsia, ubakaji na ulawiti wakati na baada ya utawala wa al-Bashir, wawajibishwe.

"Tunaona kila siku, kamati inayoundwa tena na tena, mara zote inakuwa na wanaume, jambo ambalo linatuchanganya akili," Jamous anasema. Anaongeza, "mbali na tunayoyasema, linapokuja suala la utekelezaji, wanarudi nyuma kwa dhana inayofanana kutomuona mwanamke - ama kutowaona (wanawake) kama wasiofaa kuwa kwenye nafasi hizo."

Harakati zilizofanyika nchini Sudan ni moja ya maandamano mengi yaliyotokea mwaka juzi na jana kwenye mataifa tofauti duniani.

"Kila mapinduzi yanayotokea yanatamanisha kufanyika mapinduzi mengine," Salah anasema.

***Makala haya yamendikwa kwa msaada wa vyanzo tofauti - 0754691540***



HABARI MBEYA

# Wachimbaji wapiga jeki ujenzi wa gereza

**Na Nebart Msokwa, CHUNYA**

CHAMA cha Wachimba Madini Mkoa wa Mbeya (Mberema), kimeikabidhi serikali msaada wa vifaa mbalimbali kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Gereza la Wilaya ya Chunya linalojengwa katika Kata ya Mbugani.

Msaada huo ambao unagharimu zaidi ya Sh. 600,000 ulikabidhiwa na chama hicho kwa Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mhandisi Maryprisca Mahundi ambaye ndiye aliyeomba.

Akikabidhi msaada huo, Mwenyekiti wa Chama hicho, Leonard Manyesha, alisema vifaa walivyonunua ni mifuko 20 ya saruji na mabati bando moja na kwamba wachimbaji walichanga kutokana na kuguswa na ombi na Mkuu wa Wilaya hiyo.

Alisema wataendelea kuchanga vitu vingine ili kuhakikisha gereza hilo linafunguliwa na linaanza kufanya mapema kama serikali inavyokusudia pamoja na kuwasogezea huduma wananchi wa wilaya hiyo ambao wanalazimika kupelekwa katika Gereza la Ruanda lililopo jijini Mbeya.

"Mkuu wa wilaya alituomba tusaidie ujenzi huu alipotembelea na kubaini kuwa jiko bado lilikuwa halijakamilika kutokana na uhaba wa vifaa, hili gereza ni muhimu kwa sababu mahabusi wanalazimika kupelekwa Mbeya Mjini," alisema Manyesha.

Diwani wa Makongolosi, Sailon Mbalavata ambaye ni mwanachama wa chama hicho cha wachimbaji, alisema gereza hilo litasaidia Wilaya ya Chunya ndio wilaya pekee katika Mkoa wa Mbeya ambayo ilikuwa haina gereza.

Alisema kwa sasa wananchi wanafurahia kutokana na kusogezwa kwa huduma hiyo kwa maelezo kuwa walikuwa wanatumia gharama kubwa kwenda kuwaona ndugu zao jijini Mbeya ambao wapo mahabusu.

Akipokea vifaa hivyo Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, aliwashukuru wadau hao kwa mchango waliotoa kwenye mradi huo kwa madai kuwa wangeamua kuisubiri Serikali, wangechelewa zaidi kukamilisha.

Alisema baada ya kutembelea gereza hilo na kubaini tatizo la kukosekana kwa jiko katika gereza hilo aliamua kuwashirikisha wadau mbalimbali na kwamba miongoni mwa wadau wa kwanza kushiriki ni wachimbaji.

"Hili gereza letu ni jipya kwa hiyo inahitajika miundombinu mingi, sasa tukisubiri serikali ijenge yote tutachukua muda mrefu sana, kwa hiyo tunatakiwa sehemu zingine tujiongeze wenyewe, nawashukuru sana wachimbaji kwa kujitoa," alisema Mahundi.

Pia aliahidi kutoa viatu jozi 22 kwa ajili ya wafungwa ili wafanye kazi zao za kurekebishwa tabia wakiwa salama.

# Wizara kuvunja kanda zote za makamishna wa ardhi

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inakusudia kuanzisha mfumo mpya wa usimamizi wa ardhi kwa kuvunja kanda zote nane za makamishna wa ardhi nchini.

Badala yake utaanzisha usimamizi mpya kwa kupeleka kamishna wa ardhi katika kila mkoa kuanzia mwezi ujao, kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, aliyasema hayo jana jijini Mbeya wakati akifungua mafunzo ya siku mbili ya mfumo wa ukusanyaji kodi ya ardhi ambayo yanawashirikisha maofisa ardhi na mipango miji kutoka mikoa saba ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

"Kuanzia mwezi ujao tunaanza kutangaza ni kinanani wanakwenda kuanzisha mikoa, hizi kanda nane tunazifuta, kwa hiyo tutakuwa wawakilishi wa kila mkoa, na tunaanzisha rasmi Ofisi ya Ardhi ya Mkoa na ndani ya ofisi hiyo kutakuwa na mtu anayeratibu mambo ya mipango miji," alisema Lukuvi.

Alisema kuwa kila halmashauri inayohitaji kufanya mabadiliko ya mipango miji, itaishia katika ngazi ya mkoa na haitatakiwa kwenda katika ngazi ya kanda kama iliyo hivi sasa.

Lukuvi alisema kuwa lengo la serikali kuchukua uamuzi huo ni kusogeza huduma kwa wananchi kwa kuwa imebaini kuwa suala la umbali limekuwa ni kikwazo kikubwa cha wananchi kupata hati zao za umiliki wa ardhi.

Alisema mpaka sasa kuna mrundikano mkubwa wa hati za umiliki wa ardhi kwenye ofisi za makamishna wa ardhi wa kanda ambazo hazijachukuliwa na wananchi na baada ya uchunguzi imebainika kuwa walioshinda kufika kuzichukua wanaishi mbali na ofisi hizo.

"Mpaka hivi sasa ninavyozungumza kuna hati miliki za ardhi zaidi ya milioni 20 kwenye ofisi zetu za Makamishna wa Ardhi nchi nzima hazijachukuliwa, tumebaini hii inatokana na umbali maana mwananchi aliyepimiwa ardhi yake kule Halmashauri ya Mpimbwe mkoani Katavi anapaswa kwenda kuchukua hati yake kwenye ofisi ya Kamishna wa Ardhi wa Kanda mjini Tabora, inawezeka kabisa akawa hana fedha ya kumfikisha Tabora na ndio sababu tunahitaji sasa huduma hizi azipate kwenye mkoa wake," alisema Lukuvi.

Akifafanua zaidi alisema kuwa ndani ya Ofisi ya Ardhi ya Mkoa kunakuwa na kila kitu kinachohitajika kwa ajili ya upimaji na umilikishaji wa ardhi kwa wananchi, hivyo hata hati ya umiliki wa ardhi itatolewa katika ngazi ya mkoa.

Alisema kwa vile nchi inakoelekea itakuwa na mfumo mpya wa utoaji wa hati za umiliki wa ardhi kwa njia ya kielektroniki, hata saini ya Kamishna Mkuu wa Ardhi itakuwapo kwenye mfumo, hivyo hati zote zitakazotolewa katika ngazi ya mkoa zitakuwa zimesainiwa na Kamishna Mkuu wa Ardhi.

"Katika ofisi hizi za ardhi za mkoa hakuna kitu kitakachokuwa nje ya uwezo wenu, mtafanya kila kitu na kazi ya wizara itabaki kuratibu tu mfumo kuhakikisha kila kitu kinakwenda vizuri," alisisitiza Lukuvi.

Mthamini Mkuu wa Serikali kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Evaline Mugasha, alisema lengo la serikali ni kuwa na mfumo mmoja wa kukusanya kodi ya ardhi nchi nzima.

Alisema mfumo huo utawashirikisha wadau wote wa ardhi, kuanzia wachora ramani, wapimaji mpaka kwa watoaji wa hati miliki ili kuhakikisha hakuna kipande cha ardhi nchini ambacho hakitakuwa kinalipiwa kodi.



Mafundi wa kampuni ya Kichina inayojenga kipande cha barabara ya Mbeya– Tabora, kuanzia Chunya mjini hadi Mji wa Makongolosi chenye urefu wa kilomita 39, kwa kiwango cha lami, wakiendelea kusuka daraja la Mto Lupa, lenye urefu wa zaidi ya mita 30, juzi.
**PICHA: NEBART MSOKWA**

# Vijana lawamani kutorejesha mikopo

**Na Nebart Msokwa, KYELA**

VIKUNDI vya vijana mkoani Mbeya, vinadaiwa kuwa ndivyo vinaongoza kwa kutorejesha fedha za mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri kwa ajili ya kuwezesha makundi maalumu kuendesha shughuli zao za ujasiriamali.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, wakati Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa ilipofanya ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo wilayani Kyela ikiwa ni pamoja na vikundi vya wajasiriamali.

Alisema vijana wanaojitokeza kuomba mikopo hiyo ni wachache, lakini hata hao wanaojitokeza nao wamekuwa wagumu kurejesha mikopo hiyo kwa wakati ikilinganishwa na makundi mengine.

Alisema vikundi vinavyoongoza kwa uaminifu kwenye mikopo hiyo ni vya wanawake vikifuatiwa na vya watu wenye ulemavu ambavyo pia ndivyo vinaoongoza kwa kuchangamkia mikopo hiyo.

"Baada ya kuona tatizo hili ni kubwa la vijana kutorejesha mikopo ndio maana tukabadili mfumo wa ukopeshaji, badala ya kukopesha fedha sasa hivi tunakopesha vitu, lakini kwa vikundi vya wanawake tuna ujasiri hata wa kuvikopesha fedha," alisema Chalamila.

Vilevile alisema vijana wamekuwa wazito kujiunga kwenye vikundi ili wawe na sifa za kupata mikopo hiyo kwa maelezo kuwa wamekuwa wakisingizia kuwa kila mmoja ana shughuli yake ya kumwingizia kipato tofauti na mwingine.

Alisema awali Halmashauri za Mkoa huo zilikuwa hazina mfumo mzuri wa kutenga asilimia 10 ya mapato kwa ajili ya mikopo hiyo kutoka kwenye mapato ya ndani kwa maelezo kuwa zilikuwa hazitengi kila mwezi.

Alisema kwa sasa kila halmashauri inatenga fedha hizo na kuzihifadhi kwenye akaunti maalumu na muda ukifika vikundi vinavyostahili vinakopeshwa.

Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Solomon Itunda, aliwashauri vijana kuchangamkia fursa hiyo kwa kujiunga kwenye vikundi ili wakopeshwe fedha hizo na wakuze shughuli zao na kwamba ikiwezekana kila kata iwe na vikundi vya wajasiriamali.

Alisema serikali iliamua kuweka utaratibu huo wa kuyakopesha makundi hayo maalumu kutokana na umuhimu wake katika uzalishaji mali na kwamba kitendo cha vijana kukosa uaminifu kinakatisha tamaa.

Itunda alisisitiza kuwa wananchi wa Mkoa wa Mbeya wana mwitikio mkubwa wa kulipa kodi mbalimbali na hivyo halmashauri zina fedha nyingi ambazo zinahitajika kwa ajili ya kuvikopesha vikundi hivyo.

"Tuliwaahidi wananchi wakati tunaiuza Ilani ya Chama chetu mwaka 2015 kuwa tutatoa mikopo na Watanzania wakatuamini, sasa tumekuja kwa ajili ya kuangalia kama hiyo mikopo inatolewa, imeonekana wanawake wanakopa sana kwa sababu pia ni waaminifu," alisema Itunda.





# LAAC yatia neno majengo Chamwino

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), imeshauri Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuchukua majengo yaliyokuwa yakitumiwa na halmashauri ya Chamwino kuwa sehemu ya Kituo cha Afya cha Makole.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Abdallah Chikota, alitoa ushauri huo jana wakati wajumbe wa kamati hiyo walipotembelea miradi kadhaa inayotekelezwa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Miradi hiyo ni pamoja na Kituo cha Afya Makole, kituo cha kisasa cha mabasi yaendayo mikoani na Soko Kuu la Ndugai.

Chikota alisema kituo hicho kina ufinyu wa eneo, hivyo ni vyema wakaangalia namna ya kuchukua majengo hayo.

"Kwanini msiangalie uwezekano wa kuyachukua majengo yaliyokuwa yakitumiwa na Chamwino na hiyo Shule ya Sekondari ya Viwandani ikahamishwa ili majengo na eneo hilo litumike kituo cha Afya?" alihoji.

Kutonana na ushauri huo, Katibu Tawala wa Mikoa wa Dodoma, Kessy Maduka, alisema uongozi wa mkoa umepokea wazo hilo na utaliangalia kama linawezekana.

Awali, Mganga Mfawidhi wa Kituo hicho, Dk. George Matiko, alisema serikali ilitoa Sh. milioni 572 kwa ajili ya kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto.

Dk. Matiko alisema huduma zimeimarika na kwa sasa na huduma ya upasuaji kwa wajawazito zimekuwa zikifanyika kwa mafanikio.

"Tumepunguza vifo vya mama na mtoto baada ya kujenga jengo ambalo lina vigezo vinavyotakiwa kimataifa,"alisema.

Kwa upande wa mradi wa soko na kituo cha mabasi, Mhandisi Mshauri Emmanuel Malimbo alisema ujenzi wa soko umefikia asilimia 87 na mkandarasi ameshalipwa asilimia 64 ya gharama za ujenzi huku ule wa kituo cha mabasi ukifikia asilimia 85.

Naye Harish Jethwa kutoka Kampuni ya ujenzi ya Mohammed Builders, aliwahakikisha wabunge kuwa watakamilisha ujenzi huo katika muda uliopangwa ambao ni Februari 15, mwaka huu.

**"Tumepunguza vifo vya mama na mtoto baada ya kujenga jengo ambalo lina vigezo vinavyotakiwa kimataifa," alisema.**

# Askofu atoa somo uchaguzi 2020

**Na Peter Mkwavila DODOMA**

ASKOFU wa Kanisa la Evangelist Asembbless of God (EAGT) Jimbo la Kusini, Robert Mangwela, amewataka wananchi kutowachagua wanasiasa wanaotafuta madaraka kwa nguvu kwa maslahi yao katika uchaguzi mkuu unaofanyika mwaka huu.

Aidha, amewataka wanasiasa kuacha tabia ya kukimbilia kwa waganga wa kienyeji ili kupata nafasi za uongozi badala yake wamwombe Mungu awapatie fursa hiyo ya kuongoza.

Mangwela alisema hayo Jumapili iliyopita katika ibada maalum ya kuwasimika viongozi wa Kanisa la New Jerusalem EAGT, Ihumwa jijini Dodoma.

Alisema katika uchaguzi huo, wananchi wasichague wanasiasa watakaosababisha kutoweka kwa amani kwa sababu ya maslahi binafsi.

Askofu huyo alisema viongozi ambao wanaotakiwa kuchaguliwa ni wale wenye sifa ya kuongoza watu kwa upendo, amani na ushirikiano na si kwa kutafuta madaraka au kuongoza kwa mabavu, dharau, ubinafsi na uonevu.

"Kiongozi anatakiwa kuwa kioo cha jamii na kujenga utamaduni wa kutatua matatizo ya watu ambao wanakabiliana nayo na si kuibua migogoro," alisema.

Kiongozi huyo alisema kuwa taifa la Tanzania haliwezi kuwa na viongozi wanaoingia madarakani kwa ujanja ujanja na kwa kufanya fitina na kwamba watu wa namna hiyo hawawezi kuwa viongozi bora.

Kadhalika, alisema taifa haliwezi kusonga mbele kama litaongozwa na viongozi waliopatikana kutokana na nguvu ya waganga wa kienyeji na iwapo watapatikana, wataongoza kwa maelekezo ya waganga wao.

Alisema kiongozi bora anapatikana kutoka kwa Mungu na atakuwa mwenye hofu ya Mungu.



Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, akizungumza na wauzaji na wachinjaji wa kuku katika soko la Mwembe Tayari, wakati akihamasisha suala la usafi sokoni hapo, jijini humo jana. PICHA: PETER MKWAVILA

# Maelfu wajiunga vifurushi vya NHIF

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umekusanya zaidi ya Sh. bilioni nne kutokana na michango ya wanachama 4,976 waliojiunga kupitia vifurushi vipya vya mfuko huo.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alisema hayo jana alipokuwa akijibu hoja mbalimbali za wabunge kuhusu vifurushi hivyo kwenye Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Alisema hadi Desemba, mwaka jana, wanachama 3,343 walikuwa wamejiunga na hadi sasa wamefikia 4,976.

"Michango yake kwa Desemba ilikuwa Sh. bilioni 3.4 lakini kwa Januari peke yake tumepata Sh. milioni 668, hivyo kuwa zaidi ya Sh. bilioni nne," alisema.

Awali, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za mfuko, Konga alisema asilimia 60 ya wanachama walijiunga kwenye vifurushi vya 'Wekeza Afya' na 'Timiza Afya' huku asilimia 40 wakijiunga na kifurushi cha 'Najali Afya'.

"Hadi sasa tumefanya kampeni ya uhamasishaji ngazi ya mikoa kwenye mikoa 10 lengo ni kuhakikisha kampeni za uhamasishaji zinafanyika katika mikoa mingine iliyobaki kabla ya Juni, mwaka huu," alisema.

Alitaja mbinu zinazotumika kuwa ni kutoa elimu ya kuwafikia wananchi waliopo kwa njia mbalimbali ikiwamo minada, masoko na mikusanyiko mingine.

Hata hivyo, alisema ili kutoa unafuu kwa wananchi katika vifurushi hivyo kwa kushirikiana na wadau wengine wanakamilisha utaratibu wa wananchi kuchangia kwa awamu kwa utaratibu utakaojulikana kama 'Dunduliza' ili wananchi wengi wanufaike.

Sambamba na hilo, alisema mfuko umeongeza wigo wa wananchi kujiunga kupitia makundi kama vile wamachinga, bodaboda, madereva, baba na mamalishe, wakulima, wanafunzi wa vyuo na watoto chini ya miaka 18.

Mkurugenzi huyo alisema kuna kasi ndogo ya wananchi kujiunga hivyo, Wizara ya Afya na wadau wanaendelea na maandalizi ya Muswada wa kutunga sheria ya bima ya afya kwa wote itakayoweka ulazima wa wananchi kuwa na bima.


"Tumejipanga kabla na baada ya kutungwa kwa sheria, Mfuko umeandaa mkakati madhubuti wa masoko na elimu kwa umma ili kuhakikisha wananchi walio wengi wananufaika na bima,"alisema

Naye, Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko huo, Spika Mstaafu Anne Makinda, alisema utaratibu wa dunduliza utasaidia wananchi wasio na uwezo wa kulipa kwa mkupuo.

Akihitimisha kikao hicho, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Peter Serukamba, alisema wabunge wanawajibu wa kuhamasisha wananchi kujiunga wakati maandalizi ya sheria yakiendelea.

"Niwaombe sana wanasiasa tuhamasishe wananchi wetu, kama harusi tunachanga tunashindwaje kuelimisha wananchi wajiunge," alisema.

HABARI ZANZIBAR



# Waziri Viwanda ataja siri ushindani bidhaa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, amesema ushindani wa bidhaa nchini unahitaji mpangilio maalum unaotokana na sera, sheria pamoja na soko la uuzwaji wa bidhaa hizo.

Aliyasema hayo hivi karibuni wakati akifungua mkutano wa wajasiriamali kuhusu mpango wa kuhimili ushindani wa kibiashara nchini uliofanyika mjini Zanzibar.

Alisema ushindani wa biashara unahitaji mpangilio kwa kutoa mafunzo ya uzalishaji wa bidhaa kwa wajasiriamali, ili kuweza kufuata maadili ya wataalamu kwa kukuza uzalishaji na kuongeza kipato kwa wafanyabiashara wadogo.

Amina alisema kuwa wajasiriamali wa bidhaa ya mwani wameweza kupatiwa mafunzo ya mwani wa aina mpya, ambayo unauwezo wa kutoa mbegu ya mwani kwa wingi na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa hiyo.

Aidha, alisema wajasiriamali waliopata mafunzo kwa upande wa Pemba ni katika Kijiji cha Makangale, Tumbe, Chokocho pamoja na Kusini, Kaskazini na Magharibi kwa upande wa Unguja.

Alieleza kuwa changamoto zilizopo kwa wasiriamali hao ni ukosefu wa baadhi ya vifaa vya kufanyia kazi pamoja na boti ya uokozi pia wanahitaji mafunzo ya uokoaji na kuogelea.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeshatiliana saini mkataba katika kampuni mbili tofauti pamoja na utayarishaji wa ujenzi wa kiwanda cha mwani.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti ya Kupunguza Umaskini (Repoa), Dk. Donald Mmari, alisema wamekuwa wakishughulikia sera ya masoko ya ndani na ya nje ya bidhaa mbalimbali, ikiwamo bidhaa za mboga ngozi pamoja na zao la mpunga kwa lengo la kuimarisha bidhaa hizo ili ziweze kuingia katika ushindani wa kibiashara.

Alieleza kwa upande wa bidhaa ya mwani huwasaidia kipato kwa wakulima wa mwani kutokana na kukua kwa uzalishaji wa bidhaa hiyo na kuweza kumiliki soko la ushindani.

Alisema sera ya viwanda ina lengo la kukuza uzalishaji wa bidhaa kwa kukidhi mahitaji ya masoko pamoja na kuweza kuingia katika soko la ushindani.



Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Kiuyu Micheweni Pemba, wakiwa katika foleni wakisubiri kupatiwa huduma ya kuhakiki taarifa zao na wengine kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura jana. **PICHA: BAKAR MUSSA**

# ZEC yaanza kuboresha daftari la wapigakura

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAKAMU Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), Mabrouk Jabu, amesema wananchi wote wenye sifa wataandikishwa katika daftari la kudumu la wapigakura wakiwamo ambao hawajapata vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi.

Jabu alisema hayo huko Micheweni Wilaya ya Kaskazini wakati akizungumza na wananchi waliofika kujiandikisha.

Alisema wanafahamu kwamba wapo baadhi ya watu bado hawajapata vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi, hivyo hawawezi kuandikishwa katika daftari la kudumu la wapigakura.

''Zipo kasoro zimejitokeza kwa baadhi ya watu kushindwa kuandikishwa katika daftari la kudumu la wapigakura...tutahakikisha hakuna mtu anayeachwa na kushindwa kuandikishwa katika daftari hilo," alisema.

Aidha, aliwaomba wanasiasa kuwahamasisha wafuasi wao kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura ili kupata haki ya kuchagua viongozi wao.

Naye Mkurugenzi wa ZEC, Thabit Idarous, aliwataka wanasiasa kuacha kutoa vitisho na kujenga mazingira ya jazba za kisiasa ambazo zinaweza kusababisha joto la kisiasa.

''Zoezi la uandikishaji wa daftari la kudumu la wapigakura halitaki jazba za kisiasa...waacheni wananchi wajitokeze kujiandikisha," alisema.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Micheweni Pemba, Salama Mbarouk Khatib, alisema wamejipanga kuimarisha ulinzi katika mkoa wa Kaskazini ambao unaendelea na zoezi la daftari la kudumu la wapigakura.

Alisema hakuna sababu za kufanya vurugu na matukio ambayo yanaweza kuhatarisha amani na utulivu katika kipindi hicho ambapo zoezi la uandikishaji wa daftari la kudumu la wapigakura likiendelea.

Alieleza kuwa zoezi la uandikishaji wa daftari la kudumu la wapigakura ni moja ya fursa na haki ya msingi ambayo itawawezesha wananchi kupiga kura katika uchaguzi mkuu ujao.

## CCM yaanza maandalizi ushindi 2020

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Kaskazini Unguja, Iddi Ame Haji, amewataka viongozi wa kamati za siasa ya mkoa kuhakikisha kwenye uchaguzi mkuu ujao hakuna jimbo litakalochukuliwa na upinzani.

Akizungumza na wananchi wa Jimbo la Mkwajuni Shingwi baada ya kufungua tawi la chama ambalo limejengwa na Mwakilishi wa Jimbo hilo, Ussi Yahya, kwa gharama za Sh. milioni 12, alisema chama hicho kimejipanga kikamilifu.

Alisema ni aibu kwa viongozi wa mkoa wa Kaskazini Unguja kupoteza majimbo ya uchaguzi na kuchukuliwa na wapinzani.

Alisema katika uchaguzi wa mwaka 2015, baadhi ya majimbo ya mkoa huo yalichukuliwa na wapinzani ikiwamo Jimbo la Nungwi, Kijini na Bumbwini.

''Sitokubali kuona Mkoa wa Kaskazini Unguja unapoteza majimbo ya uchaguzi na kuchukuliwa na wapinzani," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Jimbo la Mkwajuni, Khamis Nyange Ussi, alisema ushindi wa CCM hauna mjadala katika uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano kazi iliyofanyika ni kuimarisha chama kupitia jumuiya zake, huku matawi ya kisasa ya chama yenye hadhi yakijengwa.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Ussi Yahya, alisema ataendelea kutekeleza ahadi ya ilani ya uchaguzi ya chama kwa wapigakura wa jimbo hilo ikiwamo usambazaji wa majisafi na salama.

Alisema alipoingia madarakani katika kipindi cha miaka minne moja ya kilio kikubwa cha wananchi ni tatizo la majisafi na salama.

Alisema tatizo hilo amelipatia ufumbuzi kwa kusambaza maji katika shehia zote za jimbo hilo, hivyo kupunguza usumbufu uliokuwa ukiwakabili wanawake.

**Kwa upande wake Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Ussi Yahya, alisema ataendelea kutekeleza ahadi ya ilani ya uchaguzi ya chama kwa wapigakura wa jimbo hilo ikiwamo usambazaji wa majisafi na salama.**

# Kampuni 10 za kununua pamba zaingia matatani

**Na Happy Severine, SIMIYU**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Simiyu, imeanza kazi ya kuchunguza kampuni 10 kati ya 22 ambazo zilikuwa zikinunua pamba katika mkoa huo, kutokana na kushindwa kulipa madeni ya wakulima mpaka sasa.

Taasisi hiyo imesema kuwa kampuni hizo zinadaiwa kiasi cha Sh. bilioni 4.5 na wakulima ambapo licha ya kupewa maagizo na viongozi wa kitaifa na mkoa kuhakikisha wanalipa madeni hayo hadi Desemba 31, 2019, lakini wameshindwa.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Takukuru Mkoa, Joshua Msuya, wakati akiongea na waandishi wa habari ofisini kwake Mjini Bariadi, kwenye mkutano wa kutoa taarifa ya robo ya pili Oktoba-Desemba, 2019.

Msuya alisema kuwa wameamua kuchunguza kampuni hizo kutaka kujua ni kwa nini wameshindwa kulipa madeni hayo ya wakulima, ikiwamo kushindwa kutekeleza maagizo ya viongozi.

Kamanda huyo wa Takukuru alisema kuwa kumekuwapo na mkanganyiko wa taarifa za malipo kati ya kampuni hizo na vyama vya msingi vya ushirika (Amcos).

"Kwenye uchunguzi wa awali Amcos zimeleta malalamiko kwetu na kutaja kampuni wanazodai, lakini tuliziita hizo kampuni kuwahoji kwa nini wanadaiwa, wao walisema tayari wamelipa madeni yao na hawadaiwi," alisema Msuya.

Aliongeza kuwa kutokana na mkanganyiko huo, taasisi hiyo imeamua kufanya uchunguzi wa kina kutaka kujua uhalisi wa malipo hayo ambayo bado wakulima wameendelea kudai.

Katika hatua nyingine, Kamanda huyo alisema katika kipindi hicho wamepokea malalamiko 68, ambapo kati ya hayo baadhi yanatoka kwa wakulima wa pamba kutolipwa pesa zao mpaka sasa.

Pia Msuya alisema taasisi hiyo imechunguza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya elimu yenye thamani ya Sh. 100,000,000 ikiwamo na miradi ya maji yenye thamani ya Sh. bilioni 1.2.

Alisema katika uchunguzi huo wamebaini kuwa miradi yote ya elimu na maji inachelewa kukamilika kinyume na mikataba, kutokana na fedha za malipo kuchelewa kutoka hazina na uwezo mdogo wa makandarasi.



Waumini wa Kiislamu wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Kaimu Katibu wa Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Mkoa wa Dodoma, Twaha Mwaya, aliyefariki dunia Jumapili, wakielekea katika maziko kwenye makaburi ya Oyster Bay Maili Mbili, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Wakulima 12,000 kushiriki maonyesho

**Na Faustine Feliciane, MOSHI**

ZAIDI ya wakulima 12,000 kutoka Tanzania na nchi jirani wanatarajiwa kushiriki maonyesho ya kilimo yanayofanyika leo kwenye Uwanja wa Ushirika mjini hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa mafunzo ya kilimo hai yaliyofanyika kwenye kituo cha mafunzo ya Kilimo Hai, wilayani Mwanga, mshauri wa mawasiliano wa Taasisi ya Kilimo Hai Tanzania (TOAM), Costantine Akitanda, alisema maonyesho hayo ya kila mwaka yatazinduliwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe.

"Tunatarajia kuwaona wakulima kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania wakishiriki katika maonyesho haya muhimu, lakini kutakuwa na washiriki wengine kutoka nchi za jirani pamoja na watu kutoka Ulaya ambao watakuja kushuhudia," alisema Akitanda.

Alisema kuwa maonyesho hayo yatakuwa fursa kwa wakulima kufanya biashara na pia kujifunza masuala mbalimbali ya kilimo hai.

"Kutakuwa na wataalamu wa kilimo hai, lakini wakulima wenyewe watapata fursa ya kubadilishana ujuzi na uzoefu," aliongezea Akitanda.

Maonyesho hayo yanafanyika leo huku yakitanguliwa na mafunzo juu ya kilimo hai kwa waandishi wa habari.

Mafunzo hayo kwa pamoja yamewezeshwa na Ubalozi wa Ufaransa nchini na SwissAid Tanzania kupitia kwa TOAM.

---

**"Tunatarajia kuwaona wakulima kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania wakishiriki katika maonyesho haya muhimu, lakini kutakuwa na washiriki wengine kutoka nchi za jirani pamoja na watu kutoka Ulaya ambao watakuja kushuhudia," alisema Akitanda.**

# Bunge lafagilia utendaji Wizara ya Madini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeipongeza Wizara ya Madini kutokana na mafanikio kadhaa yaliyojitokeza katika sekta ya madini ikiwamo ukuaji, ukusanyaji wa maduhuli, huku ikishauri kuendelea kuisimamia.

Kamati hiyo imesema kwamba mafanikio hayo yamepatikana kutokana na matumizi mfumo wa kisasa.

Pongezi hizo zinafuatia taarifa mbalimbali za utekelezaji wa shughuli na miradi iliyotekelezwa na wizara na taasisi zake kwa kipindi cha nusu mwaka kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ambazo zimewasilishwa kwa kamati hiyo.

Kamati ya Bunge imeeleza kuwa sekta ya madini imepiga hatua, huku ikitoa pongezi kwa Rais John Magufuli na kueleza kuwa sababu za kuitenganisha iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini na kuanzishwa kwa Tume ya Madini zinaonekana.

Aidha, kamati hiyo imetoa ushauri kwa wizara na kuitaka kuendelea kuisimamia sekta ya madini kwa lengo la kuhakikisha kwamba sekta hiyo inazidi kuchangia zaidi katika pato la taifa, ukuaji wa uchumi na maendeleo ya taifa.

Awali, akitoa taarifa kwa kamati kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa majukumu ya wizara, Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Madini, Augustine Ollal, ameieleza Kamati ya Bunge kuwa kwa kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2019, sekta ya madini ilishika nafasi ya pili kwa kasi ya ukuaji wa asilimia 13.7 ukichangiwa zaidi na ongezeko la uzalishaji wa madini ya dhahabu na makaa ya mawe.

Ameongeza kuwa hadi kufikia Desemba 31, 2019, wizara kupitia Tume ya Madini ilikusanya maduhuli ya kiasi cha Sh. 242,531,173,458.83 sawa na asilimia 103 ya lengo la nusu mwaka na asilimia 51.5 ya lengo la makusanyo ya mwaka mzima.

Akizungumzia mauzo ya madini ya dhahabu kwenye masoko ya madini ameeleza kuwa, kwa kipindi cha Julai hadi Novemba 2019, kiasi cha dhahabu kilichozalishwa katika masoko ya Geita, Chunya, Kahama, Mwanza na Mara kimeongezeka hadi kufikia kilo 5,546.6 ikilinganishwa na kiasi cha kilo 1,188.4 kipindi cha nyuma kabla ya kuendeshwa kwa kaguzi za kimkakati katika maeneo hayo.

"Mheshimiwa mwenyekiti, wizara ilikusudia kuanzisha masoko ya madini katika mikoa yote nchini, hadi kufikia mwezi Desemba, 2019 jumla ya masoko 28 na vituo vya ununuzi wa madini 25 yalikuwa yameanzishwa nchini," alisema Ollal.

Pia alieleza kuwa, baada ya wizara kufanya kaguzi za kimkakati za leseni za biashara ya madini katika maeneo ya Geita, Mara, Mwanza, Chunya, Kahama na Arusha kumekuwa na ongezeko la leseni 308 kutoka leseni 696 za biashara ya madini kabla ya ukaguzi wa kimkakati kufikia leseni 1004, huku ongezeko hilo likitajwa kuchangiwa na kuimarika kwa utendaji wa Tume ya Madini.

Vilevile, aliitaja Maabara ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) na kueleza kwamba, ilipata ITHIBATI ya Kimataifa ya uchaguzi wa sampuli za dhahabu kwa ya tanuru kutoka Shirika la SADCAS na kueleza kwamba, itasaidia sampuli zinazopimwa katika maabara za taasisi hiyo kuweza kuaminika kimataifa na kuruhusu upimaji wa sampuli kutoka nje ya nchi na kupunguza gharama za uchunguzi wa sampuli zetu nje ya nchi.

Naye Waziri wa Madini, Doto Biteko, aliieleza kamati hiyo kuwa wizara ipo katika mchakato wa kuandaa andiko la kuanzisha Bodi ya Kusimamia Wajiolojia nchini ambayo inalenga katika kudhibiti wajiolojia wanaotoa taarifa zisizo sahihi kuhusu tafiti za madini nchini.

Aidha, Waziri Biteko aliishukuru kamati hiyo kwa pongezi na kuendelea kuishauri na kueleza kuwa, mafanikio hayo yanatokana na kujituma kwa watumishi wa wizara na taasisi zake ikiwemo msukumo mkubwa unaotolewa na Rais Magufuli kwa sekta hiyo.

Aidha, ametumia fursa hiyo kuwataka wadau wa madini nchini kutekeleza shughuli zao kwa kufuata Sheria na taratibu zilizowekwa na kueleza kuwa, wizara inataka kuona wafanyabiashara wanafanya biashara zao bila kukamatwa kamatwa huku akisema kuwa, wizara itaendelea kuboresha mazingira ya biashara na shughuli za madini kuwawezesha Watanzania zaidi kushiriki na kumiliki uchumi wa madini.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Prof. Simon Msanjila, alieleza kamati hiyo kuwa katika mkakati wa kuwaendeleza watumishi na kuwajengea uwezo, jumla ya watumishi 12 na kuwa jana walitarajia kuelekea India kwa ajili ya kujifunza masuala ya jimolojia ambayo yanahusisha pia masuala ya utambuzi wa madini na uthaminishaji madini.

## HABARI KIMATAIFA

# Bondia Uingereza amsujudia Buhari

**LONDON,** Uingereza

BONDIA wa Uingereza, Anthony Joshua, alionekana akisujudu mbele ya Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari mjini London.

Joshua (pichani) ambaye historia yake inaonyesha anatoka Nigeria pia aliuambia umati uliokusanyika kwamba yuko tayari kusimama na Nigeria iwapo atahitajika.

**Rais Buhari yupo mjini London kwa mkutano wa uwekezaji ambao hufanyika kila mwaka ifikapo Januari 20.**

Picha za Joshua kusujudu zimetoa hisia tofauti katika mitandao ya kijamii huku wakosoaji wa Buhari wakikasirika kwamba Joshua hakuzungumzia kuhusu changamoto zinazowakabili vijana wa Nigeria.

Kupitia akaunti yake ya mtandao wa Instagram, Joshua aliandika kuwa: Ni kuhusu utamaduni na heshima kwa viongozi wetu".



Hata hivyo, watu wengi walimpongeza Joshua kwa kukumbuka historia alikotoka na kusujudu mbele ya Rais Buhari, ikiwa ni hali ya kitamaduni kuonyesha heshima kwa wakubwa.

Rais Buhari yupo mjini London kwa mkutano wa uwekezaji ambao hufanyika kila mwaka ifikapo Januari 20.

Picha za mkutano huo katika mji mkuu wa Uingereza pia zilichapishwa katika mtandao wa Youtube na kitengo cha habari nchini Nigeria.

Mmoja wa wasaidizi wa Buhari, Tolu Ogunlesi alichapisha picha ya mkutano huo katika mtandao wa kijamii wa twitter akiandika: "AJ!!! akiwa London na Rais". **BBC**



Maseneta nchini Marekani wakijiandaa kusikiliza mashtaka dhidi ya Rais Donald Trump. **PICHA: REUTERS**

## Vikundi vya kigaidi vyashambuliana Nigeria

**LAGOS,** Nigeria

MAPIGANO makali ya kufyatuliana risasi kati ya makundi mawili ya itikadi kali kaskazini mashariki mwa Nigeria yamesababisha wapiganaji wengi kuuawa.

Wapiganaji waliokuwa kwenye magari ya wazi kutoka tawi la Boko Haram ambalo ni tiifu kwa Abubakar Shekau walivamia kambi moja ya kundi hasimu linalojiita Dola la Kiislamu la Afrika Magharibi (ISWAP).

Inaelezwa kuwa hatua hiyo ilisababisha makubaliano makali ya risasi ambayo yalisababisha vifo vingi.

Wapiganaji wa Boko Haram waliishambulia kambi ya kijiji cha Sunnawa katika Wilaya ya Abadam karibu na mpaka na Niger.

Wanamgambo wa kundi la ISWAP awali waliwavamia Boko Haram katika eneo la Diffa lililoko jirani ya Nigeria ambako waliwateka nyara wanawake 13. DW

# Tshisekedi atishia kufukuza mawaziri

**KINSHASA,** DRC

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Félix Tshisekedi, ametishia kuwafuta kazi mawaziri wake na hata kulivunja bunge, iwapo washirika wake wa kisiasa ambao wanaegemea katika mrengo wa Rais wa zamani wa nchi hiyo, Joseph Kabila, wataendelea kumdharau.

Rais Tshisekedi alisema kuna baadhi ya mawaziri ambao wamekuwa wakimwambia kuwa, wanapata shinikizo, na kusisitiza kuwa, hana nia ya kulivunja bunge lakini, iwapo mzozo utazuka, atalazimika kufanya hivyo.

"Ninayoyasema ndio ambayo yatafanyika na ambayo nimedhamiria kufanya ndio yatakayotekelezwa, sababu raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo wamenipa jukumu la kuwaongoza na bila shaka wataniuliza nini nimewafanyia kwa muda wa miaka mitano," alisema Tshisekedi na kuongeza:

"Wamenipa taabu sana wanasubiri nishindwe kutimiza kazi yangu, wananisukuma kufanya mambo ambayo sijapanga kufanya, kama ni kuvunja bunge naweza kulivunja, na kama itabidi nifikie hatua hiyo sitachelewa kufanya hivyo," alisema Tshisekedi.

Katika hatua nyingine, Tshisekedi ametupilia mbali madai ya kuwapo mpango wa kuigawa nchi hiyo, akisema mazungumzo hayo hayana msingi na ni mbinu za kutaka kuchelewesha ajenda ya maendeleo kwa taifa hilo.

Aidha, alisema anashangazwa na namna ambavyo baadhi ya watu wanataka kulikuza suala la kuigawa vipande nchi hiyo, kiongozi huyo akisisitiza kuwa hakuna atakayejaribu kufanya hivyo.

Matamshi yake yamekuja baada ya majuma kadhaa yaliyopita baadhi ya wanasiasa kuzituhumu nchi za ukanda na baadhi ya wanasiasa wa DRC kutaka kuligawa eneo la mashariki mwa nchi hiyo.

Rais Tshisekedi ambaye amekuwa madarakani kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa, aliingia katika maelewano na chama cha zamani cha Rais Kabila cha PPRD, kushirikiana naye katika serikali yake, baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2018. **RFI**

## Wamkamata, wamwachia Besigye

**KAMPALA,** Uganda

JESHI la Polisi nchini Uganda limemwachia huru mwanasiasa wa upinzani nchini humo, Kizza Besigye baada ya kumzuia kwa saa kadhaa katika kituo cha polisi cha Nalufenyaa baada ya kukamatwa mjini Jinja akifanya mkutano.

Kabla ya kukamatwa, kwa saa kadhaa Besigye na wafuasi wake walikabiliana na polisi ambao walikuwa wakitumia mabomu ya machozi na maji ya kuwasha kukabiliana na wafuasi wake.

Kupitia ukurasa wake wa kijamii wa mtandao wa Twitter, Besigye aliweka picha zinazoonyesha namna polisi walivyotumia nguvu kuwakabili wafuasi wake wakati akijiandaa kwa mkutano wa maadhimisho ya miaka 15 tangu kuundwa kwa chama cha FDC. **RFI**

# Magufuli aahidi uchaguzi huru, haki mwaka 2020

**Na Salome Kitomari**

RAIS John Magufuli, amesema Serikali imejipanga kuhakikisha uchaguzi mkuu wa mwaka huu utafanyika katika mazingira ya amani, huru na haki.

Aidha, amesema taasisi na asasi mbalimbali zitakaribishwa kuja kuangalia Tanzania inavyokomaa katika demokrasia.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana wakati wa halfa ya sherehe za Mwaka Mpya 2020 kwa mabalozi na wawakilishi wa kimataifa iliyofanyika Ikulu, jijini Dar es Salaam.

Rais aliwashukuru mabalozi wa mataifa, taasisi za kimataifa kwa ushirikiano mkubwa uliwezesha kupatikana kwa mafanikio na maendeleo kwa Watanzania kwa miaka mitano sasa, na kuwaomba kuendeleza ushirikiano na uhusiano uliopo.

Aidha, aliwasihi kuendelea kuunga mkono jitihada za kuleta maendeleo nchini. Alisema uhusiano umeimarika baina ya Tanzania, mashirika na taasisi mbalimbali, na kwamba walitembelea nchi mbalimbali na kufungua balozi mpya saba.

Alisema wataendelea kufanya maboresho kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo mazingira ya kufanya biashara.

"Nawaomba muwashawishi wafanyabiashara kutoka kwenye nchi zenu kuja kuwekeza Tanzania, ni mahali pazuri pa kufanya biashara," alisema.

Aidha, alisema serikali itaendelea kufungua balozi mbalimbali, kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwamo la kuwahudumia wakimbizi.

Aliishukuru Jumuiya ya Kimataifa kwa kuunga mkono urejeshaji wa wakimbizi makwao, na kwamba Serikali inasikitishwa kwa hujuma na propaganda zinazofanywa kwa lengo la kukwamisha suala hilo.

Rais alieleza mafanikio mbalimbali yaliyopatikana toka aingie madarakani mwaka 2015.

Alisema tathmini ya zaidi ya miaka minne ambayo serikali imekuwapo madarakani, serikali kwa kutumia dira ya taifa ya maendeleo na ilani ya CCM ya mwaka 2015-2020 na mipango ya kitaifa na kikanda, iliandaa mpango wa taifa wa maendeleo wa miaka mitano.

Alisema mpango huo lengo ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi na watu na kuhakikisha rasilimali za taifa zinatumika vizuri.

Alisema kuimarishwa kwa shughuli za kilimo kumesaidia ukuaji wa uchumi na kushuka kwa mfumuko wa bei.

Kwa mujibu wa Magufuli, kati ya 2015 viwanda vipya 4,877 vimejengwa na baada ya marekebisho ya sheria ya Madini mwaka 2017, makusanyo yaliongezeka, na kwamba mauzo ya dhahabu yaliongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 1.469 hadi 1.743 mwaka 2018/19. Pia, mapato ya serikali Sh. bilioni 168/ 346 mwaka 2018. 19.

Aidha, alisema idadi ya watalii imeongezeka kutoka milioni 1.1 mwaka 2015 hadi milioni 1.5 mwishoni mwa mwaka 2018, na kwamba idadi hiyo iliongeza mapato kutoka Dola za Marekani bilioni 1.9 hadi bilioni 2.488 kwa kipindi hicho.

Kwa upande wa miundombinu ni barabara, madaraja, reli ya kisasa, kukarabati meli na miundombinu ya reli, nishati ya umeme, usafi wa anga umeimarisha na kufufua Shirika la Ndege (ATCL) vitajengwa viwanja 12 vyenye hadhi ya kimataifa.

Wasafiri wa usafiri wa anga wameongezeka kutoka milioni 4.8 hadi milioni 5.8 mwaka 2018.

Alisema maeneo mengine ni kuimarisha huduma za kijamii kama za afya, elimu na maji, ikiwamo kuongeza tiba na kuimarisha huduma za magonjwa makubwa na kuunguza kupeleka wagonjwa wengi nje ya nchi.

Alisema Sh. trilioni 1 zimetumika kugharamia elimu bure na mikopo ya elimu ya juu imeongezeka kutoka Sh. bilioni 341 mwaka 2015 hadi bil 450 mwaka huu.

Rais Magufuli alisema miradi ya maji imetekelezwa yenye thamani ya Sh. trilioni 3 na kwa sasa upatikanaji wa maji ni asilimia 84 kwa mjini na asilimia 64 vijijini.




Kaimu Meneja wa NMB Kanda ya Kusini, Haji Msingwa, akimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema (katikati), viti na meza vilivyotolewa na NMB kwa ajili ya Shule ya Sekondari Magingo ya wilayani Songea, Ruvuma. Anayeangalia kulia ni Meneja wa NMB Madaba, Esther Kiwona. Habari Uk. 8. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Wapewa mafunzo ubora wa bidhaa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WATU 5,302 katika Wilaya za Kakonko, mkoani Kigoma, Urambo mkoani Tabora na Dodoma, wamepatiwa elimu kuhusu faida za viwango, umuhimu wa kutumia bidhaa zilizothibitishwa ubora pamoja na fursa zinazopatikana Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Huo ni mkakati wa shirika hilo wa kukuza kwa jamii hatua itakayosaidia kuondoa bidhaa zisizo na ubora kwenye soko la Tanzania.

Ofisa Masoko wa TBS, Rhoda Mayugu, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki kuhusu majumuisho ya kampeni ya kueneza elimu ya viwango kwa wananchi katika mikoa hiyo mitatu ya kanda ya kati.

Alitaja kundi la kwanza kuwa lilikuwa na wanafunzi, la pili la wajasiriamali na tatu la wananchi na kwamba kati ya waliopata elimu hiyo wanafunzi ni 4,227, wajasiriamali 75 na wananchi 1,000.

Mayugu alisema kwa wanafunzi elimu hiyo ilitolewa shuleni pamoja na kwa wananchi na wafanyabiashara walifuatwa wanapoendeshea shughuli zao ikiwamo kwenye masoko na minadani.

Wajasiriamali katika mikoa hiyo mitatu, alisema walipatiwa elimu kuhusiana na utaratibu kuthibitishiwa ubora wa bidhaa wanazozalisha.

Alisema wajasiriamali hao wanathibitishiwa bure bidhaa zao na kupatiwa alama ya ubora na shirika hilo kwani gharama zote wanalipiwa na serikali kwa miaka mitatu.

"Wale waliopata elimu hiyo wameahidi kuthibitisha ubora wa bidhaa wanazozalisha ili kupanua soko lao," alisema Mayugu.

Pia Mayugu alisema wajasiriamali na wananchi kwa ujumla walielimishwa kuhusiana na mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2019 ambayo yameleta mabadiliko katika Sheria ya Viwango Na: 2 ya mwaka 2009.

Kwa mujibu wa Mayugu kutokana na mabadiliko hayo, majukumu ya kuthibitisha ubora na usalama wa chakula na vipodozi ambayo awali yalikuwa chini ya iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) sasa yanafanywa na TBS.

# Mabula ataka kasi upimaji ardhi

**Na Munir Shemweta,** KIGOMA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amezitaka halmashauri nchini kupanga, kupima na kumilikisha ardhi ili kuepuka migogoro na kuongeza mapato ya serikali kupitia kodi ya pango la ardhi.

Dk. Mabula alitoa agizo hilo juzi mkoani Kigoma wakati akizungumza na watumishi wa sekta ya ardhi wa halmashauri nane za mkoa huo akiwa katika ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi.

Ziara hiyo anafanya katika halmashauri za Buhigwe, Kasulu, Mji Kasulu, Kakonko, Kibondo, Kigoma, Manispaa Ujiji/Kigoma na Uvinza.

Alisema, wakurugenzi wa halmashauri wanapaswa kutambua kuwa wana jukumu la kusimamia halmashauri zao, ili ziwe na miji yenye mpangilio mzuri huku akibainisha kuwa kama maeneo ya miji hiyo yataachwa bila kupangwa, kupimwa na kumilikishwa yatakuwa ovyo na mengi kuingia kwenye urasimishaji.

"Halmashauri zote nchini jukumu la kupanga miji ni lenu. Wizara itasimamia nidhamu na ajira na mkizubaa katika hili miji itaendelea kuwa mibaya na serikali haitaki kuona ujenzi holela ukiendelea," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, urasimishaji unaofanyika sasa katika maeneo mbalimbali umesababishwa na kasi ndogo ya upangaji miji unaofanywa na halmashauri na kinachofanyika katika jambo hilo ni ni huruma ya Rais John Magufuli kwa wananchi na kubainisha kuwa mwisho wa wake ni mwaka 2023.

Alisema, hata idadi ndogo ya hati zilizotolewa katika Halmashauri za Mkoa wa Kigoma ni ishara ya kasi ndogo ya upangaji na upimaji katika mkoa.

Naibu Waziri Mabula alishangazwa na Halmashauri za Wilaya za Kigoma na Kasulu kwa kushindwa kutoa hata hati moja katika kipindi cha nusu mwaka huku Buhigwe ikitoa hati sita tu, hivyo kuutaka mkoa kuzisimamia ili kupanga, kupima na kumilikisha maeneo mengi zaidi.

Mabula pia alionyeshwa kutofurahishwa na kasi ya ukusanyaji mapato ya kodi ya ardhi katika mkoa wa Kigoma. Kwa kipindi cha nusu mwaka 2019/20 halmashauri za mkoa huo zimekusanya Sh. 312,233,500.9 sawa na asilimia 13 tu huku Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na Kasulu zikiwa zimekusanya mapato ya ardhi chini ya asilimia 1.2. Halmashauri pekee iliyofanya vizuri ni Kakonko iliyokusanya Sh. 17,281,142.59 sawa na asilimia 28.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi **piga 0758 112 332. Karibu EFL**.

**TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSITUTE:** Inatangaza mhula mpya wa masomo Certificate na Diploma za kilimo na maendeleo ya jamii.maelezo zaidi tembelea tovuti yetu www.tracdi.ac.tz Simu:**0714404491/0746995144**

**WAHUDUMU WA HOTELI WANAHITAJIKA,** Hoteli ndogo Bagamoyo inatafuta wahudumu, wapishi, usafi, bartender wenye vyeti. **Piga 0757 129 546.**


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO


### TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA TREKTA

KIDUMU INVESTIMENT LTD ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA TREKTA AINA YA MASSEY FEGUSON 165 YENYE NAMBA ZA USAJILI T 817 ABB KWA YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

TAARIFA YA POLISI
KHM/RB/10/2020

215592502

### KUPOTEA KWA KADI

Goldermeir Samwel Shoo anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya Landcruiser Prado yenye namba ya usajili T131 CTS iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochocte cha Polisi.

Polisi Taarifa:
DAR/OST/RB/6218/2020

215592602

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**PHILMON LUBASHA.** Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC.484 AZB** aina ya **SAN-LG** Yeyote akayeiona atoe taarifa kituo cha Poilisi Taarifa ya polisi.

**MAJ/RB/TR/28/2020.**

115593902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**CHAMWINO MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;06/2020**

**Ombi la OLIMPA EZEKIEL KUSSAGA**
**Kuteuliwa msimamizi wa mirathi**
**marehemu RIZIKI.A.MAHUNDI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 23/01/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 17/01/2020

Sahihi ya Hakimu,
RESIDENT MAGISTRATE
MOROGORO

215593002

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Kiatika mahakama mwanzo MJINI TANGA
USIMAMIZI WA MIRATHI NAMBA 169/2019

OMBI LA HALIMA ALLY NASSORO KUTEULIWA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHMU RAJABU ABDALLAH RAJABU
KWA YEYOTE ANAYE HUSIKA

WATU WOTE WANAODAI KWA WANA NA UHUSIHANO WOWOTE NA MIRATHI YA MAREHEMU HUYO WANAALIKWA WANAALIKWA KUJA NA KUHUDHURIA KESI WAKITAKA MNAMO TAREHE 07/02/2020

KABLA HUYO MUOMBAJI HAJATEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI HIYO

WOSIA WA MAREHEMU HUYO UPO MAHAKAMNI WAWEZA KUKAGULIWA TAREHE 20/01/2020

5593502


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi

Kwa Bei Poa

Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO




# MADRID WAMSAJILI NYOTA WA FLAMENGO

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imekamilisha usajili wa kinda wa Brazil, Reinier Jesus kutoka Flamengo.

Mshambuliaji huyo alikuwa akihusishwa na usajili huo unaotajwa kuwa wa thamani ya euro milioni 30, huku awali iliripotiwa kwamba angesajiliwa wakati atakapofikisha umri wa miaka 18, Januari 19.

Ujio wa Reinier ulithibitishwa Jumatatu, na amesaini mkataba wa miaka sita na nusu kukaa hapo kwenye dimba la Santiago Bernabeu. Alifunga mabao sita katika mechi 14 alizoichezea Flamengo kwenye Ligi Kuu ya Brazil, maarufu kama Serie A, mwaka jana.

Wakati wake wa kucheza kwa kipindi kifupi kwenye timu ya wakubwa ya Flamengo, Reinier ametwaa taji la Brasileiro na Copa Libertadores. Alikuwa pia kwenye kikosi cha Flamengo ambacho kilifungwa na Liverpool kwenye fainali ya Klabu Bingwa ya Dunia.

Kiungo huyo mshambuliaji mwenye mbinu, ufundi, ubunifu na nguvu, Reinier alikuwa pia akihusishwa na klabu kadhaa za Ulaya baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia kwenye michuano ya Mataifa ya Amerika Kusini chini ya umri wa miaka 17.

# Arteta akubali Arsenal kutosajili Januari hii

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amejiandaa kwa uwezekano wa Arsenal kutosajili wachezaji wapya mwezi huu baada ya kubainisha hakuna mazungumzo yanayoendelea kwa siku za hivi karibuni.

Arsenal wapo nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England wakiwa na pointi 29, wakipitwa alama 10 na Chelsea waliopo nafasi ya nne, na kuwaacha 'Washika Bunduki' hao wa London katika hatari ya kukosa kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao na pengine hata kwenye Ligi ya Europa.

Tangu kocha mpya, Arteta achukue mikoba ya kuinoa klabu hiyo mwezi uliopita, Arsenal imekuwa ikihusishwa na wachezaji kadhaa kutaka kuwasajili, hasa wakati huu wakiwa wanakabailiwa na majeruhi wengi.

Nyota wa Paris Saint-Germain, Layvin Kurzawa, Thomas Lemar wa Atletico Madrid na beki wa Bayern Munich, Jerome Boateng wamekuwa wakitajwa kuhusishwa na mpango wa kwenda pale kwenye Dimba la Emirates.

Lakini Arteta anaona uwezekano huo ni mdogo kwa Arsenal kuingia sokoni kwa sasa.

Wakati alipoulizwa kama Arsenal pengine watamsajili yeyote mwezi huu, Arteta alisema: "Pengine kuna uwezekano. Hakuna chochote kinachoendelea kwa sasa tangu wikendi iliyopita."





# *Neville ataka Woodward aondoke Man U*

**MANCHESTER,** England

GARY Neville amesema kikosi cha Manchester United ni "kisichosameheka" kwa kile kinachoendelea pale kwenye dimba la Old Trafford na amemtaka Makamu Mwenyekiti Mtendaji, Ed Woodward (pichani) kuondoka.

United walifungwa na wapinzani wao, Liverpool Jumapili na sasa wamepitwa pointi 30 na vinara hao, ambao wanakaribia kulibeba taji hilo kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 30.

Neville, ambaye alishinda mataji nane ya Ligi Kuu akiwa pale United chini ya Kocha Alex Ferguson, ameonyesha hasira kwa hali inayoendelea ndani ya klabu hiyo kwa sasa na anaamini ni muda muafaka kwa familia ya Glazer inayomiliki klabu hiyo kuchukua maamuzi.

Alisema: "Siamini uwekezaji uliowekwa kwenye kikosi kwa miaka mitano, sita na saba na unakuwa na matokeo kama haya dimbani.

"Siwezi kubadili umiliki wa United, hakuna anayeweza. Nashindwa kuelewa kwa nini wamiliki wanasita kuchukua maamuzi ya haraka."Kwa uhakika mambo yanavyokwenda yanatia hasira kubwa na hali hii haiwezi kuvumiliwa kwa muda mrefu zaidi."

HABARI MICHEZO

# Inter Milan yathibitisha kutuma ofa ya Eriksen

**MILAN,** Italia

INTER Milan imepeleka ofa kwa Tottenham kwa ajili ya kumsajili kiungo wa kimataifa wa Denmark, Christian Eriksen, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo ya Italia, Piero Ausilio.

Eriksen ameingia kwenye miezi yake sita ya mwisho kwenye mkataba wake na Spurs huku yeye mwenyewe akitaka kuondoka, na Inter kwa muda mrefu imekuwa ikihusishwa kutaka kumsajili.

Inter ilionyesha wazi kabisa nia yake ya kumsajili nyota huyo wakati Ofisa Mtendaji wa klabu hiyo, Giuseppe Marotta alipoonekana akiwa na wakala wa Eriksen, huku Ausilio awali alisema ana uhakika wa dili hilo kufanikiwa.

Jambo hilo likamfanya kocha Jose Mourinho, kuishutumu klabu yake hiyo ya zamani kwa kutoonyesha heshima – huku Inter wakisistiza hawajafanya jambo lolote baya.

Lakini sasa Inter wanaonekana wamechukua hatu zaidi, huku Ausilio akithibitisha kwamba, ofa imetolewa.

Akizungumza na Sky Sport Italia, Ausilio alisema: "Tumetoa ofa rasmi kwa Tottenham kwa ajili ya kumsajili Christian Eriksen na sasa tunasubiri.

"Klabu nyingi zinamwania, lakini sisi tunajiamini, tunajaribu kumpata mchezaji kama Eriksen."

Ausilio pia alibainisha kwamba, klabu hiyo imefikia makubaliano na Chelsea kwa Victor Moses baada ya Frank Lampard kuthibitisha kuwa muda wa Mnaigeria huyo kucheza kwa mkopo kule Fenerbahce umeisha na kwamba wanaangalia wapi anapokwenda.





# GUADIOLA AKERWA UEFA KUTAKA KUONGEZA MECHI

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anaamini siku 400 au 500 kwa mwaka zitailazimu Ligi ya Mabingwa Ulaya kupanuliwa kwa sababu Klabu za Ligi Kuu ya England tayari zina mechi nyingi sana za kucheza.

Chama cha Klabu za Ulaya (ECA), na Shirikisho la Vyama vya Soka Ulaya vipo kwenye mazungumzo ya kuongeza mechi nne zaidi za Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo matokeo yake watakaoingia fainali watalazimika kucheza mechi 17.

Hata hivyo, huku City jana Jumanne walikuwa wanacheza na Sheffield United ukiwa ni mchezo wao wa nane ndani ya wiki tatu na nusu, Guardiola anaona kwamba timu za England zitakuwa na mzigo mkubwa zaidi.

"Nafikiri suluhisho ni kuufanya mwaka uwe na siku 400, hilo ndilo suluhisho. Kuongeza siku 400 au 500. Baada ya hapo tunaweza kuongeza mashindano mengine. Pengine UEFA au FIFA wanaweza kuzungumza kuhusu hilo. Tuna siku chake kwa mwaka, hili ndio tatizo," alisema Guardiola.

Kuongezwa kwa mechi za Ligi ya Mabingwa Ulaya, kunaweza kuwa na matokeo hasi kwa michuano ya Kombe la EFL la nchini England.

# *Mbappe: Liverpool hii inacheza kama mashine*

**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, ameielezea Liverpool kama "mashine" wakati huu wakiwa kwenye mbio za kuwania kulitwaa taji lao la kwanza la Ligi Kuu ya England tangu mwaka 1990, na ameiambia BBC Sport ana furaha kwa asilimia "100%" kwa miamba hao wa Ufaransa wakati uvumi ukizidi kumhusisha na kwenda Real Madrid.

Liverpool pia imekuwa ikihusishwa na Mbappe - ambaye anachukuliwa na wengi kama ndiye mchezaji bora kijana duniani licha ya kocha, Jurgen Klopp kusema bei ya mshambuliaji huyo iko nje kabisa ya hali halisi.

Na wakati mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwenye umri wa miaka 21, ambaye alijiunga na PSG mwaka 2017 kwa ada ya thamani ya pauni milioni 165.7, alithibitisha kwamba kwa sasa ana furaha na klabu yake hiyo wakati akizindua mfuko wake wa hisani wa 'Inspired by Kylian Mbappe (IBKM)' akasema anaziangalia mbio za ubingwa za Liverpool kama zinazomvutia.

"Kile wanachofanya Liverpool kwa wakati huu ni chakufurahisha," alisema Mbappe. " Wako kama mashine.

"Hawajapoteza mchezo. Ukiwaangalia unaweza kusema kila kitu ni rahisi, lakini si rahisi kihivyo. Jamaa wamejipanga, wanacheza mechi kila baada ya siku tatu na wanashinda, wanashinda, wanashinda.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LAMPARD AMTAJA CAVANI CHELSEA

## ●●● Kuleta mchezaji mzoefu ni kitu ambacho siwezi kukiweka mbali kwa sababu nadhani...

**LONDON** England

FRANK Lampard amemtaja mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Edinson Cavani, lakini akasisitiza Chelsea haipo karibu kuongeza straika mwingine.

**Kocha huyo wa Chelsea, Lampard amekuwa akifunguka kwamba 'Blues' – ambayo imefutiwa kifungo cha usajili katika dirisha hili la Januari, itasajili tu kama dili la mpango huo litakuwa sahihi kwa klabu.**

Hata hivyo, baada ya mechi ya Jumamosi kukumbana na kipigo cha bao 1-0 nyumbani kwa Newcastle United, Lampard alikiri Chelsea inahitaji kuimarishwa katika theluthi ya mwisho na kwamba watakuwa wakitazama uwezekano wa kufanya biashara kama ikiwezekana mwezi huu.

Cavani anataka kuondoka PSG baada ya kujikuta akiangukia kuwa nyuma ya Mauro Icardi kwenye kikosi cha kwanza cha Thomas Tuchel, ingawa ofa yake kutoka Atletico Madrid imekuwa ikikataliwa.

Lampard alizungumza kuhusu matamanio yake kwa Cavani, lakini akaweka wazi kuwa hajakaribia kumwongeza katika kikosi chake.

"Yeye ni mchezaji mzuri, nilicheza dhidi yake na kila wakati nilikuwa napenda mawazo na mtazamo wake na ni wazi rekodi yake ya ufungaji mabao inajielezea yenyewe," Lampard alimzungumzia Cavani wakati wa mkutano na wanahabari Jumatatu.

"Sijui kabisa ni vipi suala lake lilivyo, hivyo tutaona. Ni mchezaji mzoefu lakini kuna wachezaji wengine wengi pale.

"Tu wachanga kama kikosi, tunajua kuhusu mpito, hivyo kuleta mchezaji mzoefu ni kitu ambacho siwezi kukiweka mbali kwa sababu nadhani wachezaji makinda mara nyingine wanahitaji msaada na kama hilo ndivyo lilivyo, litatusaidia.

"Nadhani [wa] muda mrefu kwa Januari ni vigumu. Hatujaona wengi. Nadhani ni vigumu hivyo [wa] muda mfupi pengine ni kitu tunachokitazama kwa sababu nadhani kuna mambo yanayotoa msukumo kwa msimu huu kumaliza sehemu tunayoitaka.

"Tunatazama, lakini hakuna cha kukueleza ambacho kinaweza kutokea mara moja."

Lampard amesisitiza Chelsea haitakuwa na haraka ya kufanya dili lolote, wakati akiongeza hakuna taarifa zaidi kuhusu uwezekano wa kuondoka kwa Olivier Giroud na Victor Moses.

## ZISIKUPITE

### INTER YAMKOMALIA ERIKSEN

INTER Milan itaipa Tottenham ofa ya pauni milioni 12.8 pamoja na nyongeza ili kumsajili kiungo Mdenmark Christian Eriksen, 27, mwezi huu. ***(Guardian)***

### DEMBELE KUMRITHI RASHFORD

MANCHESTER United wamejiunga katika ofa ya pauni milioni 43 kwa mshambuliaji wa Lyon, Mfaransa Moussa Dembele, kufuatia Marcus Rashford kukumbwa na majeraha. ***(Foot Mercato, via Manchester Evening News)***

### WERNER ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL ni lengo la mshambuliaji wa RB Leipzig na Ujerumani, Timo Werner, 23, ambaye anataka kwenda kukipiga Ligi Kuu England. ***(Bild, via Sport Witness)***

### FERNANDES AWEKEWA NGUMU

KOCHA msaidizi wa Sporting Lisbon, Emanuel Ferro amekanusha matarajio ya kiungo Mreno Bruno Fernandes, 25, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United, kuondoka klabuni hapo Januari hii. ***(A Bola, via Mirror)***

### VAN PERSIE AIONYA UNITED

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Arsenal na Manchester United, Robin van Persie ameionya United kutomharakisha straika Marcus Rashford, 22, kurejea dimbani kufuatia kukumbwa na majeraha. ***(Manchester Evening News)***

### ZAHA AITULIZA PALACE

WINGA wa Crystal Palace, Wilfried Zaha ameiambia klabu kuwa yupo tayari kubaki kwa kipindi kilichobaki msimu huu, wakati kukiwa hakuna klabu ambayo ipo tayari kufika thamani yake ya pauni milioni 80 inayotakiwa na miamba hiyo ya Selhurst Park kwa nyota huyo wa kimataifa wa Ivory Coast. ***(Mail)***

### AHAKIKISHIWA ULAJI UNITED

KIBARUA cha Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer kipo salama hata kama itashindwa kufuzu kushiriki michuano ya Ulaya kwa msimu ujao. ***(Sun)***

### HOLGATE AZUIWA EVERTON

EVERTON imekataa ofa mbili kwa beki wao, Muingereza Mason Holgate, wakati Newcastle United, Bournemouth na Sheffield United ni miongoni mwa timu zinazovutiwa na huduma ya mchezaji huyo. ***(Football Insider)***

### MOSES KUMFUATA CONTE INTER

INTER Milan inakaribia kukamilisha dili la mkopo kwa winga wa Chelsea, Victor Moses, 29, kumuunganisha na kocha wake wa zamani, Antonio Conte. Fenerbahce, klabu ambayo mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria haitamzuia kuondoka. ***(Mail)***

### AWEKEWA NGUMU LIVERPOOL

LIVERPOOL haipo tayari kumuacha kiungo wa kimataifa wa Uswisi, Xherdan Shaqiri, 28, kuondoka klabuni hapo mwezi huu huku kukiwa na taarifa ya Roma kuvutiwa naye. ***(Sky Sports)***

### UNITED KUMGEUKIA VECINO

MANCHESTER United imejiunga katika mbio za kumsajili kiungo wa Inter Milan na Uruguay, Matias Vecino, 28, kama uwezekano wa mbadala wa Bruno Fernandes ikitokea kumkosa. ***(Sky Italy, via Mirror)***

## HABARI MICHEZO

# ZFF kugeukia mikataba ya wachezaji

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

Mkurugenzi wa Mashindano wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Ali Mohmmed, amesema ipo haja sasa kwa wachezaji kuhakikisha wanawasilisha mikataba yao ili kuepusha usumbufu kipindi cha usajili wa wachezaji wakati wa dirisha dogo na kubwa.

Akizungumza na gazeti hili, alisema kuwapo kwa kopi ya mkataba katika Ofisi za ZFF, kutasaidia kupunguza migogoro pale mchezaji anapohama timu moja kwenda nyingine.

Alisema katika kipindi hiki cha upitishaji fomu za usajili wa dirisha dogo, changamoto hiyo imejitokeza kwa wachezaji wengi ambao wanataka kuhama klabu zao huku timu anayotoka wakikataa kumtoa mchezaji husika kwa madai bado wana mkataba naye.

Aidha, alisema ni vema kwa wachezaji kuwa makini na kuisoma mikataba ya timu kabla ya kujaza ili kupunguza migogoro mingi ya kugombania mchezaji kati ya klabu na klabu jambo ambalo halipendezi katika soka la sasa.

"Wachezaji wengi hawana utamaduni wa kutunza mikataba yao au hata kuomba kopi ya mikataba pale wanaposaini katika jambo linalosababisha migogoro kati ya timu anayotoka na anayohamia," alisema.

Alisema kwa upande mwingine zipo klabu ambazo si waaminifu ikiwamo kufoji mikataba ya wachezaji ambao tayari muda wa kubaki katika timu husika umemaliza na kumwongezea miaka mingine ili aendelee kuitumikia pasipo kumshirikisha mchezaji husika, hivyo kuwasilisha ZFF nakala ya mikataba ya wachezaji kutasaidia kuepuka wajanja kama hao na migogoro isiyo na maana.



Meneja wa Bia ya Kilimanjaro, Pamela Kikuli, akizungumza na wageni waalikwa pamoja na waandishi wa habari (hawapo pichani), wakati wa uzinduzi wa Kilimanjaro Marathon uliofanyika mwishoni mwa wiki Moshi, mkoani Kilimanjaro. **NA MPIGAPICHA WETU**

# AZAM KUMKOSA CHIRWA IKIIVAA MWADUI FC LEO

**Na Shufaa Lyimo**

AZAM FC itashuka katika dimba la Kambarage mkoani Shinyanga leo kuivaa Mwadui FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara bila uwapo wa straika wao, Obrein Chirwa kutokana na kuumia kifundo cha mguu, imeelezwa.

**Akizungumza na Nipashe jana, daktari wa klabu hiyo, Mnandi Mwankemwa, alithibitisha Chirwa kukosa mchezo huo wa leo ambao wanawania pointi tatu muhimu ili kupunguza wigo dhidi ya Simba.**

Simba iliyoshuka dimbani mara 16 msimu huu, ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 41 wakati Azam FC ambayo imeshacheza mechi 15 ipo nyuma yake ikiwa na alama 32.

Daktari huyo wa Azam FC, alisema mbali na Chirwa pia watamkosa Abdallah Kheri pamoja na Richard Djodi ambaye anasumbuliwa na misuli ya paja.

"Hali za wachezaji wa kikosi chetu ni nzuri isipokuwa wachezaji hao watatu ambao ni majeruhi," alisema Mwankemwa.

Kwa upande wa kocha msaidizi, Idd Chechen alisema kikosi chao kinaendelea vizuri kuelekea katika mchezo huo wa leo.

Alisema wataingia uwanjani kwa tahadhari katika mchezo huo, huku lengo lao likiwa ni kuvuna pointi hizo tatu ugenini.

"Kikosi kipo vizuri kuivaa Mwadui kesho [leo], kila mchezaji ana morali nzuri ili kuiweka mahali pazuri timu," alisema Cheche.

Aliwataka mashabiki wao kujitokeza kwa wingi kuisapoti timu ili itimize malengo waliojiwekea msimu huu.

Mwadui ipo katika nafasi ya 16 katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 17 baada ya kushuka dimbani mara 15 msimu huu.



Msanii maarufu wa filamu nchini Jacqueline Wolper (kushoto), akifuatiwa na mkongwe wa Bongo Fleva, Dully Sykes, Mkuu wa Kitengo cha Mauzo wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo (wa pili kulia) sambamba na Mkuu wa Kitengo cha Thamani kwa Wateja, Hilda Nakajumo wakati wa uzinduzi wa kampeni maalum ya DStv ya "Tia Kitu Pata Kitu", ambapo sasa mteja wa DStv akilipia kifurushi chake anapandishwa daraja na kupewa kifurushi cha juu zaidi bila gharama za ziada. Ofa hii ni kwa wateja wa DStv wa kifurushi cha Bomba, Family, Compact na Compact Plus. **NA MPIGAPICHA WETU**

# DStv yaja na 'Kitu Juu ya Kitu!

**Na Mwandishi Wetu**

Baada ya kuwashangaza wateja wake kwa punguzo kubwa la bei ya vifurushi vya DStv, Kampuni ya MultiChoice Tanzania imefungua mwaka kwa ofa ya aina yake, ambapo sasa mteja akilipia kifurushi chake huzawadiwa kifurushi cha juu yake bila malipo ya ziada, imeelezwa.

Ofa hii ambayo imepewa jina la "Kitu Juu ya Kitu" imeanza rasmi ambapo sasa mteja wa DStv akilipia kifurushi chake atapatiwa kifurushi cha juu yake bila gharama za ziada na hivyo kuweza kupata chaneli za kifurushi cha juu kuliko kile alicholipia.

Mkuu wa kitengo cha thamani kwa wateja wa MultiChoice Tanzania, Hilda Nakajumo, amesema ofa hiyo ni kwa wateja wote wa DStv kuanzia kifurushi cha Bomba hadi wale wa kifurushi cha Compact Plus.

"Ofa hii ni mahsusi kwa wateja wetu wa kuanzia kifurushi cha Bomba hadi Compact plus na kila mteja atakayelipia kifurushi chake atapandishwa daraja kwenda kifurushi cha juu yake ndani ya muda wa saa 48," alisema Hilda.

Akielezea zaidi kuhusu ofa hiyo jana jijini Dar es Salaam, alisema kwa mfano mteja wa kifurushi cha Bomba cha Sh. 19,000 akilipia kifurushi chake, moja kwa moja atapandishwa daraja na kupelekwa kifurushi cha Family cha Sh. 29,000 bila kulipia gharama za ziada.

Hilda alisema wakati wote MultiChoice Tanzania imekuwa kinara katika kuwapatia wateja wake wa DStv burudani kabambe kwa gharama nafuu na ndiyo sababu mwishoni mwa mwaka jana walishusha bei za vifurushi vyao hadi asilimia 36.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo, alisema ofa hii ni ya aina yake huku akitoa mfano kwa wapenda soka ambapo kwa mteja wa kifurushi cha Family cha Sh. 29,000 akilipia atapandishwa hadi kifurushi cha Compact cha Sh. 44,000 na hivyo kushuhudia ligi kubwa duniani ikiwamo michezo yote ya Ligi Kuu ya Uingereza bila kusahau La Liga, Serie A na michuano mingine mikubwa ulimwenguni.

# Michezo

Jumatano Januari 22, 2020

Nipashe




Lampard amtaja Cavani Chelsea HABARI UK.30

HAINA KUFELI...





Mshambuliaji wa Kimataifa wa Tanzania na Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, akisaini mkataba wa miaka minne na nusu wa kuitumikia Aston Villa inayoshiriki Ligi Kuu England usiku wa kuamkia jana, akitokea KRC Genk ya Ubelgiji. **Picha ndogo;** akionyesha jezi namba 20 atakayoitumia. **PICHA: MTANDAO**

## Mbelgiji Yanga ajifutua Singida

**Na Somoe Ng'itu**

MTATUSAMEHE! Wachezaji na viongozi wa Yanga wametoa kauli hiyo kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya wenyeji wao Singida United unaotarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa Liti (zamani Namfua) ulioko mkoani Singida.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, amesema kuwa mechi hiyo inatarajiwa kuwa ngumu kwa sababu kila timu inahitaji kujiweka sawa baada ya kufanya vibaya katika mechi zilizopita.

Eymael alisema anatarajia wachezaji wake wataongeza umakini katika mchezo huo na hatimaye kupata pointi tatu wanazoziwania ili kurejea katika ushindani wa kuwania taji la ligi hiyo msimu huu.

"Itakuwa mechi ngumu, hii ni ligi yenye ushindani, lakini tumejiandaa kukabiliana na changamoto yoyote itakayojitokeza, baadhi ya wachezaji ni wapya na ni mara yao ya kwanza katika mchezo huo wa ugenini, wameahidi kufanya vizuri," alisema Eymael.

Nahodha Msaidizi, Juma Abdul aliliambia gazeti hili kuwa wamejiandaa kwenda 'kufuta' makosa yaliyotokea katika mechi mbili zilizopita na hatimaye kurejea katika mbio za ubingwa kwa kasi.

"Napenda kuwaambia mashabiki wetu wasikate tamaa, kila kitu kimerekebishwa kuelekea mechi ya kesho (leo), Yanga itatengamaa na tutapambana kupata ushindi, bado kocha mpya alikuwa anakijenga kikosi, lakini kwa sasa tupo tayari kwa mapambano," alisema Abdul.

# Samatta apewa zigo kubwa

### ●●● Asema 'haina kufeli', Mwakyembe amtabiria kuwa 'Messi', TFF, Simba na Yanga watoa neno...

**Na Mwandishi Wetu**

MBWANA Samatta ana mzigo mkubwa wa kuhakikisha anainusuru Aston Villa katika wimbi la kushuka daraja baada ya juzi usiku kusaini mkataba wa miaka minne na nusu ya kuitumikia klabu hiyo ya Ligi Kuu England akitokea KRC Genk ya Ubelgiji kwa pauni milioni 10.

**Villa ambayo ipo nafasi ya 18 katika msimamo wa Ligi Kuu baada ya kushuka dimbani mara 23 ikishinda mechi sita, sare nne na kupoteza 13 hivyo kujizolea pointi 22, inahitaji msaada mkubwa wa Samatta katika upachikaji mabao kutokana na mshambuliaji wao tegemeo, Mbrazili Wesley kuumia ambapo atakuwa nje ya uwanja hadi mwishoni mwa msimu.**

Samatta, 27, ambaye hadi sasa msimu huu alishaifungia Genk mabao 10 katika mashindano yote ikiwa ni pamoja na bao dhidi ya Liverpool katika Uwanja wa Anfield kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, atakuwa na kazi ya kuongeza idadi ya mabao kwa Villa ambayo imesharuhusu nyavu zake kutikiswa mara 44 huku ikitupia 29 tu msimu huu.

Mshambuliaji huyo wa Tanzania, atakuwa akimtegemea zaidi nahodha wa Aston Villa na mpisha mkubwa wa mabao wa klabu hiyo, Jack Grealish kumlisha, ambaye kabla ya mechi ya jana dhidi ya Watford alikuwa na pasi za mwisho sita.

Kocha wa Aston Villa, Dean Smith aliiambia tovuti ya klabu hiyo: "Ni mwenye furaha kufanikiwa kumnasa Mbwana katika klabu hii.

"Amefunga mabao kipindi chote cha kazi yake na ninatazama mbele kufanya naye kazi."

Akizungumzia kutua kwake Aston Villa, Samatta ambaye ameifungia Genk jumla ya mabao 76 katika mechi 191 alizoichezea, alisema: "Ni mwenye furaha sana, ni hatua kubwa kwangu mimi katika wasifu wangu. Ni hatua kubwa kwa nchi yangu pia. Kila mmoja alikuwa akitazama kwa Mtanzania kucheza Ligi Kuu England.

"Ninajua mengi kuhusu Aston Villa. Nilikuwa nikitazama [rekodi za mfungaji wa Villa kwenye Ligi Kuu] Gabby Agbonlahor wakati akiwa hapa."

Nahodha huyo wa Taifa Stars amesema ilikuwa ni ndoto ya wote hususan Watanzania kuona anafanikiwa kusajiliwa na Klabu ya Ligi Kuu England.

Aidha, Samatta ambaye ana mabao 18 katika mechi 51 alizoichezea Taifa Stars, alisema ataendelea kupambana na kuhakikisha anapeperusha vema bendera ya Tanzania katika ligi hiyo maarufu na yenye kutazamwa na mashabiki mbalimbali wa soka duniani.

"Ilikuwa ndoto, asante Aston Villa kwa kuifanya ndoto hii kuwa kweli, ndugu Watanzania nawashukuru kwa maombi yenu, mapambano bado yanaendelea. Haina Kufeli," alisema Samatta ambaye amezaliwa Desemba mwaka 1992.

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Harrison Mwakyembe alisema serikali inahitaji kuona mshambuliaji huyo anapata mafanikio zaidi ya hayo ambayo amefikia sasa kwa sababu uwezo huo anao.

"Alipofika Samatta sio kilele cha mafanikio, tunahitaji kumuona anakuwa Messi wa dunia nyingine," Mwakyembe alisema na kufafanua kuwa heshima aliyofikia nyota huyo si ya kujengewa sanamu pekee.

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), lenyewe limempongeza nahodha huyo na kumtakia mafanikio zaidi katika kuendelea kupeperusha vema bendera ya nchi.

Katika taarifa yake ilisema kuwa linaamini ataendelea kuipambania kaulimbiu yake ya 'Haina Kufeli' ili kutimiza ndoto zake za kuwa mwanasoka gwiji zaidi duniani.

Klabu yake ya zamani ya Simba nayo imempongeza kwa kueleza: "Hongera sana Mbwana Samatta kwa hatua kubwa ambayo umepiga kwenye maisha yako ya soka. Wanasimba tunakutakia kila la kheri kwenye timu yako mpya ya Aston Villa."

Watani zao, Yanga nao wamempongeza Samatta kwa kusaini mkataba wa miaka minne na klabu hiyo ya England na kusema sasa milango ya wachezaji kutoka Tanzania itafunguka zaidi.

"Klabu ya Yanga inampongeza Mbwana Samatta kwa kujiunga na Aston Villa inayoshiriki Ligi Kuu England maarufu EPL," ilisema kwa kifupi taarifa ya klabu hiyo.

Samatta aliyepewa jezi namba 13, anakuwa mchezaji wa tatu kusajiliwa hapo Villa Park mwezi huu baada ya Danny Drinkwater na Pepe Reina kutoka Chelsea na AC Milan.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >